**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Kumi na Mbili - Tarehe 28 Juni, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kabla sijamwita mwuliza swali la kwanza niwataarifuni tu kwamba maswali ambayo yalikuwa yaulizwe jana kwa mujibu wa Kanuni ya 35, Spika atakuwa akiyaweka taratibu taratibu katika siku zijazo hadi maswali hayo yatakapoisha na mtaona katika *Order Paper* ya leo kuna maswali ya jana mawili ambayo yameingizwa katika orodha ya shughuli za leo zilizopo mbele yetu. Sasa moja kwa moja namwita Mheshimiwa Herbert Mntangi.

Na. 95

**Mapato Yanayotokana na Wilaya Kugawanywa**

**MHE. HERBERT MNTANGI** aliuliza:-

Kwa kuwa, kabla ya kuanzishwa kwa iliyokuwa Wilaya ya Muheza yenye majimbo ya Uchaguzi ya Muheza na Mkinga, Muheza ilikuwa katika Wilaya ya Tanga; na kwa kuwa, hivi sasa Mkinga imekuwa Wilaya kamili na Muheza kupata hadhi ya Mji Mdogo:-

(a) Je, kuna utaratibu gani wa kisheria unaosimamia ugawaji wa mali kwa Wilaya mbili baada ya Wilaya mama kugawanywa?

(b) Kama upo utaratibu wa aina hiyo. Je, iliyokuwa Wilaya ya Muheza ilipata mgao gani halali baada ya kutenganishwa na Wilaya ya Tanga?

(c) Je, ni utaratibu gani unaongojewa baada ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri kutoa ahadi ya Mji Mdogo wa Muheza ili kuwezesha kuundwa kwa Halmashauri ya Mji Mdogo wa Muheza ambao ndio Makao Makuu ya Wilaya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Tanga iligawanywa katika Wilaya mbili yaani Tanga na Muheza mnamo tarehe 1 Januari, 1974. Hakuna utaratibu wa kugawa mali kwa Wilaya mbili zilizogawanywa. Baada ya Wilaya mama kugawanywa mali zote za Wilaya ni mali za Serikali Kuu na zinasimamiwa na Wizara ya Miundombinu kwa niaba ya Serikali. Isipokuwa Serikali hutenga Bajeti kwa ajili ya ujenzi wa Miundombinu katika Wilaya mpya pamoja na vifaa vya kazi.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika jibu la sehemu (a), hakuna mgao uliofanywa wakati Wilaya ya Muheza ilipotenganishwa na Wilaya ya Tanga. Serikali tangu wakati huo imekuwa ikitenga Bajeti kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa Wilaya mpya ya Muheza.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu unaofuata baada ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kutoa hati ya Mamlaka ya Mji Mdogo wa Muheza ni kuunda rasmi kwa Baraza la Mamlaka chini ya Kifungu cha 45(1) cha Sheria ya Serikali za Mitaa namba 7 ya mwaka 1982 (Mamlaka za Wilaya) Sura 287.Wajumbe wa Baraza la Mamlaka ya Mji Mdogo ni kama wafuatao:-

(i) Mwenyekiti ambaye atachaguliwa na wajumbe wa Mamlaka kutoka miongoni mwa Wenyeviti wa Vitongoji vilivyomo katika eneo la Mamlaka husika.

(ii) Wenyeviti wa Vitongoji vyote vilivyomo katika Mamlaka.

(iii) Wajumbe watatu watakaoteuliwa na Halmashauri ya Wilaya ambamo Mamlaka imo.

(iv) Mbunge anayewakilisha Jimbo ambamo Mamlaka imo.

(v) Wajumbe wanawake wasiopungua theluthi moja ya wajumbe wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa mujibu wa Kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya Muheza kilichofanyika jana tarehe 27/6/2007 Mamlaka ya Mji mdogo wa Muheza itaanza rasmi tarehe 1/7/2007 na wamepewa Ofisi na vifaa katika Kata ya Mbaramo karibu na Soko Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikao cha kwanza cha Baraza kitafanyika tarehe 30/6/2007 ili kuweka mkakati wa kuanza utekelezaji ikiwa ni pamoja na kukusanya mapato, usafi wa mji na kusimamia ulinzi na usalama.

Baraza la Mamlaka ya Mji Mdogo litawajibika kwa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya husika. unapenda kuchukua fursa hii kuwaagiza Wakurugenzi wa Halmashauri wote ambamo katika maeneo yao kumeanzishwa Mamlaka za Miji Midogo wazingatie utaratibu huu ili kukamilisha mchakato wa kuanzisha rasmi Mamlaka za Miji Midogo.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa mwongozo mpya aliotutolea. Hata hivyo ningeomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa upo utaratibu ambao unaelekeza kwamba pale ambapo panakuwa na Makao Makuu ya Mji panapaswa vilevile kuwa na Halmashauri ya Mji. Je, ni lini basi hii Halmashauri ya Mji wa Muheza itapatikana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Mji au Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya kuna vigezo maalum ambavyo vipo kwa ajili ya kuanzisha Mamlaka ya Mji.

Kwa hiyo, Halmashauri ya Wilaya ya Muheza itakuwa Halmashauri ya Mji itatimiza vigezo ambavyo vimewekwa kwa mujibu wa Sheria. Mpaka sasa hivi vigezo hivi kwa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza havijatimia. Kwa hiyo, hapo vitakapotimia Halmashauri ya Mji ya Muheza itaanzishwa. *(Makofi)*

Na. 96

**Ujenzi wa Chuo cha "Marine Sciences"**

**MHE. USSI AME PANDU** aliuliza:-

Kwa kuwa, ujenzi wa Chuo cha *'Science Marine'* unaofanyika Buyu Zanzibar unaendelea:-

(a) Je, mpaka sasa ujenzi huo umefikia hatua gani?

(b) Je, Ujenzi huo utamalizika lini kwa mujibu wa Mkataba?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kumjibu swali hili naomba kwa niaba ya wanawake na kwa wananchi wa Mkoa wa Mara ambao wengi wamenipigia simu nitoe salamu za rambirambi kwa familia ya Marehemu Amina Chifupa Mpakanjia, kufuatia kifo cha huyo binti ambaye amefariki juzi na atazikwa leo na tuwaombee wote waliofiwa wawe na utulivu na nguvu na tunaiombea roho ya Marehemu, Mungu aweke mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mbunge wa Mtoni, swali lake lenye sehemu (a) na (b) napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Taasisi ya Sayansi za Bahari ya Chuo Kikuu Dar es Salaam na siyo Chuo cha "*Marine Sciences*" umegawanyika katika awamu mbili. Awamu ya kwanza ni jengo mjumuisho *(multi-purpose)* lenye ofisi, maabara, vyumba vya kufundishia na maktaba.

Awamu ya pili ni majengo yaliyobaki, kama bweni la wanafunzi, majengo ya huduma na "*aquarium*". Mkandarasi ni Kampuni ya China *Railway Jiangchan Engineering (T) Ltd*. Na msanifu msimamizi *(Architect and Consultant)* ni Chuo Kikuu kishiriki cha Usanifi Majengo (*UCLAS*).

(a) Mkandarasi amekamilisha sehemu ya msingi wa Jengo mjumuisho *(Multi-purpose)* lenye ofisi, maabara, vyumba vya kufundishia na maktaba.

(b) Ujenzi wa awamu ya kwanza ulianza rasmi mwezi Machi, 2005 na kwa mujibu wa Mkataba, ulitarajiwa kukamilika baada ya miezi 18. Hata hivyo, ujenzi huo haujakamilika kutokana na ufinyu wa Bajeti. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimefanya mazungumzo na Benki ya *CRDB* kuomba mkopo na Benki ya *CRDB* imeonyesha nia ya kukubali kuwakopesha Chuo kiasi cha shilingi bilioni 6.369 kwa ajili ya kumaliza ujenzi iwapo Serikali itakubali kukidhamini kupewa mkopo huo.

Mazungumzo kati ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia na Wizara ya Fedha yanaendelea kuhusu Chuo kuwekewa dhamana. Mazungumzo hayo yatakapokamilika hatua ya pili ya kumalizia ujenzi wa Taasisi hiyo utaanza mara moja. Aidha Wizara yangu imetenga shilingi bilioni 1 katika Bajeti yake ya mwaka 2007/2008 kwa ajili ya ujenzi wa Taasisi hiyo.

**MHE. USSI AME PANDU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naomba niulizwe swali la nyongeza. Wakati tunatembelea ujenzi ule kupitia Kamati yetu tulikuta ule ujenzi unakwenda kwa kusua sua sana na nafikiri ni kutokana na tatizo la fedha. Je, endapo yule Mkandarasi ataenda Mahakamani kuishitaki Serikali kwa kuwa muda umepita sijui Mheshimiwa Waziri anaweza kulieleza nini Bunge hili?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri katika Mkataba uliowekwa kati ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Mkandarasi kipengele cha 62, kinatamka wazi kwamba iwapo mradi huu utakatishwa kutokana na dharura kama vile vita, matatizo ya kifedha kinachofanyika sio kwenda Mahakamani kwa Mkandarasi bali ni Mkandarasi kupewa pesa aliyoitumia hadi hapo ilipofikia na ni kitu ambacho tumeshafanya.

Pia kipengele kinasema katika hiyo hali Mkandarasi anawajibika kulinda maeneo anayoyajenga. Kwa hiyo, tuna uhakika kabisa kwamba uhusiano tulio nao na kwa kipengele hiki cha Mkataba Mkandarasi hawezi kwenda Mahakamani.

Na. 97

**Uhusiano wa Tanzania na Afrika Kusini**

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, pamoja na vitisho vya Makaburu kwa nchi yetu ilipoamua kuweka Makao Makuu ya Kamati ya Ukombozi wa Bara la Afrika na Kambi za Wapigania Uhuru wa *ANC* chini ya uongozi wa Mwalimu Nyerere, Tanzania tulisimama imara kuondoa ubaguzi wa rangi Afrika ya Kusini:-

Je, sasa Tanzania na Afrika ya Kusini tunashirikiana kwa jambo gani la faida kwa nchi zetu kama kielelezo cha ushindi wa uhusiano wetu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA – (MHE. CYRIL A.CHAMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na kwa ruksa yako naomba nitumie fursa hii kwa niaba ya wananchi wote wa Jimbo la Moshi Vijijini na kwa niaba yangu binafsi, kutoa pole kwa familia ya Marehemu Mbunge mwenzetu kwa Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, kwako wewe Mheshimiwa Mwenyekiti na kwa Wabunge wenzangu wote katika msiba mkubwa uliotupata wa kuondokewa na Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia. Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema peponi. Amin.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya salaam hizo za rambirambi kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa pamoja na vitisho vya Makaburu kwa nchi yetu ilipoteuliwa na Umoja wa Nchi Huru za Afrika kuwa Makao Makuu ya Kamati ya Ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika na kujenga Makazi ya Wapigania Uhuru wa *ANC* chini ya uongozi wa Mwalimu Nyerere, Tanzania tulisimamia imara dhidi ya ubaguzi wa rangi Afrika Kusini.

Kutokana na misingi mizuri ya kisiasa iliyowekwa tangu wakati wa harakati za kupigania ukombozi barani Afrika kati ya Tanzania na Afrika Kusini, uhusiano wetu umeendelea kukua, kuimarika na hivyo kujenga ushirikiano madhubuti wa kiuchumi kati ya nchi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 81 ya uwekezaji kutoka nje ya Tanzania ainafanywa na nchi kumi.

Aidha, kwa mujibu wa tathmini iliyofanywa na Kituo cha Uwekezaji (*TIC*), Benki Kuu ya Tanzania na Idara ya Takwimu (*TNBS*), kati ya nchi hizo 10, Afrika Kusini inaongoza kwa kuwekeza asilimia 34.4 ya mitaji yote katika miradi mbalimbali. Uwekezaji huu pamoja na mambo mengine umeongeza ajira, mapato ya Serikali na umeboresha tija ya wafanyakazi kwa kuwafunza Teknolojia mpya katika sekta zilizonufaika na uwekezaji huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti,tarehe 22 Septemba, 2005 viongozi wakuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, na wa Jamhuri ya Afrika ya Kusini, Mheshimiwa Rais Thabo Mbeki, walitia saini Mkataba wa kuanzishwa Tume ya Marais ya Ushirikiano wa Kiuchumi kati ya Tanzania na Afrika Kusini *(Presidential Economic Commission (PEC)* huko Pretoria, Afrika Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti,uanzishwaji wa Tume hii ya Marais ya Ushirikiano wa Kiuchumi ni kielelezo muhimu kwetu na ishara nzuri ya uhusiano na ushirikiano kati ya nchi zetu mbili kiuchumi.

Miongoni mwa mambo muhimu ya faida kwa nchi zetu yaliyoainishwa katika Tume hiyo ya ushirikiano ni pamoja na:-

- Ukuzaji na Udhibiti wa vitega uchumi; na
- Uepushaji wa ulipaji kodi mara mbili na udhibiti wa ukwepaji wa kodi na mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti,tarehe 5 Aprili, 2007, Tume hii ya Marais ya Ushirikiano wa uchumi ilifanya mkutano wake hapa nchini, mjini Dar es Salaam. Matokeo ya mkutano huo yalikuwa uwekaji saini wa makubaliano yafuatayo:-

- Sheria aya usafiri wa majini na masuala yanayohusiana na sheria hiyo.
- Ushirikiano katika maeneo ya uhamiaji
- Uondoaji wa malipo ya visa kwa wamiliki wa pasi za kidiplomasia na za utumishi uliotukuka.

Tume hii ilipokea pia Mapendekezo ya nafasi zilizopo za kuanza miradi ya pamoja katika ukanda wa Maendeleo wa Kati *(Central Corridor)* na ule wa Mtwara *(Mtwara Corridor)* na maeneo maalum ya Kiuchumi *(Special Economic Zones*) hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kabla ya kuundwa kwa Tume hii ya Marais ya ushirikiano wa Kiuchumi baina ya Tanzania na Afrika Kusini, tumekuwa tukishirikiana katika mambo mengi ya faida kwa nchi zetu mbili. Miongoni mwa mambo hayo ni pamoja na uwakilishwaji wa kidiplomasia katika nchi zote mbili kupitia Ofisi za Kibalozi. Tanzania ina Ubalozi mjini Pretoria na Afrika Kusini ina Ubalozi wake mjini Dar es Salaam.

Aidha, Tanzania na Afrika Kusini zina makubaliano ya jumla katika ushirikiano wa kiuchumi, Sayansi, Ufundi na Utamaduni tangu mwaka 1995. Yapo pia makubaliano ya Mamlaka ya Anga (*Aeronautical Authorities*) kati ya Serikali zetu mbili tangu mwaka 2003. Kwa ujumla, tunashirikiana na Afrika ya Kusini katika mambo mengi yenye manufaa kiuchumi.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kutoka na maelezo ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyatoa sasa. Kwamba kuna mawazo na makubaliano ya kushikiana katika masuala ya miradi ya pamoja kama ile ya Uhuru *corridor.* Je, Waziri anaweza kutueleza ni aina gani ya Miradi itakayojengwa kwa ushirikiano na nchi ya Afrika ya Kusini.

Pili, tuliposhughulika katika ukombozi wa Bara la Afrika hususani na nchi kama hiyo pamoja na nchi kama Msumbiji, kule Msumbiji wenzetu walitoa Jengo kwa Serikali yetu kama kumbukumbu na kutambua juhudi ya Tanzania na pia Zambia tulijenga barara na reli ya uhuru.

Sasa Waziri atakubaliana nami kwamba kwa nchi kama Afrika ya Kusini tunajitaji kuwa na mradi mmoja wa kihistoria ambao utakuwa ni kumbukumbu kwa nchi yetu badala ya kuzungumzia habari ya uwekezaji tu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA (MHE. CYRIL A. CHAMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ambayo imeainishwa katika Mtwara *Development Corrodor* na *Central Development Corridor* ni ile miradi ambayo inahusiana na miundombinu hasa kwa ajili ya kufungua maeneo haya yaweze kufikika kwa ajili ya kutumia raslimali nyingi zilizopo katika maeneo hayo. Vilevile kwa ajili ya kuyafungua maeneo hayo ili makampuni ya Tanzania na Afrika Kusini yaweze kufika mpaka Rwanda, Burundi na Mashariki mwa *DRC.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili linalohusu mradi wa kihistoria, nakubaliana naye kwamba ni kweli Msumbiji wametupa jengo na tumekuwa na miradi ya pamoja kati ya Tanzania, Zambia na China na ni kweli kwamba ni vizuri kwamba kama tutakuwa na mradi wa pamoja na Afrika ya Kusini na ndiyo maana katika jibu langu la msingi nikasema kwamba Maraisi wetu wameunda tume ya pamoja.

Lengo mojawapo la tume hiyo ni kuwa na miradi ya namna hiyo, miradi mikubwa ambayo itakuwa ya kihistoria lakini si tu kwa ajili ya historia iliyopo lakini ni kwa ajili ya kuhakikisha kwamba manufaa ya kiuchumi yanawafikia Watanzania na vile vile Waafrika Kusini ambao wanashiriki katika miradi hiyo. *(Makofi)*

Na. 98

**Upotevu wa Fedha kwa Vocha Zisizo Sahihi**

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA** aliuliza**:-**

Kwa kuwa kwa muda mrefu Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali amekuwa akilalamikia matumizi yenye mashaka kwa njia ya vocha zisizo sahihi au zisizo na nyaraka:-

(a) Je, tangu Julai, 2001 hadi Juni 2006 ni kiasi gani cha fedha kimepotea wakati ukaguzi au wakati wa matumizi kutokana na vocha zisizo sahihi kwa Hesabu za Serikali Kuu na Serikali za Mitaa na kati ya fedha hizo ni kiasi gani cha fedha kimethibitika kutumika kwa taratibu za matunzo ya fedha za Serikali na ni kwa sababu gani zemefanya hati zisionekane kabla wakati wa ukaguzi na kupatikana baadaye?

(b) Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya upoteaji wa hati hizo za kutotunzwa vizuri wakti wote wa uandishi, ukaguzi na uhifadhi?

(c) Je, watu wangapi kati ya wahusika wamepoteza hati hizo kwa makusudi au uzembe na wangapi kati ya hao wamechukuliwa hatua kutokana na makosa hayo katika kipindi cha kati ya mwaka 2001 hadi 30 Juni, 2006.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Wilbrod Peter Slaa, Mbunge wa Karatu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Julai, 2001 hadi Juni, 2005 hoja zilizohusu malipo yasiyo na nyaraka (*unvouched expenditure*) zilikuwa zenye jumla ya shilingi 13,718,996,927.95 na sasa kiwango hiki kimepungua na kufikia shilingi 43,485,351.00 (sawa na asilimia 0.003 ya kiwango cha awali) baada ya nyaraka husika kuwasilishwa kwa wakaguzi.

Malipo yenye nyaraka pungufu *(improperly vouched expenditure)* yalikuwa shilingi 80,734,216,390.64 na sasa kiwango hiki kimepungua kufikia shilingi 1,550,059,502.42 sawa na asilimia 0.019 ya kiwango cha awali.

Aidha kuanzia Julai 2005 hadi Juni 2006; malipo yasiyokuwa na nyaraka yalikuwa shilingi 1,319,857,934.00, na malipo yenye nyaraka pungufu yalikuwa shilingi 56,511,145,057.00 ikiwa ni pamoja na kiasi hiki kinahusu bakaa ya shilingi 1,550,059,502.42 ya miaka ya 2001 hadi 2005. Nyaraka zenye jumla ya shilingi 33,709,476,043.00 zimekwishahakikiwa na hoja kufungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Serikali za Mitaa, hoja zinazohusu vocha zisizo na nyaraka au zenye nyaraka pungufu zimekuwa zikipungua kutoka shilingi 11.66 bilioni mwaka 2000/2001 hadi shilingi 5.26 bilioni mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kufafanua kuwa malipo haya si malipo yenye hati zisizo sahihi bali ni zenye nyaraka pungufu kutokana na sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vocha zisizo na nyarala *(unvouched expenditure*) zinahusisha malipo yote ambayo hukosa viambatanisho vinavyotakuwa katika kukamilisha malipo husika; kwa upande mwingine vocha zenye nyaraka pungufu (*improperly vouched expenditure)* zinahusisha malipo yote ambayo huwa na viambatanisho pungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu kubwa ya mapungufu haya kwa miaka kadhaa sasa ni kutokana na mawasiliano sahihi kati ya Wakaguzi na wakaguliwa. Kwa mfano fedha zinazohusu Maendeleo ya Halmashauri huwa ndani ya Bajeti za Mikoa.

Lakini fedha halisi *(funds transfers*) kutoka Hazina hupelekwa moja kwa moja kwenye Halmashauri husika bila kupitia mikoani na hivyo Halmashauri hupeleka Hazina stakabadhi ya kukiri kupokea fedha hizo. Nyaraka pekee inayopelekwa Mikoani ni *Exchequer Issue Notification* inayohusisha fedha za maendeleo zilizopelekwa kwenye Halmashauri. *(Makofi)*

Hivyo Mkaguzi anapofanya ukaguzi kwenye Mkoa husika akihitaji kuona stakabadhi ya kukiri kupokea fedha hizo ni wazi hataipata na hivyo huandika hoja chini ya malipo yasiyokuwa na nyaraka.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imechukua hatua za makusudi za kuajiri Wahasibu na Wakaguzi wa ndani wenye sifa na uelewa mzuri katika uandishi na uhifadhi wa nyaraka za Serikali.

Aidha Serikali inazidi kuimarisha Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani kwani ndivyo venye majukumu ya kuhakikisha mapungufu kama hata hayatokei. Vile vile Serikali itaendelea kutoa adhabu kwa Afisa yeyote atakayebainika kupoteza fedha na mali za umma zikiwemo nyaraka za malipo kama Kanuni za fedha zinavyoelekeza.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka ya 2001 hadi 30 Juni, 2006 hakuna kumbukumbu ya Afisa yeyote aliyepoteza nyaraka za malipo kwa makusudi au uzembe.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa baadhi ya Hati au Nyaraka hizi zingine ni katika manunuzi au ni katika vifaa vilivyonunuliwa lakini havikuingizwa kwenye kitabu, au ni katika fedha zilizowekwa lakini hazikuingizwa kwenye vitabu vya hesabu; na kwa sababu hawa watu wanaofanya kazi hii ni wataalam waliosomeshwa kwa pesa nyingi; na kwa sababu kuna ushahidi pia kwamba wakati mwingine hati hizi huwa zinaondelea kwenye ma-*batch,* na hii imetokea kule Karatu na kesi ikapelekwa Mahakamani.

Je, Waziri anaeleza nini kwamba hawa watu waliosoma kwa utaratibu huu sio wanaandaa njia ya wizi kwa makusudi kwa kupoteza hizi nyaraka lakini baadaye wanakwenda kuzitafuta mahali pengine kwa utaratbu wowote wa kiujanja ujanja?

Swali la pili, Kwa kuwa ni kweli njia moja ya kuzuia uhalifu ni kupata taarifa mapema na mawasiliano ya uhakika. Ni kitu gani kinachofanya Wizara wakati inapeleka fedha, kwa nini haipeleki pamoja na zile *transfer*/hati zinazohusika ili Wahasibu wa Wilaya na wa Mikoa wawe na taarifa sahihi kabla hawajafanya hata matumizi yao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyoelewa, taarifa zote hizi za *CAG*, baada ya kutoa Ripoti yake, zinakwenda kwenye *PAC* na tunazihakikisha kwamba fedha zile zilizopotea, kama zimepotea ni hatua gani inayochukuliwa na Waziri wa Fedha huleta kwenye Bunge hili baada ya *PAC* kudhibitisha kwamba fedha zile kweli hazikupotea au nyaraka zile kweli zilikuwepo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hatuwezi kuwa na wasi wasi tu kwamba nyaraka zilizoletwa si sahihi au zimekwenda kuundwa huko. Kama haijathibitika kwamba ni makosa kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, Mhasibu yule hana kosa. Na maadam inathibitishwa katika *PAC* na Waziri wa Fedha anakubaliwa na Bunge hili baada ya kuthibitika na hatua mbali mbali zilizochukuliwa. Kwa hiyo ni sawa na ndio maana tunamwambia hakuna yeyote aliyepoteza nyaraka kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba aidha amefanya kwa uzembe au amefanya kwa makusudi kwa kuiba fedha za Serikali. *(Makosa)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri, napenda kuongezea jibu kutoka Wizara ya Fedha. Nipende tu kusema kwamba Sheria ya mwaka 2001 ya Fedha ambayo ilifanyiwa marekebisho mwaka 2004 na ambapo *Regulations* za Sheria hii ziliandaliwa mwishoni mwa mwaka 2005, zinaitaka sasa *PAC* itoe mapendekezo kwa Waziri wa Fedha kwa hatua gani au *penalty* gani ambazo zichukuliwe kwa Wahasibu ambao ni wazembe.

Kwa hiyo, kwa taarifa hii ya 2005/2006 ambayo *PAC* nafikiri ili-*discuss* mwezi wa Februari, 2007 tunategemea kwamba *PAC* imwandikie Waziri wa Fedha hatua gani ambazo zinatakiwa zichukuliwe kwa hao ambao walihusika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ahsante sana! Sasa tunahamia Wizara ya Maji. Kabla sijamwita mwuliza swali, niwataarifu tu Waheshimiwa Wabunge kwamba kwa maswali tuliyonayo ni mengi na muda uliobaki ni mdogo. Kwa hiyo, swali litakuwa ni moja moja kwa kila Wizara.

Na. 99

**Mradi wa Maji – Kitumbi**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO (K.n.y. MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA)** aliuliza:-

Kwa kuwa wakati wa ujenzi wa barabara ya lami kati ya eneo la Chalinze na Segera, Mkandarasi alikuwa akivuna mawe eneo la Kitumbi Handeni na kwa kuwa eneo hilo limegundulika kuwa na mkondo mkubwa wa maji yanayoweza kuhudumia maeneo ya Kitumbi hadi Kabuku:-

(a) Je, Serikali iko tayari kutekeleza mradi huo ambao kwa mantiki gharama zake zitakuwa ndogo ukilinganisha na miradi kama ile ya Benki ya Dunia ambayo imepata fedha nyingi kule Handeni lakini matumizi yake si ya tija?

(b) Je, Serikali iko tayari kunipa wataalam niende nao katika eneo hilo ili wakajionee na hatimaye tuanze kazi ya utekelezaji wa mradi huo?

(c) Kama jibu ni ndiyo, nitapewa lini wataalam hao?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mbunge wa Jimbo la Handeni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ina taarifa kuhusu kuwepo kwa mkondo wa maji katika eneo la Kitumbi katika Wilaya ya Handeni. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji akiongozana na wataalam wa Wizara pamoja na Viongozi wa Wilaya ya Handeni alitembelea eneo hilo katikati ya mwezi Januari 2007 alipokuwa kwenye ziara ya Wilaya ya Handeni. Sampuli ya maji hayo ilichukuliwa na kufanyiwa uchunguzi na kuonekana kwamba maji yanafaa kwa matumizi. Wizara yangu imepanga kuwapeleka wataalam kutoka Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa *(DDCA)* katika eneo hilo mwezi Julai 2007 ili kufanya uchunguzi na kupima uwingi wa maji ya chanzo hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo hayo yatatumika katika kufikia uamuzi wa matumizi ya mkondo huu wa maji, ikiwa ni pamoja na kuhudumia maeneo ya Kitumbi hadi Kabuku. Usanifu wa kina ndio utaainisha gharama za mradi na hivyo kujua kama gharama itakuwa ndogo ukilinganisha na gharama ya miradi inayotekelezwa Wilayani Handeni chini ya mradi wa maji na usafi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mbunge wa Handeni kwa kutufahamisha chanzo hiki cha maji ambacho hatimaye kinaweza kuwa ni chanzo kizuri cha kuaminika kuongeza maji katika maeneo ambayo majaribio ya uchimbaji wa visima hayakuweza kufanikiwa kupata maji ardhini. Pia tunaomba ushirikiano wake Mheshimiwa Mbunge katika kuwahamasisha wananchi ambao wana miradi ya mawe ya kokoto sehemu hizi wahame ili kuhifadhi chanzo hiki kipya.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa katika swali lake la kwanza, Mheshimiwa Kigoda, ameeleza utekelezaji usio na tija wa miradi inayofadhiliwa na Benki ya Dunia; na kwa kuwa katika Jimbo la Bumbuli kuna miradi ya aina hiyo inayofadhiliwa na Benki ya Dunia kama; Mradi wa Kwa Kidole, Bumbuli, Kweminyasa, Soni Mbuzii na Mgwashi, Je Waziri atakubaliana na mimi kwamba Wataalam hao tunawahitaji ili watusaidie kutengeneza mipango ya utekelezaji *(Action Plan)* ili miradi ya Bumbuli isikumbwe na tatizo lililotokea Handeni?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Bumbuli kwa hivi sasa na lenyewe litaingia katika Programu ya Maji ya Visima vile kumi vya kila Wilaya. Na katika Jimbo la Bumbuli kutakuwa na visima vinne, kimojawapo kikiwa Kijiji cha Kwaminyasa, kingine katika kijiji cha Kwa Kidole, kingine Bumbuli na kingine Mgwashi. Hata hivyo, miradi hii kwa Jimbo la Bumbuli bado haijaanza na tunatarajia itaanza mapema mwishoni mwa mwezi wa Nane. Na kwa hali hiyo basi, baada ya mambo mengi ambayo tumejifunza kufuatana na utekelezaji wa awali katika Wilaya 14, tumejifunza mengi kwamba tunaomba kila Halmashauri na kila Mheshimiwa Mbunge, washirikiane katika kuhakikisha kwamba wale Wakandarasi watakaochaguliwa kujenga miradi hii, wawe na sifa za kuweza kufanya kazi hizo na pia wawe na uwezo wa kifedha wa kuweza kumudu kasi ya kuendesha miradi hiyo.

Na. 100

**Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria**

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Bukombe ina matatizo makubwa sana ya maji na kwa kuwa visima vifupi vinapochimbwa havina uwezo wa kuhimili kiangazi kinapotokea Wilayani hapo, na kwa kuwa mradi wa Maji wa Ziwa Victoria umebakia kilomita 100 kufika Bukombe:-

(a) Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Wilaya ya Bukombe kuhusiana na mradi wa maji wa Ziwa Victoria kufika Bukombe ndani ya Utawala wa kipindi cha 2005/2010 wenye Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya?

(b) Kwa kuwa mradi huo utaanza kujengwa toka Kahama kuja Bukombe, maeneo ya Kanegere, Gerezani, Masumbwe, *Nyakusuru Mine,* Lubeho, Bukombe Ushirombo (Makao Makuu ya Wilaya) Runzewe, Uyovu na Mgodi wa Tulawaka yatanufaika na mradi huo. Je, Serikali iko tayari na itafurahia kuona wananchi wa maeneo hayo wananufaika na mradi huo au itafurahia kuona wananchi wanaendelea kuteseka kwa shida hiyo ya maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel J. Luhahula, Mbunge wa Jimbo la Bukombe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya kwanza ya mradi unaotoa maji Ziwa Victoria kupeleka miji ya Kahama na Shinyanga, utakuwa na uwezo wa kutoa maji mita za ujazo 80,000 kwa siku na kutosheleza mahitaji ya watu 420,000 wa Kahama na Shinyanga pamoja na vijiji 54 ambavyo viko umbali usiozidi kilomita 5 kutoka kwenye Bomba Kuu ikiwemo Wilaya ya Bukombe iliyoko umbali wa Kilomita 100 toka kwenye mradi huu. Aidha, Wizara yangu inaendelea kupokea mapendekezo mbali mbali kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge wa maeneo ambako mradi huo unapita. Mapendekezo hayo yatachambuliwa ili kuona uwezekano wa kuyahusisha maeneo zaidi kwenye awamu ya pili ya mradi huo. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Vijiji vya Masumbwe, Lugunga, Lutembela, Bwelwa na Iponya na Mji wa Ushirombo vimeingizwa kwenye awamu ya kwanza ya Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira ambavyo ni kati ya Vijiji 10 vilivyochaguliwa na Wilaya ya Bukombe. Aidha, vijiji vilivyobakia vya Kanegere, Gerezani, *Nyakusuru Mine,* Lubeho, Runzewa, Uyovu na Mgodi wa Tulawaka vitaingizwa kwenye awamu ya pili ya Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini kulingana na maamuzi ya Halmashauri ya Wilaya yenyewe.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Labda nitapenda tu kuipongeza Serikali kutokana na majibu yaliyotolewa na Naibu Waziri na majibu yaliyotolewa pia na Mheshimiwa Waziri tarehe 21. Basi, naomba tu Serikali itekeleze kama ilivyosema. Ahsante sana.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kuniruhusu niulize swali la nyongeza. Matatizo yaliyoko Bukombe yanafanana sana na matatizo yaliyoko katika Jimbo la Busanda; na Bukombe inapakana kwa sehemu kubwa sana na Jimbo la Busanda ambalo linapakana na Ziwa Victoria; Serikali inasema nini kuhusu vijiji vya Jimbo la Busanda, kuna mradi wa maji wa Nyahagomba na kuna ahadi ya Bwawa kijiji cha Katoro na visima mbali mbali, lakini, hakuna kinachotekelezwa. Serikali inasema nini kuweza kuwasaidia wananchi hawa wa Jimbo la Busanda ambao wanaona wenzao wako kwenye Programu?

**MWENYEKITI:** Naona kama ni swali jipya kabisa! Labda kama Mheshimiwa Naibu Waziri ana jibu. Lakini nadhani ni swali jipya, lije katika utaratibu wa kawaida.

Na. 101

**Ujenzi wa barabara zenye faida kubwa**

**MHE. YONO S. KEVELA (K.n.y. MHE. JACKSON M. MAKWETA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ina lengo la kutaka kukuza uchumi nchini:-

(a) Je, Serikali itakubali ombi langu kwamba, itilie maanani ujenzi wa barabara zenye faida kubwa kiuchumi kwanza ili ipate fedha za kuendelea na ujenzi wa barabara nyingine zisizo na faida kubwa kiuchumi?

(b) Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya Njombe - Lupembe katika kiwango cha lami ili kurahisisha usafirishaji wa chai na mbao toka Lupembe, matunda na mchele kutoka Bonde la Kilombero?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jackson Makweta, Mbunge wa Njombe Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya mradi wowote mkubwa wa barabara kujengwa, hufanyiwa upembuzi yakinifu *(feasilibility study)* ili kuona kama ina faida za kiuchumi *(economic justification)* na hivyo kustahili kujengwa na kwa kiwango gani, yaani kwa lami au changarawe. Kwa hiyo, Serikali inatilia maanani ujenzi wa barabara kwa kuzingatia faida za kiuchumi kama anavyoomba Mheshimiwa Mbunge.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Njombe – Lupembe inayoanzia Kibena na kuishia Tarafa ya Lupembe yenye urefu wa kilometa 66.35 haipo kwenye mpango wa kujengwa kwa kiwango cha lami kwa sasa kutokana na uwezo mdogo wa Serikali kifedha. Mkakati wa Serikali kwa sasa ni kujenga kwanza hatua kwa hatua kwa kiwango cha lami barabara kuu zinazounganisha nchi yetu na nchi jirani, pamoja na barabara zinazounganisha miji mikuu ya mikoa, mfano ile iendayo Ruvuma kupitia Njombe na baadaye barabara ya mikoa kutegemea upatikanaji wa fedha na kipaumbele cha barabara husika.

Hata hivyo, kwa kuzingatia umuhimu wa barabara ya Njombe-Lupembe, Serikali itaendelea kuifanyia matengenezo mbalimbali kila mwaka ili iendelee kupitika wakati wote, na pia katika kuzingatia matakwa ya vipaumbele vilivyoainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 hadi 2010. Kwa mfano katika mwaka wa fedha 2006/2007 jumla wa shilingi milioni 40.9 zimetolewa na kutumika kwa matengenezo ya kawaida ya barabara hii na hali ya barabara ni nzuri.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa barabara ya Njombe – Lupembe inalingana kabisa na ile barabara ya Njombe – Makete, yaani kupitia Kata ya Igosi na Kipengele; na kwa kuwa hii barabara ya Njombe – Makete mara nyingi inapojengwa inawekwa kifusi cha udongo, siyo cha kokoro na hivyo kusababisha kwamba sasa hivi haipitiki, ina mashimo marefu sana na kuleta kero kubwa kwa wananchi wa Igosi, Kipengele, Makete na Njombe kwa ujumla. Je, ni lini Serikali itaweka kifusi cha kokoto kuliko ilivyo sasa hivi kuweka kifusi cha udongo mpaka

kusababisha usumbufu mkubwa sana katika Jimbo letu la Njombe hasa Wilaya ya Njombe na Mkoa wa Iringa kwa ujumla?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hiyo ya Njombe – Makete imekuwa ikitengenezwa kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge. Lakini, kutokana na ufinyu wa Bajeti, matengenezo hayajawa makubwa kama ambavyo angependa au ambavyo na sisi tungependa. Hata hivyo, katika mwaka huu ujao wa fedha, bado fedha zimewekwa kwa ajili ya kuendelea kutengeneza barabara hiyo ya Njombe – Makete ambayo hata mimi niliikagua na nikaona hali hiyo. Tuombe kwamba fedha zikiwa zinatosheleza, basi itatengenezwa kwa kiwango ambacho kitaridhisha ili barabara hiyo ipitike mwaka mzima.

Na. 102

**Hitaji la Boti – Mtwara**

**MHE. MOHAMED S. SINANI** aliuliza:-

Kwa kuwa boti iliyokuwa ikitumika kuvusha wananchi kutoka Mtwara kuelekea Msangamkuu imeharibika miaka mingi na kwamba, wananchi wa maeneo hayo wanahatarisha maisha yao kwa kutumia mtumbwi midogo midogo kuvukia:-

Je, ni lini Serikali itawapatia wananchi hao boti nyingine ili kunusuru maisha yao?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Said Sinani, Mbunge wa Mtwara Mjini naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1990 Serikai ilinunua boti kwa ajili ya kuvusha wananchi kutoka Mtwara kuelekea Msangamkuu. Boti hiyo ilikuwa na uwezo wa kubeba abiria 25 na ilikuwa inamilikiwa na Wizara yangu hadi mwaka 1998 ilipokabidhiwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara. Boti hiyo iliuzwa kwenye mnada mwaka 2004 kutokana na uchakavu. Sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Said Sinani, Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inategemea kutenga fedha za kununua boti nyingine mpya katika mwaka wa fedha 2008/2009 ili wananchi wa maeneo hayo waweze kupata huduma bora ya kuvuka.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante! Kwa kuwa swali la msingi linafanana na mazingira yaliyoko Kilwa; swali langu kwa ufupi,

nataka kujua ni lini wananchi wa Kilwa wa Tarafa ya Pande kuelekea Makao Makuu ya Wilaya ya Masoko, Kilwa Kisiwani kuelekea Makao Makuu ya Wilaya ya Masoko, watapata nao Boti ili iweze kuwasaidia kwa sababu wamekuwa wakitumia Boti zisizokuwa na uhakika ambazo zinawazimikia wakati wowote na hakuna usafiri mwingine mbadala.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali haijapata uwezo wa fedha wa kununua Boti katika eneo hilo alilolitaja. Lakini, pindi uwezo utakapopatikana tutaiangalia hali hiyo ili wananchi wa maeneo hayo na wenyewe waweze kupata kivuko.

Na. 103

**Makumbusho ya Kwihara Tabora na Ujiji Kigoma Kutambuliwa**

**MHE. SAID J. NKUMBA (k.n.y. MHE. AZIZA SLEYUM ALLY)** aliuliza:-

Kwa kuwa ni Sera ya Serikali kuendeleza maeneo ya kihistoria yenye malikale; na kwa kuwa njia na makazi yaliyotumiwa na watumwa na Mvumbuzi Dr. Livingstone kutoka Bagamoyo hadi Kigoma hakuna matunzo yoyote:

Je, Serikali inasema nini kuhusu makumbusho ya Kwihara Tabora na yale ya Ujiji Kigoma ambayo hayatangazwi kabisa na historia hiyo kusahauliwa kwa jamii yetu?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Tabora, kama ifuatavyo:-

Njia ya Kati ya Biashara ya Watumwa na Vipusa ina urefu wa Kilomita 1200 kutoka Ujiji Kigoma hadi Mji wa Kihistoria wa Bagamoyo. Ni kweli kwamba makumbusho ya Kwihara Tabora na yale ya Ujiji Kigoma ni vituo muhimu vya kumbukumbu ya Njia na Makazi yaliyotumiwa na Watumwa na Mvumbuzi Dr. David Livingstone, kutoka Bagamoyo hadi Kigoma. Aidha, vituo hivyo vinatambuliwa na Serikali kama Kumbukumbu za Taifa kwa Tamko la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa kuyatangaza maeneo hayo, Wizara ilianzisha Makumbusho ndogo katika maeneo hayo pamoja na kutengeneza vipeperushi vinavyotangaza Kituo cha Kumbukumbu cha Dr. David Livingstone na kuelimisha Umma kuhusu historia ya Vituo. Sambamba na juhudi hizo, Wizara yangu hivi sasa ina mpango wa kuboresha Vituo vya Ujiji na Kwihara pamoja na njia yote ya biashara ya watumwa na vipusa. Hivi sasa Serikali inajenga kituo cha taarifa na kumbukumbu katika Makumbusho ndogo ya Ujiji Kigoma na kazi hiyo inatarajia kukamilika mwishoni mwa 2007. Kutokana na hatua hizo, Chuo Kikuu cha *Suton Hall*, Idara ya Historia imeanzisha safari kwa wanafunzi wanaojifunza masomo ya Historia ya Afrika kutembelea njia ya kati ya biashara ya watumwa na vipusa kila mwaka. Mwaka

2007, timu hiyo ilitembelea na kujifunza maajabu ya Mji Mkongwe wa Bagamoyo na Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2007/2008, Wizara yangu kwa kupitia Mradi wa kujenga uwezo ambao unafadhiliwa kwa pamoja baina ya Tanzania na Serikali ya Sweden, kupitia Shirika la Maendeleo *(SIDA)* na kusimamiwa na Idara ya Mambo ya Kale, imepanga kufanya ukarabati wa Makumbusho ya Kwihara Tabora. Baada ya ukarabati huo, Serikali itajenga Kituo cha Taarifa na Kumbukumbu ili kueleimisha Umma kuhusu Historia ya Kituo cha Kwihara na kuvutia Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutangaza Makumbusho ya Kwihara Tabora na yale ya Ujiji Kigoma, Wizara yangu kupitia Mradi wa kujenga uwezo wa Idara ya Mambo ya Kale inaandaaa programu ya Kitaifa ya Mambo ya Kale ya kuhamasisha jamii kuhusu uhifadhi na uendelezaji wa urithi wa utamaduni. Hivi sasa mtaalam mshauri amekamilisha rasimu ya programu hiyo ambayo utekelezaji wake utaanza mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kwamba, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipotembelea Mkoa wa Kigoma hivi karibuni, pamoja na mambo mengine, alitembelea Makumbusho ya Ujiji Kigoma na kukagua Maendeleo ya ujenzi wa Kituo cha Taarifa na Kumbukumbu.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imetupa matumaini kwamba itaimarisha kile Kituo cha Historia cha Dr. Livingstone; na kwa kuwa pia Tanzania tumebahatika kuwa na Meli ya Lihemba iliyotengenezwa na Wajerumani mwaka 1913 na ndiyo meli pekee Duniani ambayo mpaka sasa inatembea; Je, meli hii ya kihistoria haiwezi kuunganishwa katika programu au mradi huu wa ukumbusho wa Dr. David Livingstone?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikiliza ombi la Mheshimiwa Mzindakaya na tutalifanyia kazi. *(Makofi)*

Na. 104

**Mapato Yatokanayo na Utalii wa Mlima Kilimanjaro**

**MHE. ALOYCE B. KIMARO** aliuliza:-

Kwa kuwa, mapato yanayopatikana kutokana na Utalii wa Mlima Kilimanjaro ni makubwa kuliko mapato ya Hifadhi zote Tanzania:-

(a) Je, ni kiasi gani cha mapato kimepatikana kutoka kwa kila Hifadhi zetu kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita?

(b) Je, wananchi wanaozunguka Hifadhi hizo na kuzitunza wamepata mapato kiasi gani kwa ajili ya shughuli za maendeleo?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha mapato ya maisha ya vijana wanaopandisha watalii Mlima Kilimanjaro kwa kuhakikisha wanalipwa vizuri na *Tour Operators?*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapato yaliyopatikana kutoka Hifadhi za Taifa Tanzania kwa kipindi miaka mitatu iliyopita kwa pamoja ni kama ifuatavyo:-

§ Mwaka 2003/2004: Jumla ya Shilingi 22,783,864,553/=.

§ Mwaka 2004/2005: Jumla ya Shilingi 31,323,963,320/=.

§ Mwaka 2005/2006: Jumla ya Shilingi 43,014,298,256.33.

§ Jumla Kuu iliyopatikana ni Shilingi 97,122,126,130/=.

(e) Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanaoishi katika Vijiji karibu na maeneo ya Hifadhi za Taifa wamepata jumla ya shilingi 2,280,982,969/= kutoka *TANAPA* kwa ajili ya miradi ya Maendeleo. Kwa mfano, Ujenzi wa madarasa ya shule za msingi, ujenzi wa madarasa ya shule za sekondari, nyumba za walimu, majengo ya utawala, mabweni, zahanati, maabara, ununuzi wa samani za shule, ujenzi wa majosho ya mifugo, viwanja vya michezo, miradi ya umeme unaotokana na mionzi ya jua, elimu ya UKIMWI na kadhalika, ambapo jumla yake kwa miaka mitatu iliyopita ni shilingi 2,280,982,960/=.

(f) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha mapato ya vijana wanaowapandisha watalii katika Mlima Kilimanjaro, Serikali inawashauri vijana hao waunde Chama chao cha Wafanyakazi ambacho kitakuwa na katiba na viongozi. Katiba hiyo itaainisha shughuli wanazofanya, haki na wajibu wa kila mwanachama. Chama hiki hakina budi kisajiliwe na Msajili wa Vyama huru vya wafanyakazi na waajiri nchini Maofisa wa Wizara ya Kazi, Ajira na Vijana watakuwa tayari kuwasaidia kufanya shughuli hiyo.Ili chama hicho kiweze kuwa na nguvu zaidi ya kuwahudumia wanachama wake kwa ufanisi, hakina budi kujiunga na Shirikisho la Vyama huru vya Wafanyakazi *(TUCTA).*Sheria za kazi Namba 6 na Namba 7 za Mwaka 2004 zimeainisha sekta nane (8) za kazi ambazo chama hicho kinaweza kujiunga kwa kuangalia shughuli zake zinaoana na sekta ipi. Viwango vya chini vya mishahara vitawekwa na kila bodi ya kila sekta hizo nane.

Kwa kuwa chama hizo kitakuwa chini ya sekata ya usafiri na huduma ya mawasiliano, chama kitadai kiwango cha chini cha malipo kilichoainishwa kwa sekta hiyo. Aidha, kwa kuwa wafanyakazi wanafanya kazi kwa saa nyingi, utaratibu wa malipo ulioainishwa katika sheria Na. 6 ya *Employment and Labour Relations Act* ya 2004 utazingatiwa. Sheria mpya ya Utalii ambayo iko kwenye mchakato, itazingatia kuwa wenye sifa za kufanya kazi hiyo watakuwa ni Watanzania tu. Kwa mujibu wa sheria hiyo, Watanzania watapata fursa ya kufaidika zaidi kimaslahi tofauti na hali ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu iko tayari kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge ili kuwasaidia vijana hawa waweze kuandikisha chama chao chini ya sheria ya vyama huru vya wafanyakazi hapa nchini. *(Makofi)*

**MHE: ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa hawa vijana ndio wanaozalisha pesa yote inayoingia Serikalini kutokana na huo mlima; na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri alikiri hapa Bungeni wakati wa kipindi cha Bajati mwaka jana 2006 kwamba hawa vijana wananyanyasika sana. Je, anaweza kutoa tamko kabla hawajaandikisha hicho chama chao kwamba *TANAPA* na *Kilimanjaro National Park* wasimamie kwa karibu mishahara yao mpaka hapo chama chao cha wafanyakazi kitakachosimamiwa na Wizara ya Kazi kitakapoanzishwa?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana hawa ambao wanabeba mizigo ya watalii siyo wafanyakazi wa *TANAPA*. Tungemwomba Mheshimiwa Mbunge, ambaye ndiye Mwenyekiti wa vijana hawa, awasaidie chama chao kiandikishwe na Mrajisi wa Vyama Huru vya Wafanyakazi ili waweze kusaidiwa. (*Makofi*)

Na. 105

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID (k.n.y. MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiyo sheria mama na hivyo kuwa muhimu kwa Watanzania wengi kuisoma na kuielewa na kwa kuwa haipatikani kirahisi na ikipatikana bei yake ni kubwa sana Tshs. 3,500/= ambayo wananchi wa kawaida hawawezi kuimudu.

(a) Je, kwa nini Serikali isisambaze sheria hii mama nchi nzima kwenye taasisi zote za Serikali na *NGO* vijijini na Mijini bure?

(b) Je, kwa nini Serikali isifidie gharama na kuiuza Katiba hiyo kwa bei nafuu kwa mfano Tshs. 500 na zichapishwe kwa wingi ili kila Mtanzania anayehitaji aweze kuipata?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano, ni sheria mama na hivyo ni muhimu kwa Watanzania kuisoma na kuielewa. Katika kufahamu hili, Serikali kwa makusudi kabisa ilichukua hatua za kupunguza bei ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano kwa kutoa ruzuku ya uchapishaji. Nakala za Katiba huchapishwa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Bei ya shilingi 3500 ni bei ambayo Serikali imepanga ili kufidia gharama halisi ya uchapaji tu. Gharama hii haijumuishi gharama za uendeshaji wa ofisi ambazo hujumuisha mishahara ya wafanyakazi, umeme, maji, uendeshaji wa mitambo na kadhalika. Serikali haipati faida yoyote katika mauzo ya Katiba bali hutoa huduma tu. *(Makofi)*

Serikali ingependa kutoa nakala za Katiba Bure kwa wadau lakini hali ya kifedha hairuhusu. Tunaomba Mheshimiwa Mbunge, awe na subira na pale hali ya uchumi itaruhusu naamini Serikali itaweza kugawa nakala za Katiba ya Jamhuri ya Muungano bure.

Kama nilivyoeleza katika jibu langu la awali hali ya kifedha ndiyo inayosababisha Serikali kushindwa kuiuza Katiba kwa bei chini ya shilingi 3,500. Wizara yangu inafahamu kuwa ni vema kama Katiba ingesambazwa kwa wingi ili kila Mtanzania anayehitaji aweze kuipata. Mpaka hapo hali ya uchumi itakapokuwa nzuri na hivyo kuiwezesha Serikali kumudu gharama zote za uchapishaji itabidi wananchi waendelee kuchangia kwa kulipa kiasi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukua nafasi hii kuzipongeza taasisi mbalimbali za Serikali pamoja na mashirika yasiyo ya Kiserikali ambayo yamekuwa yakitoa elimu ya Katiba kwa wananchi kupitia *Radio,* Luninga, Midahalo mbalimbali, semina na magazeti mbalimbali. Serikali, kupitia taasisi na mashirika yake itaendelea kushirikiana na taasisi zisizo za Kiserikali kuhakikisha kwamba wananchi wanapata elimu inayostahili ya Katiba. (*Makofi*)

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kama alivyokwisha kueleza Mheshimiwa Waziri kwamba somo la Katiba ni somo muhimu sana. Je, kwa nini Serikali isifanye *syllabus* inayohusu Katiba ikaona lazima kwa shule za Sekondari ili hatimaye somo hili la Katiba likaweza kuwafikia raia wote hasa hii *generation* inayokuja? (*Makofi*)

**WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mheshimiwa Zubeir kwa swali lake na ushauri mzuri aliyoutoa. Tutawasiliana na taasisi husika katika kuona kwamba hilo linafanyika. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Muda wa maswali umeisha na maswali yetu yamekwisha tutakubaliana Waheshimiwa Wabunge kwamba kwa sababu ya idadi iliyokuwa imeongezeka ya maswali ndiyo maana palipatikana swali moja tu la msingi. Nitawaomba

watakaokuwa wakiongea baada ya hapa waweke mic zao vizuri kwa sababu *hansard* na waandishi wa habari wanalalamika kwamba hatusikiki vizuri.

Baada ya hapo niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba Hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu ya yaliyotokea jana itaendelea hadi Jumatatu. Huu ndiyo uamuzi wa Kamati ya Uongozi na Mheshimiwa Spika. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wengi bado mtapata nafasi muendelee kujiandaa kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Ninayo barua ya kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Mheshimiwa Mramba, akiwaalika Waheshimiwa Wabunge kutembelea maonyesho ya 31 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam. Anasema kwamba maonyesho hayo yatafunguliwa rasmi na Mheshimiwa A. Gwebuza Rais wa Msumbiji, tarehe 4 Julai 2007. Kutakuwa na mahudhuria ya mataifa kutoka nje, Wizara 6, taasisi 24 na wafanyabiashara binafsi wasiopungua 1500.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, mmeombwa kuhudhuria na mkifika pale ili kupata usaidizi wa kupokelewa na kutembezwa kwenye mabanda ya mawasiliano mnaweza kupata mwongozo zaidi kwa kumwona ndugu mmoja anayeitwa Edwin Rutageruka, mwenye simu Namba 0754 658881. Mtatolewa taarifa zaidi kwenye ubao wa matangazo.Naomba kuwatangazia wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji na biashara kwamba leo tarehe 28 Juni, 2007 kutakuwa na kikao kuanzia saa 4.30 asubuhi katika ukumbi wa mikutano namba 432 ghorofa ya 4 jengo la utawala na kikao hiki kimeitishwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo ya Uwezekezaji na Biashara Mheshimiwa William Shellukindo.

Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mwenyekiti, wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, anawatangazia kwamba Kamati imepanga kukutana mara baada ya kikao cha asubuhi hii saa saba. Anawaomba wajumbe wa kamati hiyo wahudhurie kikao hicho kitakachofanyika katika ukumbi namba 133 jengo la utawala. Nimeambiwa tuna wageni ambao ni madiwani 30 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe popote pale mlipo Waheshimiwa Madini msimame. Karibuni sana Bungeni.

Tangazo la mwisho Mheshimiwa Haroub Masoud ana wageni wake tunaomba wasimame hapo walipo. Ana wanne kutoka Oman ambao ni Rajab Masoud, Shehe Masoud, Bahati Omar na Ahmed Nassor Said na vile vile watatu kutoka Zanzibar ambao ni Masoud Masoud, Alka Ali Salim, Abdisalaam Haroub na mke wake Bibi Ugwa Said, mama asimame. Karibuni sana Bungeni, Dodoma. (*Makofi*)

## KAULI ZA MAWAZIRI

### Tuhuma za Ubadhirifu wa Fedha za Benki Kuu ya Tanzania *(BOT)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kutoa Kauli ya Serikali, kwa huzuni kubwa natoa pole kwetu sote kwa kifo cha Mbunge mwenzetu kijana mdogo, Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, aliyefariki juzi na anatarajiwa

kuzikwa hii leo. Tunamwomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu Amina Chifupa Mpakanjia, mahali pema peponi. Amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapenda kutoa maelezo yafuatayo kuhusiana na baadhi ya hoja zilizotolewa na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kuhusu Makadirio ya Matumizi ya fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa mwaka wa fedha 2007/2008.

Tuhuma za Ubadhirifu wa Fedha Benki Kuu:- Suala la tuhuma lililotolewa katika Benki Kuu kuhusiana na ufujaji au ubadhirifu wa fedha kwenye akaunti ya madeni ya biashara ya nje nimekuwa nikilitolea maelezo katika vipindi tofauti ndani ya Bunge au kupitia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha na Uchumi. Aidha, nimeweza kutoa ufafanuzi kwa Waheshimiwa Wabunge, wakati wa majumuisho ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2006/07 na pia kwenye maelezo yangu ya majumuisho ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2007/2008. Nilitumia fursa hiyo kuwaarifu Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na Serikali kufanya uchunguzi wa kina ili kufahamu undani na ukweli kuhusu tuhuma za ubadhirifu wa fedha katika akaunti ya madeni ya biashara ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii tena kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge kuwa, Serikali imemwagiza Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali *(Controller and Auditor General (CAG)* kusimamia uchunguzi ambapo tayari zabuni zimeshatangazwa kwa kampuni za ukaguzi za kimataifa kufanya ukaguzi huo. Zoezi hili linategemewa kukamilika kabla ya mwisho wa mwaka huu iwapo taratibu za msingi zitakamilika mapema. Mwisho wa kupeleka zabuni ni tarehe 28 Juni, 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tuhuma dhidi ya Gavana na wafanyabiashara wa hapa nchini, labda niseme tu kuwa sisi ndani ya Serikali tumeweza kuliona suala hili ikiwa limeingizwa kwenye mtandao wa *internet* na mtu ama watu tusiowajua. Serikali kupitia vyombo vyake vya dola ndio watashughulikia suala hili.

Aidha, tunapenda kutoa wito iwapo yupo mtu au kikundi cha watu kinachohusika na utoaji wa taarifa hizo kupitia mtandao wa *internet* wajitokeze na kutueleza ukweli ili taarifa zake zitusaidie kufanya maamuzi kwa maslahi ya Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *Export Guarantee Scheme.* Huu ni utaratibu wa Serikali wa kutoa *collateral* kwa wananchi wanaotaka kuzalisha bidhaa na kusafirisha nje na ndio maana ya jina la *Export Guarantee Scheme.* Hii inafanyika katika maeneo ya uzalishaji, kwa wale wenye miradi mizuri, lakini *collateral* zao hazikidhi mikopo.

Mfuko huu ulianzishwa kupitia Bunge hili na watu kadhaa wamefaidika na mfuko huu. Nia ni kuhamasisha uzalishaji nchini ili kuongeza kuuza bidhaa na kuweza kuimarisha uchumi wetu badala kama ilivyo hivi sasa ambapo nchi inaagiza zaidi nje kuliko kuuza nje.

Utaratibu wa Utoaji Dhamana ya Serikali: Kwanza kabisa, baada ya kuwa na mradi ambao ni wa kuzalisha bidhaa na kuweza kusafirisha nje unakwenda benki yako kuomba mkopo. Benki hufanya upembuzi yakinifu. Wakiona mradi ni mzuri na una lengo la kuuza bidhaa nje wanakubali kukupa mkopo.

Lakini kwa kuwa mhusika hana *collateral* inabidi apewe mkopo na kudhaminiwa na Serikali. Umuhimu wa miradi ya aina hii ni kuongeza ajira, kuongeza fedha za kigeni na kuongeza pato la Taifa pamoja na mauzo ya nje pia yaweze kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu dhamana ya mkopo iliyoombwa kwa ajili ya mradi wa *Sumbawanga Agricultural and Animal Food Industries (SAAFI)* kupitia mpango wa *Export Credit Guarantee Scheme*. Dhamana itolewayo na Serikali ni sawa na asilimia 75 (75%) ya ombi la mradi.

Kwa msingi huo mradi huo ulipewa dhamana ya mkopo ambao ulitolewa tarehe 4 Februari 2005 kwa kipindi cha mwaka mmoja hadi tarehe 4 Februari 2006. Dhamana hiyo ya Serikali ilipitishiwa Benki Kuu ya Tanzania ambayo nayo ilitoa idhini kwa benki ya *Standard Chartered* kutoa mkopo huo. (*Makofi*)

Kufuatia kuwasilishwa maombi ya *extension* ya mradi na baada ya benki ya *Standard Chartered* kuufanyia tathmini ya thamani ya mradi iliridhika kuwa dhamana ya mkopo inayohitajika inayoombwa na *SAAFI* siyo ya kulipwa katika kipindi cha mwaka mmoja na kumalizika na ili kuuwezesha mradi huo kuweza kuurejesha mkopo ilipendekezwa kuhamishiwa Benki ya Raslimali Tanzania *(TIB)* ambao ni Wakala wa Benki Kuu ya Tanzania kwa aina hiyo ya miradi ambayo inahitaji dhamana ya Serikali ya kipindi kirefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki Kuu inafanya kazi ya uwakala wa Serikali na huwa kama *conduit* ya kupitishia fedha hizo. Ni vizuri suala hili lieleweke kwa Waheshimiwa Wabunge na pia kwa wananchi. Serikali inaweza kuhamisha mpango huu kutoka Benki Kuu na kuipeleka kuhudumiwa na Wakala mwingine moja kwa moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema ieleweke kuwa lengo la utoaji wa dhamana za mkopo wa aina hiyo itolewayo na Serikali ni utaratibu wa kawaida na tunausisitizia ili kuwawezesha Watanzania kuanzisha miradi mikubwa ya aina hiyo. Na kwa mantiki hiyo, mradi wa ufugaji, uchinjaji na usindikaji nyama wa *SAAFI* ambao Mheshimiwa Mzindakaya ni Mwenyekiti wake ulipatiwa dhamana za mikopo ya muda mrefu kupitia *TIB* ambao ni Wakala wa Benki Kuu. Utaratibu huo huo umetumika kwa wakopaji wengine waliokidhi matakwa haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuwahamasisha Waheshimiwa Wabunge na wananchi ambao wanayo malengo ya kuanzisha miradi mikubwa yenye tija na ambayo itaimarisha uwezo wetu wa kuuza bidhaa nje, kutumia fursa iliyopo kwa

kuomba dhamana ya Serikali. Hii ni baada ya aina ya mradi unaotarajiwa, kufanyiwa *valuation* ili kubaini *economic viability* yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2007/2008 - Ofisi ya Waziri Mkuu na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. SAID JUMA NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwa niaba ya wananchi wa Sikonge naomba nichukue nafasi hii kutoa salaam za rambirambi kwa kifo cha Mheshimiwa Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia. Mungu ailaze mahali pema peponi roho yake. Amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetumwa hapa na wananchi wa Sikonge na nikija hapa nizingatie wakubwa wangu wa kazi ni wawili, kwanza wananchi wangu walionipigia kura, lakini mkubwa wangu wa pili ni Chama changu kilichonileta hapa. Kwa hiyo, maelezo yangu yatakuwa yanakwenda katika pande hizo mbili. Kichama niipongeze sana kwanza Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwa kazi nzuri ilizozifanya kwenye jimbo langu. Nilipoanza Ubunge simu tulikuwa tunazisikia tu. Lakini sasa hivi tuna *tigo* tunaongea, tuna *celtel* tunaongea, tuna *voda* tunaongea. Kwa hiyo, hatuna matatizo makubwa sana ya mawasiliano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kiujumla niipongeze sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwa kuleta Mapinduzi makubwa sana ya elimu hasa elimu ya msingi na baadaye elimu ya Sekondari. Kwenye elimu ya Sekondari Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Chama cha Mapinduzi kwenye Ilani tulikuwa tumeahidi tutakapofika mwaka 2010 asilimia 50 ya wanafunzi wanaomaliza darasa la saba wawe wanapata elimu ya Sekondari. Lakini leo hii mwaka huu wa 2007 tunamaliza tumevuka malengo zaidi ya asilimia 80 wanapata elimu ya sekondari haya ni mafanikio makubwa sana. Niwaombe wenzangu wapinzani mwenzio hata kama hamkubaliani katika baadhi ya mambo akifanya vizuri msifu, kwenye hili ni vizuri Watanzania wote, kwa kweli bila kuangalia itikadi tukisifu Chama cha Mapinduzi na Serikali yake katika mafanikio haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niseme yale niliyotumwa na wananchi wangu. Nianze na suala la kilimo. Yako maelezo mengi toka tupate uhuru kilimo ni uti wa mgongo, kilimo ni muhimili wa uchumi. Haya yote yanadhihirisha kwamba kilimo kina umuhimu mkubwa na zaidi ya asilimia karibu 80 ya Watanzania wanategemea kilimo. Kwa hiyo, kilimo katika Tanzania kwa kweli ni muhimu sana kwa wananchi wetu na kwa Maendeleo ya wananchi wetu. Sasa huwezi ukaleta Mapinduzi ya kilimo bila wananchi hawa wanaofanya shughuli za kilimo kuwawezesha kupata mbolea.

Mbolea kwa sasa ina gharama kubwa. Kwa hiyo, wananchi wetu wengine wanashindwa kutumia mbolea kuleta Mapinduzi ya kilimo kwa sababu ya gharama si kwa sababu hawataki kutumia mbolea. Lakini Serikali ya Chama cha Mapinduzi ikajitahidi ikaamua kutoa ruzuku ya pembejeo. Sasa hapo ndiyo nataka kusema maneno. Serikali imeanzisha mpango huu wa ruzuku ya pembejeo hasa kwa mbolea, lakini nasema mbolea hii ni sadaka. Sadaka kwa mawakala, sadaka kwa wafanyabiashara. Haiwafikii wananchi au haiwafikii wakulima kule na hawafaidiki nayo.

Nataka nitoa mifano hapa. Mbolea Tabora mwaka jana tumewaomba sana, tumeiomba Wizara, tumeiomba Serikali, tunaomba mbolea hii wasipewe makampuni ya tumbaku. Mbolea yote ya ruzuku mmepeleka kwenye makampuni ya tumbaku. Sasa yalivyowanyonya wananchi, mbolea ya *NPK* Tabora iliuzwa shilingi 24,000 makampuni haya ya tumbaku yamewakopesha yamechukua ile mbolea ya ruzuku mliyowapa kwamba wao ndiyo wasambaze yamewakopesha wakulima 32,500 zaidi ya shilingi 8,500. Mbolea wanayopewa ruzuku na Serikali wao wanawakopesha wakulima zaidi ya shilingi 8,500 kwa mfuko. Mbolea ya *Urea, Urea* ruzuku Tabora iliuzwa shilingi 17,500 makampuni haya ndiyo mkayapa yenyewe yakawakopesha wakulima kwa mbolea hiyo hiyo ya ruzuku shilingi 28,750 zaidi ya shilingi 11,250. Ni unyonyaji huu! *CAN*, Tabora mbolea ya ruzuku iliuzwa shilingi 17,500, makampuni yakachukua ile mbolea ya ruzuku yakawakopesha wakulima shilingi 25,500. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kama kungekuwa na wakala mwingine au shirika wangechukua hiyo nafasi ya kufanya hivyo tusingefika mahali tukawa na zaidi kubwa kiasi hiki. Sasa naiomba Serikali kama hiyo ruzuku ipo mwaka huu msiwape makampuni ya tumbaku. Pelekeni mbolea kwenye *SACCOS*, pelekeni mbolea kwenye ushirika ili vyombo hivi viweze kuwapa wananchi kwa bei nafuu. Hii nasema sasa kwa nchi nzima isiwe tu kwa Tabora. Ruzuku ya mbolea ipelekwe kwenye vyombo ambavyo vinaweza vikawasaidia wakulima siyo vyombo ambavyo vinafanyakazi tena ya unyonyaji. Faida gani hiyo ya biashara maana hata vitabu vya mwenyezi Mungu vinakataza biashara iwe na faida kubwa. Fanya biashara lakini faida wewe baki nayo na yule unampa msaada basi naye afaidike. Utaona hiyo ruzuku baada ya wao kukopesha hivi sasa yamemrudia mkulima shilingi 610 baada ya wao kutoa gharama zao kwa kila mfuko. Shilingi 610 kwamba hiyo ndiyo ruzuku ya Serikali. Mmesikia maneno haya. Sasa mimi niombe kwenye hili tuelewane mbolea sasa ya ruzuku sasa ielekee huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni barabara. Barabara ni roho ya uchumi wa Taifa. Tabora, Kigoma, Rukwa, tuna matatizo makubwa sana ya barabara. Kwenye hili tutaendelea kusema sana kwa sababu ukija husemi habari ya barabara hueleweki huko Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwenye suala la barabara ukiona mtu anazungumza hapa suala la barabara hayo ndiyo tunayotumwa na wananchi wetu. Sasa nikija hapa nikaanza kuzungumzia habari ya bahari mtanicheka kwa sababu kwetu hakuna bahari nazungumzia habari ya barabara. Kuna matatizo, mimi naiomba Serikali kwa Mkoa kama wa Tabora tukitaka kuufungua Mkoa wa Tabora hebu hii barabara ya Itigi kuja Kigwa kwenda mpaka Tabora kupitia Urambo kwenda mpaka Kigoma tuitengeneze. Napongeza sana jitihada za Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, amekuja Tabora na anatupa ahadi na napongeza jitihada zake za kuhangaika huko na kule kutafuta fedha za

kuhakikisha barabara ile inajengwa. Sasa na sisi tujitahidi basi tunapopanga Bajeti kwa fedha za ndani tusisubiri fedha hizo za wafadhili maana mnaweza mkazipata mnaweza msizipate na sisi tunataka barabara. Barabara nyingine ni ile inayotoka Nzega, kuja Tabora kufika Ipole. Inapofika Ipole inakwenda Ruangwa nyingine inakwenda Mpanda mpaka Rukwa – Sumbawanga. Sasa hii barabara mwaka jana Mheshimiwa Mramba aliniahidi hapa kwamba kaa tulia tutaishughulikia hii barabara, leo mwaka huu imetengewa shilingi milioni 300 barabara ndefu kiasi hicho zaidi ya km 200 milioni 300 na barabara yenyewe ilishafika mahali iko hoi. *(Makofi)*

Kuna siku moja tungeweza hapa tukahamisha Makao Makuu, mkaja kule mkaona barabara zilivyo. Barabara zingine hapa unaweza ukakaa kwenye basi unakunywa na kikombe cha chai zimetengewa fedha za ukarabati bilioni 20 sisi barabara ambayo imechakaa haina lolote milioni 300 hii haki kweli jamani! Sisi wote ni Watanzania na fedha hizo zote za Bajeti na Serikali za kwetu wote. Kwa kweli inauma sana. Mimi namtafuta huyu maana tukizungumza hapa sungura sijui mdogo tunagawana, sasa huyu anayegawa wengine anawapa kubwa mimi ndiyo namtafuta ni nani huyu. Huyo mgawa sungura anawapa wengine kikubwa, wengine kidogo ni nani? Huyo kama ni sungura tugawane basi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ndugu yangu Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, alikuja kule, tumempitisha yale maeneo na nina imani siku hiyo alilala hoi. Hee, ndiyo Tanzania hiyo, maeneo mengine daraja tu likivunjika mtasikia Waziri fulani kaenda sijui nani, sisi madaraja yanavunjika na nini hakuna mtu, jamani hii Tanzania au Tanganyika?

Mimi niombe sana suala la barabara na sisi tunashida huko, naomba sana suala la barabara na wakati mwingine sisi tunataka hata changarawe tu, tupate changarawe tuweze kupita wakati wa masika na kiangazi nayo inashindikana. Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, tumempitisha mbugani katika maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie maji, nikuombe sana Waziri, niombe Sikonge kwa sasa watu wanaoweza kupata maji safi na salama ni asilimia 11.1, ni mbaya sana. Lengo letu mwaka 2010 tufike 65 asilimia. Sasa tunayo kazi kubwa, kwa hiyo, niombe sana jitihada vile vile za Serikali kuhusu suala la maji basi zipewe msukumo mkubwa. Matatizo ya maji yametupa shida nyingi, matumizi ya maji kwa wananchi wetu. Lakini vile vile mifugo na miradi mingi ya ujenzi nayo inakwama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana vile vijiji 10 ambavyo vilielekezwa basi viweze kufanyiwa kazi. Mwisho Naibu Waziri wa Maji aliahidi kuja Sikonge, sasa nimeonana na akina Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, sijui na akina nani nao wanamwomba. Ah, ukienda ofisini *file* lile la kwanza ndiyo linaloshughulikiwa kwanza. Sasa aanze kwanza Sikonge, ashughulike na Sikonge, hao wengine akina Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, akina nani wanaomba mwisho ndiyo atakwenda. Lakini aje kwanza Sikonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya haya naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ALI SAID SALIM:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti na mimi kunipa nafasi hii nizungumze machache katika Bajeti hii iliyowasilishwa mbele yetu na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Lakini awali ya yote....

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, naomba uweke chombo cha kuzungumzia vizuri ili uweze kusikika.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini awali ya yote kwanza nichukue nafasi hii nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye asubuhi hii ya leo katujalia mimi na sisi sote kuamka tukiwa na roho na tukiwa na afya njema. *(Makofi)*

Baada ya shukrani hiyo kwa Mola nichukue nafasi na mimi kutoa salamu za pole na za rambirambi kwa msiba ambao umetupata siyo kwa wazazi tu wa Amina Chifupa, lakini kwa kweli ni Waheshimiwa Wabunge wote na Watanzania kwa ujumla. Mungu aiweke roho ya Marehemu mahala pema peponi. *Amin.*

La nyongeza katika hilo ni kusema tu ni kwamba *Inallilahi wainailahi rajuun* yaani sote sisi ni wa Mwenyezi Mungu na kwake hatuna budi tutarudi. La kutakiwa kwetu sisi ni kumwombea dua na ni kusema tu kwamba ikiwa yeye alikuwa mwema basi Mwenyezi Mungu amzidishie wema wake, na kama alikuwa ni mwovu basi Mwenyezi Mungu, amsamehe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa naomba nikijikite katika mambo mawili, matatu ambayo nilikusudia kuyazungumza. La kwanza ambalo nataka nilizungumze ni suala la maafa katika nchi yetu. Nashukuru Serikali imeunda kitengo maalumu ambacho kinashughulikia masuala ya maafa. Serikali imejitahidi sana kutoa fidia au vifuta machozi kwa waathirika mbalimbali katika nchi yetu sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi yetu tulipata maafa mwaka 2001 kule Zanzibar. Maafa ambayo yalipelekea watu wengi kufariki na wengine kupoteza viungo vya miili yao, wengine leo ni Marehemu na wengine ni mayatima. Kwa upendo Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu aliiunda Tume kwenda kushughulikia suala hili na Tume ilikuja Pemba ikafanya kazi nzuri na kupeleka ripoti kwa Mheshimiwa Rais na miongoni mwa mapendekezo yake Tume hii ilitaka kwamba watu ambao wamefanyiwa tathmini basi walipwe fidia au kifuta machozi kwa jina lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipoingia katika Bunge hili mwaka 2003 niliulizia suala hili na kwa ushahidi ninayo *Hansard* hapa ya mwaka 2003, niliuliza suala hili tarehe 4 Novemba, 2003 na likajibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu wakati huo Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera alikuwa Mheshimiwa William Lukuvi ambaye sasa ni Mkuu wa Mkoa alijibu swali hili. Serikali ilitoa maelezo marefu. Lakini niyarudie yote lakini naomba nisome sehemu ya mwisho ya majibu ya Serikali. Serikali baada ya kutoa maelezo na kukubali kwamba iko haja kweli ya kulipa hicho kifuta machozi na si fidia.

Lakini mwisho alimalizia Serikali kwa kusema hivi; "Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge na waathirika wa maandamano hayo waendelee kuvuta subira wakati suala hili linashughulikiwa. Pili taratibu hizo zitakapokamilika wahusika wataarifiwa kwa uwazi wa kutosha kulingana na mazingira yenyewe."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulipita mwaka 2003, ikawa ni kimya, mwaka 2004 suala hili tukaliuliza tena, tukapata majibu mfano kama huu. Tukanyamaza, mwaka 2005 mimi binafsi nikarudia tena kuliuliza suala hili, lilipangwa kwenye *Order Paper* kwa bahati mbaya halikuja kwenye *Order Paper* nilipewa taarifa kwamba suala lako litajibiwa tarehe fulani kwenye *pigeon hole,* lakini siku ile ilipofika kwenye *Order Paper* halikuwepo, nikamwandikia Mama Mmbaga kumwuliza swali langu vipi? Majibu akaniambia kwamba bado Serikali haijakuwa na majibu. Kwa kweli hadi leo hii, ilikwenda Awamu ya Tatu mpaka ikamalizika. Suala lile halikupata ufumbuzi. Tumeingia katika Awamu ya Nne wakati nachangia hotuba ya Mheshimiwa Rais, mwaka jana pia nilitaja suala hili kwa uchungu kabisa, lakini la kusikitisha ni kwamba bado hadi leo suala hili liko kimya. Ni jambo la kusikitisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu maafa yametokea sehemu mbalimbali kwa mfano hapa Dodoma, ilitokea maafa ya treni na walioathirika Serikali iliagiza na walilipwa. Lakini kwetu sisi hadi leo suala hili kwa kweli limeshindikana. Sasa linatupa mushkeri kwa sababu hii ni nchi moja na asilimia kubwa katika waathirika hao ni sehemu ya Pemba. Katika asilimia 95 au zaidi ni Wapemba. Sasa mimi napata mushkeri kwa nini sehemu nyingine waathirika waweze kulipwa kwetu sisi iwe ni tatizo hadi leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli hili halitoi picha nzuri na Mheshimiwa Waziri Mkuu sisi Wapemba kwa kweli niseme hatuna pingamizi yoyote na Serikali ya Muungano. Sisi tunaikubali Serikali ya Muungano lakini tunaomba na Serikali yenyewe isitutenge. Imani ambayo tunaionyesha kwa Serikali ya Muungano kushirikiana nao katika kufanya kazi basi na sisi panapotokea tatizo basi Serikali iwe kifua mbele katika kutushughulikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika kumalizia hoja hii naomba Serikali, Mheshimiwa Waziri Mkuu unasikia na watendaji wako wote, sana sana Mheshimiwa Waziri Mkuu fidia hii kwa watu hawa haitazidi shilingi bilioni 1.5. Sidhani kwamba Serikali itashindwa kupata shilingi bilioni moja na nusu kuweza kulipa hawa na kero hii ikaondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba katika kutekeleza azma ya Serikali hii ya Utawala Bora basi sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu nakuomba sana kabla hujanyanyuka hili suala ulichukue na nakuomba hili ulichukulie juhudi kubwa, litakujengea heshima kubwa, si wewe tu, lakini pia na Serikali yako. Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti kwa haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo nataka nizungumzie ni suala la wajasiriamali. Nashukuru kwamba Mheshimiwa Rais ametoa shilingi bilioni moja kila mkoa kwa ajili ya wananchi kujisaidia katika shughuli zao za maendeleo. Ni jambo zuri, isipokuwa naomba nitoe tahadhari, hasa kwa upande wetu wa Zanzibar na hasa Pemba, naomba fedha hizi zitakapokuwa tayari basi zisimamiwe vizuri. Naomba zisije zikagawiwa kwa kupitia taratibu za kisiasa. Hizi ni fedha za wananchi, tunaomba zitakapokwenda Pemba basi zihudumie wananchi wote bila ya kutizama itikadi ya kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana Serikali ya Muungano iwe macho ili watu wote ambao walikusudiwa kupata faida katika pesa hii basi ziweze kuwanufaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, ni suala la ukeketaji. Hili limekuwa ni tatizo kubwa kwa kweli. Wananchi mbalimbali, taasisi mbalimbali, zimekuwa zikipiga kelele kulaani tendo hili. Lakini pamoja na jitihada zote za Serikali, taasisi binafsi, taasisi za Serikali, binafsi *NGO,* Masheikh, Mapadri na watu wengine kukemea uovu wa suala hili lakini bado ndio unasikia hapa limetendeka, pale limetendeka. Kwa hiyo, inaonekana bado kutakuwa kwa kweli kuna hitilafu na kwa kweli suala hili si la mzaha, suala la ukeketaji si jambo la mzaha kwa sababu linaondoa huyu mfanyaji, linaondoa ubora wa ile mali yenyewe, kabisa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kweli katika hali kama hii si jambo la kuvumiliwa kabisa kabisa. Mimi nadhani sasa imefika wakati Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ulete sheria hapa Bungeni, ukubali kuweka sheria kali juu ya watu wote watakaohusika na suala hili la ukeketaji na nadhani mimi sheria pekee ambayo itawafaa na suala hili kukoma haraka haraka basi ni kuleta sheria ya kunyongwa kwa yeyote ambaye atapatikana na hatia ya kumkeketa kijana yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo kuna suala la wanafunzi. Juzi nilihojiwa kwenye kipimajoto kwamba je, hawa watu wanaoharibu kwa kuwapa mimba watoto wa shule wafanywe nini? Mimi nikawaambia wahasiwe. Lakini mimi kwa kweli nadhani haitoshi hii, nabadilisha msimamo wangu kwamba hii haitoshi. Mimi nashangaa kwa kweli, watu mnakwenda kwa wanafunzi, watu wazima wapo kwa shughuli hii tu *special* kwa nini uwaache watu hawa uende ukaathiri watoto wadogo ambao unawaharibia maisha yao? *(Makofi)*

Kuna watu ambao leo wamekubuhu kwa shughuli hii kwa nini usiende hapo uende ukashughulikie na watoto wadogo? Kwa kweli Serikali hili Mama Margaret Sitta, nakuomba hili suala lishughulikie na usifanye mzaha katika hili, waokoe watoto wetu. Mimi nadhani iko haja kuweka sheria kwamba yeyote atakayebainika kumbaka au kumpa mimba mtoto wa shule basi hukumu yake iwe ni kunyongwa hadharani kabisa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi ni unapokuja kusikia kwamba mimba ile aliyempa ni mwalimu, hii kwa kweli inauma sana. Mimi nilikuwa Mwalimu nimefundisha mpaka darasa la 12 lakini nilikuwa mtu mwenye nidhamu kabisa kwa wanafunzi wangu, kwa sababu ninaamini kwamba mwanafunzi wako ni mtoto wako.

Sasa inakuwaje unafanya hamu mpaka unakwenda kumwingilia na kumpa mimba? *(Makofi)*

Sasa mimi nadhani kwa mwalimu haitoshi ni kunyongwa, lakini anyongwe na baadaye mwili wake uwekwe kwenye kioo uonekane kwamba huyu ni muovu ili iwe ni funzo kabisa, si jambo la kucheka Waheshimiwa ni jambo ambalo kwa kweli ni la kutafakari na tukazingatia na tukachukua hatua muafaka. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo matatu yaliyobakia, kwa haraka haraka sijui kama nitamaliza. Lakini niliuliza suala la JKT na JKU. Waziri akataja kwamba JKT si la Muungano. Hili suala limeleta utata, watu wengi walikuwa wanadhani kwamba JKT ni la Muungano na kwa sura ilivyo JKT ukiambiwa ni jeshi la upande mmoja kwa kweli haipendezi. Mimi nadhani kama hivyo ndivyo, kwamba JKT ni jeshi la upande mmoja tu wa Tanganyika, basi mimi nadhani iko haja ya jeshi hili kuligeuza likawa ni jeshi la Muungano na tukishaligeuza kuwa ni jeshi la Muungano basi tena hapo hakutakuwa na sababu ya kuwa na JKU kule Zanzibar. Kwa hiyo, nadhani kama hatujafanya hivyo, tufikirie kuligeuza JKT iwe ni jeshi la Muungano na kwa hivyo ule ulazima wa kuwa na majeshi mawili katika nchi mmoja basi utaondoka na kwa hivyo a*utomatically* JKU itakufa kimya kimya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka nilizungumzie ni suala la Afrika ya Mashariki, Shirikisho hili linatajwa. Kwa kweli bado ndani ya nchi yetu tuna matatizo mengi...

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mwongozo Mwenyekiti.

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI:** Kuhusu Mwongozo.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mjumbe alipokuwa anaendelea kuchangia alisema kwamba JKT ni jeshi la Tanganyika, sasa naomba hiyo Tanganyika iko wapi, au afute usemi wake.

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ali Said Salim, umemsikia Mheshimiwa Tahir, unaweza kurekebisha maneno hayo?

**MHE. ALI SAID SALIM:** Ndiyo Mwenyekiti, ulimi uliteleza. Ni jeshi la Tanzania Bara. Hivyo naomba kufuta usemi wangu kwamba ni jeshi la Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme hilo suala la Afrika Mashariki kwamba bado tuna matatizo katika nchi yetu juu ya Muungano wetu, kuna kasoro kadhaa wa kadhaa ambazo zinahitaji kufanyiwa marekebisho.

Kwa hiyo, sisi kabla ya kuelekea kwenye Shirikisho nadhani ni vyema kwanza mambo mengi ambayo tunayo ndani ya nchi yetu basi yaweze kufanyiwa marekebisho na

yaweze kusawazishwa baada ya miaka pengine 100 inayokuja tukafikiria suala la kufanya hilo Shirikisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho la kero hizi za Muungano. Moja katika jambo limekuwa ni tatizo na tumeliuliza mara nyingi tu humu Bungeni ni suala la magari haya yenye usajili wa ZNZ imekuwa ni tatizo kubwa kwamba unapopatikana na gari ZNZ kwa upande wa Bara kwa kweli inakuwa ni kosa kubwa hasa, unashangaa kwamba hii ni nchi moja.

Tunaambiwa ni nchi moja inakuwaje gari yenye usajili wa ZNZ ukija nayo Tanzania Bara inakuwa ni tatizo kuiendesha lakini namba za "T" ambazo zinatoka huku za Muungano zile zikija kule basi kwa kweli inakuwa ni halali kabisa kutumia, hata sisi magari mengine tuna namba za huku. Sasa kwa kweli haileti picha nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba Serikali juzi ilisema kwamba suala hili linaonekana kwamba ni tatizo na limeundiwa Tume ili kuona namna bora ya kuweza kulirekebisha. Naomba sasa Tume hiyo iweze kufanya haraka kulirekebisha ili udhia huu kwa watu uweze kuondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, ni suala la wafugaji wa Mbarali. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira. Mwaka jana tulipata nafasi kwenda kutembelea sehemu hii ya Bonde la Ihefu. Tulikwenda kule kuangalia na kuona namna ambavyo zoezi hili linatekelezwa. Pamoja na kuwa Serikali ilikuwa na nia njema kabisa ya kutunza vyanzo vya maji, lakini kwa kweli Serikali ikubali kwamba maandalizi yalikuwa ni hafifu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kutokana na uhafifu wa maandalizi hayo kwa kweli zoezi lile limepelekea maafa makubwa. Ndiyo nimemaliza? Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni namba 55 naomba Mwongozo wa Mwenyekiti.

Mheshimiwa msemaji aliyekaa alizungumzia kuhusu Jeshi la Tanzania Bara, pengine angefafanua ni jeshi gani hilo la Tanzania Bara? *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI:** Alikuwa akiongelea JKT ukiitofautisha na JKU. Tunashukuru tunaendelea. *(Makofi)*

**MHE. RAMADHANI A. MANENO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Kwanza nami kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Chalinze, nitoe pole kwa aliyekuwa Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Amina Chifupa, Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake yenye matumaini kwa wananchi, yenye matumaini kwa

Taifa letu hili hasa pale walipogusa maeneo mbalimbali kama miundombinu, afya, elimu, kilimo, udhibiti wa dawa za kulevya, rushwa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hii yote ni utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, chama ambacho wananchi wa Tanzania hii wanakipenda na ndiyo ambacho wanachokiona kinaweza kikawaletea maisha bora kwa kila Mtanzania. *(Makofi)*

Katika mchango wangu nianze kwanza na *TASAF II* imeanza kutekeleza majukumu yake maeneo mbalimbali lakini lipo tatizo la mlolongo au ucheleweshaji wa kupatikana kwa fedha hizo kwa wanavijiji ambao tayari wamebuni miradi yao au wameibua miradi yao kwa ajili ya maendeleo kama vile ya Zahanati, Barabara na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanapoibua miradi yao baada ya kupeleka mchanganuo wao kwenye Halmashauri za Wilaya au kwa Mkuu wa Wilaya lakini baada ya kikao au Kamati ile ya Maendeleo ikishakaa pale Wilayani ndani ya Halmashauri wanapeleka tena kwenye Idara ya *TASAF* Makao Makuu na hatimaye wao kuanza kupeleka kwenye Wizara husika ili ziweze kupitia mchanganuo huo na hatimaye kuweza kuwapa pesa. Lakini takriban inachukua miezi mitano au sita hatimaye hizo pesa kuweza kupatikana na kuchelewa ile dhamira ya jambo lenyewe lililokusudiwa na wale wananchi kwenye maeneo yetu ya vijiji. Tungeomba Serikali basi, ilitilie mkazo suala hili kupunguza mlolongo mrefu wa upatikanaji wa pesa za *TASAF*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la afya. Tunamshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema katika mikakati yetu sasa tutaelekeza nguvu zetu kwenye zahanati na vituo vya afya. Ni kweli, wananchi wamelipokea sana jambo hili na wamelipokea vizuri kwani suala la afya ni jambo la msingi sana kwenye maeneo yetu. Lakini vituo vya afya na zahanati vitakavyokamilika basi viende sambamba na watumishi kwa maana ya waganga na wauguzi. Isije ikatokea tena kama hili suala letu la elimu kwenye shule za sekondari zingine hadi sasa mpaka hivi leo bado zina upungufu wa walimu. *(Makofi)*

Lakini nina imani kwa mikakati iliyopo ndani ya Serikali yetu hii ya Chama cha Mapinduzi, jambo hilo litachukua nafasi nzuri ya kuweza kupata waganga na wauguzi. Lakini vituo vyetu vya afya vilivyopo sasa hivi navyo havina hadhi kabisa ya kuwa vituo vya afya, mgonjwa akienda pale anakata tamaa. Vituo vya afya hakuna vitanda, hakuna maabara, hakuna dawa na vitu mbalimbali vinavyoweza kumsababishia au vinavyoweza kumpa nguvu mgonjwa ya kuweza kurudi kwenye afya yake.Utakuta chumba cha akinamama wanaokwenda kujifungua kitanda kimoja, anamsubiri mwenzake akiwa sakafuni ili amalize pale kitandani na yeye naye aweze kupandishwa pale kitandani. Ni jambo la hatari sana na nimelishuhudia pale kwenye kituo cha afya cha Chalinze. Hali imekuwa mbaya kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo kile cha Afya cha Chalinze, kimebadilishwa jina, ilikuwa zahanati na sasa Kituo cha Afya. Lakini sambamba na kubadilisha jina basi

Serikali ingeona jina liende sambamba na badiliko la jengo, lile jengo lilikuwa la zahanati, ilikuwa inawahudumia wanavijiji wa vijiji kama viwili. Lakini leo hii vijiji visivyopungua 11 vinaenda kutibiwa kwenye kituo kile cha afya. Ni mrundikano mkubwa sana wa wagonjwa, msongamano mkubwa sana wa wagonjwa na mimi nikuombe kama wenzangu wanavyowaomba Manaibu Waziri kutembelea maeneo haya, basi na mimi kwa ruhusa yako nimpate Naibu Waziri wa Afya twende pale Chalinze, akaone yale mazingira ya mrundikano wa wagonjwa pale jimboni kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwani haya maombi naona ukiyaomba humu kupitia kwa Mwenyekiti au kwa Spika, unaweza ukapewa huyo Naibu Waziri ukaenda naye kwenye hiyo safari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiit, nije kwenye suala la Kitengo cha Maafa ambacho kiko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kitengo hiki ni kweli kinajitahidi kwa hali na mali kuhakikisha panapotokea maafa wanaweza kwenda kutibu haraka sana au kuwapelekea baadhi ya mahitaji hawa wananchi. Lakini kama walivyosema Wabunge wenzangu hawatazami kwa kina, kuna hali ya upendeleo fulani pale ambapo kwenda kutibu hayo maafa.

Mheshimiwa Mwenyekiit, mafuriko yamesababisha kuharibika kwa barabara nyingi sana hapa nchini, lakini unakuja kuona barabara zinazotajwa za maeneo mengine lakini upande mwingine hauwezi kutajwa kama ni eneo la kwenda kutengenezewa hizo barabara. Ninazo barabara kule kwangu zimechoka kweli kweli hazipitiki. Lakini kisa ni hayo mafuriko kwa namna moja au nyingine ndiyo maafa. Kuna barabara kama ya Lugoma – Talawanda barabara ya Ubena - Tukamisasa, barabara ya Mjembe – Gore, barabara ya Kwamduma-Mjembe, Mkange – Java, barabara ya Kiwangwa - Mkenge. Barabara hizi hazipitiki kabisa kabisa, basi katika kitengo chetu kile cha maafa kwa sababu walituambia hapa zipo pesa za kuweza kwenda kuhakikisha maeneo yaliyokuwa yameharibika ziweze kufanyiwa ukarabati basi hizo pesa zitoke kwa haraka sana ziende zikasaidie kwenye tatizo hili. Ninachokiona hapa Waziri Mkuu anayo kasi kweli kweli ya kuweza kuhakikisha na kutaka kuona kwamba jambo lolote linaloleta kero kwenye nchi hii linapata tiba, lakini wenzake wanaomsaidia nina imani kasi hii hawaendi nayo sambamba kwani sehemu zingine bado hatujaweza kupata tiba ya matatizo vile yanavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala hili la matatizo yaliyojitokeza kwenye Halmashauri zetu na kupata hati chafu na matatizo mengine ya hapa na pale. Lakini kweli utakuta kabisa kwenye Halmashauri unakuta kama *audit query* nyingine ni za kujitakia, nyingine ni za kuona kabisa watumishi wetu kwa kweli hawaendani sambamba na kasi yetu. Kwa nini ipatikane *audit query, audit query* nyingine ni *transaction* tu utakuta hawakwenda kuchukua *statement* kwa ajili ya kuweka vizuri kwenye *cash book.* Hapo unakuta mnapewa *audit query. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiit, lakini tatizo lingine unakuta kwamba ni suala ambalo vitabu vya risiti havionekani kwa muda wa miaka miwili. Halmashauri inapigwa *audit query.* Ukija kuzijibu hizi *audit query* vitabu vinavyotafutwa hata utunzaji wenyewe

hauridhishi na ndiyo unaochangia *audit query* zingine za makusudi tu. Ni watu ambao hawaitakii mema nchi hii au hawataki hii kasi inayoelekeza vizuri na Mheshimiwa Rais wetu pamoja na Mheshimiwa Mheshimiwa Mkuu ya ari, kasi na nguvu mpya. Kama nia nzuri ya Waziri Mkuu kutaka sasa tukimbie, lakini baadhi ya wenzake wanaomsaidia hawataki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule mpya za sekondari tumejenga, nashukuru sana. Lakini wanafunzi wetu kwa kweli wanapata taabu inapotokea huduma ya afya ya kupelekwa hospitali au kwenye zahanati. Basi shule zinunuliwe hata *Bajaj* ziweze kuwasafirishia hawa watoto waweze kupelekwa hospitali. Kwani wanapata taabu sana, shule zingine ziko umbali wa kilomita mpaka 50, 60. Mtoto anapoumwa pale hakuna uwezekano wowote wa kumpeleka hospitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mikopo ya elimu ya juu ya wanafunzi hawa wa elimu ya juu. Wanafunzi wale hawaelewi msemaji ni nani. Kila chuo kinazungumza vyake. Wapo wanafunzi hawakufanya mitihani, wengine wamefanya mtihani siku ya mwisho ya kumalizika kwa mitihani, lakini tatizo kila chuo kina tamko lake. Serikali sasa itamke tatizo ni nini na kwa nini kuna migomo ya wanafunzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hili tujihadhari sana na Serikali, hawa wanafunzi wa sasa hivi wanaoanza migomo ndiyo watakaokuwa viongozi wa kesho, ndiyo watakaokuwa wafanyakazi wa kesho. Sasa tunajaribu kuwajenga katika mazingira ya migomo. Lakini chanzo ni nini? Serikali iwe na tamko moja la kuona kwamba wanafunzi inawasaidiaje kuhusu suala la mikopo. Kila chuo kina tamko lake, ndiyo maana kuna baadhi ya maeneo vyuo vingine wamefanya mitihani, wanafunzi wengine kwenye baadhi ya vyuo hawakufanya mitihani. Tufikie mahala Serikali iondokane na suala hili la migomo. Kwa nini wanaweka migomo baadaye kunatokea mazungumzo ya kusitisha migomo na kutoa masharti magumu ya wanafunzi, kwa nini tufikie huko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwa haraka haraka ni kuhusu posho ya Madiwini, tufikie mahali naye hizi 60,000/= kwa kweli ni ndogo, wafikiriwe nyongeza zaidi ya 60,000/=. Hawa nao wanapigwa sindano kama vile Wabunge, Wabunge wanapigwa sindano kweli kwa maana ya kutolewa chochote kwenye mifuko yao na Madiwani nao vile vile wana wapiga kura wao, jinsi gani wanavyoweza kuwasaidia katika huduma za hapa na pale. Lakini nashukuru Waziri Mkuu kwa kuanzisha masjala ya ardhi ya vijiji nampongeza sana itapunguza kero. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nami nijaribu kuzungumza katika Bunge lako hili nimesema mwaka jana na mwaka huu nitasema. Kwa sababu nimeona kwa uzoefu wenzangu waliopata Wilaya wamesemea humu na mimi naye sitoweza na sitaacha kusema, Chalinze ifikirieni muipe Wilaya, kwani kama idadi ya watu nimesema wapo wa kutosha, hata magorofa sasa yanajengwa pale Chalinze. Kwa hiyo, ni ishara tosha tu ya kuonyesha mji unaanza kuneemeka na unastahili kupata Wilaya, sitachoka kusema mpaka kieleweke kama anavyosema Mheshimiwa Freeman Mbowe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, sina shaka kabisa na hotuba hii ya Waziri Mkuu na nina imani hata ndugu

yangu Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, ni mjumbe wa Kamati hii tulikaa pamoja kule Dar es Salaam kuipitisha kwa uzuri sana hotuba ya Waziri Mkuu nina imani yeye ni utaratibu tu kuwepo upande wa pili, lakini kwa nafasi ya mjumbe wa Kamati hii tulishirikiana pamoja kupitisha hii Bajeti au hii hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na yote ambayo nilikuwa nimeyazungumza, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja hotuba ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nami napenda niungane na wenzangu kwa niaba yangu mimi binafsi na wananchi wa jimbo la Mpanda Kati katika kutoa salamu zetu za rambirambi na pole kwako wewe wa Wabunge familia ya Marehemu Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia. Ni dhahiri kabisa Marehemu Amina alikuwa mfano na tumaini la viongozi vijana katika nchi yetu, Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo mimi napenda nizungumzie mambo mawili, matatu. Awali ya yote nilikuwa nataka kutoa mwaliko mimi nitakuwa tofauti kidogo, sikutaka kumuomba Waziri yoyote nilikuwa nataka kumualika Mheshimiwa Waziri Mkuu aje kutembelea Jimbo la Mpanda Kati na Wilaya ya Mpanda kwa ujumla wake. Nimetumwa hivyo na wananchi wa jimbo langu kwamba tafadhali kamualike Mheshimiwa Waziri Mkuu, na ikiwezekana Makamu wa Rais waje watembelee Mpanda na wananchi hao wana sababu mahususi ya kutaka kuwaalika viongozi hao wa Kitaifa waje Mpanda kwa sababu ya uzoefu uliojengeka kwamba barabara zinatengenezwa pale tu viongozi wa Kitaifa wanapotembelea katika maeneo, ama wakati wa mbio za mwenge. Kwa hiyo, wanataka na Waziri Mkuu aje Mpanda ili barabara ziweze kutengenezwa. *(Makofi)*

Baada ya kutoa mwaliko huo nilikuwa pia napenda nimuombe Mheshimiwa Waziri Mkuu akipata wasaa kabla hajaondoka Dodoma atembelee kwenye Bwalo la Polisi Dodoma, aangalie yale makazi ya askari polisi, zile nyumba ambazo zinazunguka Bwalo la Polisi Dodoma. Kwa kweli inasikitisha, ni jambo ambalo halifurahishi katika nchi ambayo leo inajivunia Uhuru wa zaidi ya miaka 45, askari wake bado wanalala katika nyumba kama zile zinazozunguka Bwalo la Polisi Dodoma na si Dodoma tu hata Tabora na maeneo mengi ya makazi ya askari wa polisi ni duni, hayafanani kabisa na kazi wanazofanya askari hawa hazifanani na hali ya unadhifu na nidhamu waliyokuwa nao askari wetu. Askari unapowaona nje wanapendeza, wasafi wananidhamu, watiifu lakini hajui askari hawa wanatoka katika nyumba gani, Mheshimiwa Waziri Mkuu ukipata wasaa zunguka pale uzione zile nyumba, nadhani ipo haja sasa Serikali kuangalia ni namna gani tunaweza kuboresha makazi ya askari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutoke katika kujenga nyumba za vioo Dar es Salaam, haya mashirika yetu ya fedha ya mifuko ya akiba yanawekeza katika kujenga majumba makubwa marefu ya kifahari ya vioo kule Dar es Salaam, kwa nini wasiwekeze sasa katika kujenga makazi ya nyumba nzuri za wafanyakazi wa Serikali na hasa askari wetu ambao watakuwa wanalipa kodi kama wanavyolipa matajiri ambao wanapanga hayo

majumba ya vioo kule Dar es Salaam. Nilikuwa nadhani sasa hivi Serikali iangalie ni namna gani itaboresha makazi ya askari polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hilo nilikuwa napenda nimuombe Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba aliwahi kutoa agizo ndani ya Bunge hili kuhusu madai ya mafao na mirathi na akatuomba Wabunge tufuatilie hilo, kwa masikitiko makubwa napenda kumuarifu Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kwamba ametujengea fitina kubwa baina ya wapigakura na Wabunge wao. Inapofikia Mbunge mwaka mzima anafuatilia mafao na madai ya mirathi ya wapigakura wake na anashindwa kupata, kuna tatizo kubwa sana Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewahi kumsikia Mheshimiwa Waziri wa Fedha akiwakumbusha wafanyakazi na watendaji wa Wizara yake ya Hazina wajenge mazingira bora ya kuhakikisha kwamba mafao yanalipwa katika wakati kwa sababu na wao pia siku moja watakuwa ni wastaafu na watahitaji kulipwa mafao yao. Hili namuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu alianglie kwamba tunapata usumbufu katika kufuatilia mafao hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeyawasilisha kwa Mawaziri na bado watendaji wameshindwa kushughulikia, kibaya zaidi na kinachoumiza ni pale mtu anayedai mirathi anakuja na *blue card* anategemea angalau hizo siku zake chache zilizobaki za maisha yake aweze kupata mafao hayo, aweze kupata lishe bora, aweze kuishi vizuri, mpaka leo anashindwa kupata malipo hayo. Hili jambo linasikitisha sana kwa sababu tu ya urasimu uliopo pale Hazina. Mimi nadhani ni vyema sasa jukumu hili lisiwe la Wabunge, kwa sababu itafikia mahali wapigakura wanashindwa kutuamini kama tunawasimamia mambo yao.

Baada ya hilo nilikuwa napenda kuzungumzia suala la Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika mjadala huu ambao unaendelea sasa hivi katika kipindi hichi cha Bajeti katika Mkutano huu ambao tunaendelea nao lilijitokeza suala la Katiba katika masuala mawili tofauti na bahati nzuri waliozungumzia wote walikuwa ni Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, mmoja alikuwa na hofu kwamba angeweza kutoa shilingi katika Wizara aliyokuwa anakusudia ili kuikwamisha Bajeti lakini akasema Katiba inamfunga. Mwingine akaizungumzia Katiba hiyo hiyo katika sura nyingine tofauti akasema Wapinzani wanakataa Bajeti lakini wao ndio wa kwanza kwenda dirishani. *(Makofi/Kicheko)*

Lakini Katiba haimlazimishi Mbunge kujiuzulu kwa sababu ya kukataa Bajeti, lakini Katiba inamfunga Mbunge, inamfunga Mbunge katika Ibara ya 90(2)(a)(b)(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inamfunga Mbunge kuweza kufikia maamuzi nadhani kwenye Bajeti ingebaki vile lakini inapofikia Wabunge kukataa Muswada wa Sheria ambayo inawakandamiza wananchi Bunge linaweza kuvunjwa. Hapa inakuja mtazamo wa maslahi kama Mbunge yule aliyekuwa anazungumzia suala la kwenda kwenye dirisha, Wabunge wengi wanatizama maslahi yao na wanasahau kwamba wao wanatakiwa watizame maslahi ya wananchi. Ndiyo pale inapokuja mgongano wa kusema sisi ndio wa kwanza kukimbilia dirishani wakati tunaikataa Bajeti, kwa hiyo, wao wanatanguliza maslahi badala ya kutizama maslahi ya watu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nadhani mjadala wa sasa hivi unaoendeshwa na vyama, hususani vyama vya upinzani kuhusu mabadiliko ya Katiba usiachwe tu, huu ufanywe ni mjadala mpana wa Kitaifa. Serikali kama mdau na yeye itizame tutengeneze Katiba ambayo itakuwa inatoa uwezo pia kwa Wabunge kuweza ama kukubali ama kukataa hasa Miswada ya Serikali ambayo haina manufaa kwa watu. *(Makofi)*

Baada ya kuzungumzia Katiba, sasa nijikite katika hotuba ya Waziri Mkuu na majumuisho ya Waziri wa Fedha. Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika majumuisho yake baada ya mambo mengi aliyokuwa ameyazungumza nataka nijikite katika mambo mawili:-

Kwanza, alizungumzia uzalendo, alikuwa anahoji uzalendo wa waandishi wa habari, sina sababu na wala mimi sipaswi kuwatetea kama ni wazalendo au si wazalendo. Ninachotaka tu kumkumbusha mama yangu Mheshimiwa Zakia Meghji kwamba uzalendo katika nchi hii ulishazika toka siku Azimio la Arusha limezikwa kule Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wazalendo wa nchi hii wamo ndani ya makaburi, wazalendo wale ambao waliacha jozi mbili ya viatu, leo tunashindana kwa kuacha majumba ya ghorofa na mashangingi, uzalendo utatoka wapi? *(Makofi)*

Waziri wa Fedha alipokuwa anahitimisha alizungumzia sana suala *SUMATRA, EWURA* na kama ndio watakuwa wasimamizi katika kudhibiti bei za usafiri na bei za mafuta, *EWURA* iko wapi? Leo kabla ya tarehe 1 Julai, 2007 mafuta yameshapanda bei hapa Dodoma, jana nimenunua dizeli shilingi 1,350 kwa lita, *EWURA* iko wapi? *SUMATRA* iko wapi katika nauli za mabasi, leo usafiri kutoka Dodoma kwenda Tabora shilingi 18,000 *EWURA* yenyewe ina watu saba wako Dar es Salaam, pamoja na sheria ilikuwa inawalazimisha kuwepo na bodi, *EWURA* katika mikoa hazijaundwa, nani atasimamia hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya sana *SUMATRA* imekuwepo lakini Mpanda nauli ya basi kutoka Mpanda kwenda Sumbawanga ilifikia shilingi 40,000/= *SUMATRA* hatukuisikia inasema, *SUMATRA* iko wapi? Ni kwamba tutaendelea kuwadanganya na kuwapa matumaini wananchi kwamba kuna vyombo vitakavyosimamia udhibiti wa bei wakati haviwezi kutimiza wajibu wake. Ni kwa sababu tayari tulishafanya kosa la msingi kabisa la kuvunja Tume ya kusimamia bei kutoka na masharti yaliyokuwepo wakati huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimalizie tu kwa sababu tayari nimeshasikia kengele ya kwanza, nizungumzie hotuba ya Waziri Mkuu ukurusa wa 19 nitaomba nipewe maelezo ya ziada, kumekuwa na matumizi na ubadhirifu mkubwa wa fedha za umma hasa katika Serikali kiasi ambacho kimemfanya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwaita watendaji na kuzungumzia taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake aliyokuwa anaiwasilisha Bungeni hapa katika ukurasa wa 19 kwa ruhusa yako naomba ninukuu alikuwa anazungumzia niende tu haraka haraka kuhusu utengenezaji wa barabara katika Halmashauri zetu kwamba; "ziletengwa shilingi bilioni 25.3 kwa ajili ya kutengeneza kilomita 10,000, lakini mpaka anapotoa taarifa yake Mheshimiwa Waziri Mkuu anasema kwamba zimetumika shilingi bilioni 19.3 kwa kutengeneza kilomita 3,181," maana yake ni kwamba fedha hizo zilizokuwa zimetengwa shilingi bilioni 25 zingeweza kutengeneza kilomita 10,000 kwa maana ya kila kilomita kwa shilingi milioni 2.5 hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zimetumika shilingi bilioni 19 kwa kutengeneza kilomita 3,000 kwa gharama ya karibu shilingi milioni 6, tunataka maelezo kwamba kwa nini gharama ya kutengeneza kilomita imefikia shilingi bilioni 19.3 wakati barabara zingetengenezwa kilomita 10,000 kwa shilingi bilioni 25, gharama zimepanda kwa sababu gani? Kwa nini kumekuwa na tofauti kubwa sana, kiwango cha fedha kilichotumika ni kikubwa ama kumekuwa na wizi ndani yake ama gharama zimeongezeka tunataka tupate maelezo, tofauti hiyo kwa nini imekuwa kubwa kiasi hicho, kutoka shilingi milioni mbili na nusu iliyokuwa imekadiriwa mpaka kufikia karibu shilingi milioni 6 na kidogo milioni sita na elfu sitini na saba kwa kilomita moja hili tulikuwa tunaomba tupate maelezo. *(Makofi)*

Mwisho kabisa ni lile nilikuwa napenda kuitahadharisha Serikali na nchi yetu kwa ujumla tunaangalia suala la huduma kuzifanya kuwa bidhaa. Huduma kwa maana ya elimu, maji na afya, sasa hivi zimegeuzwa kuwa ni bidhaa, zinatizamwa kwa ubora na zinauzwa kama bidhaa. Inapofikia huduma ikawa ni bidhaa kwa mfano elimu watu wanunue kwa hiyo wengine watapata wengine watakosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. CAPT.GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi nipate kusema machache kwa niaba ya wapigakura wa Jimbo la Newala. *(Makofi)*

Kwanza nichukue nafasi hii kumpa pole kaka yangu Luteni Hamisi Chifupa kwa kufiwa na binti yetu, nampa pole yeye na familia yake na wote walioguswa na msiba huu hasa vijana wa Tanzania na akinamama waliomdhamini kuingia katika Bunge hili na Watanzania wote kwa ujumla, tunamuombea Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi na awape ndugu faraja ya kuhimili msiba huu mkubwa. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nichukue nafasi hii kwanza kuipongeza Serikali ya CCM jinsi inavyotekeleza Ilani ya Uchaguzi, juzi ndugu yangu mmoja upande wa Upinzani alikuwa anaongea anasema kwa nini Ilani ya Uchaguzi ya CCM ndio inayotajwa tajwa hapa ndani? Sasa jamani, mimi nilisoma *parliamentary history* mwaka 1965 nikiwa *form two,* tukafundishwa hivi, ndani ya mfumo wa vyama vingi kila chama kinatengeneza *election manifesto,* Ilani ya Uchaguzi. Kila chama kinaiuza Ilani kwa wapigakura chama kilichoshinda, Ilani yake ndiyo inayotekelezwa na mipango ya Serikali lazima ifate Ilani ya Uchaguzi ya Chama kilichoshinda, ndiyo maana

tunataja humu CCM ndio tulioshinda uchaguzi, Ilani yenu hatuwezi kuitaja humu haimo katika mipango ya Serikali. *(Makofi)*

Mimi nilidhani hili ni jambo *clear,* lakini kwa sababu binadamu sisi tunakumbushana, ndio maana tunakwenda Msikitini kila Ijumaa na Kanisani kila jumapili kukumbushwa, nilikuwa namkumbusha *learned brother* mwenzangu huko aliko kwamba ndio utaratibu katika *multipartism. (Makofi)*

Lakini ndugu yangu mmoja ameongea leo anasema CCM tulizika Azimio la Arusha, Azimio la Arusha halikuzikwa, katika *politics* unaenda na wakati kilichofanyika Zanzibar ni kurekebisha Azimio la Arusha kulingana na wakati tulionao. Zamani palikuwa na watu, *Warsaw pact,* kulikuwa na watu wa *NATO Eastern Broke* na *Western Broke,* baada ya vita baridi kumalizika, tulivyoiona inaisha, tulivyoona nguvu zile za *Eastern Broke* zinapungua, tukasema tunaishije ujamaa katika mazingira ya sasa, tukarekebisha.

Azimio la Arusha linatekelezwa mpaka leo, dunia nzima nchi gani unamsomesha mtoto kwa shilingi 20,000/= kwa mwaka, Azimio la Arusha, akinamama wanatibiwa bure wale wanaohusika mambo ya kujifungua, utekelezaji wa Azimio la Arusha, watoto wanasoma bure shule ya msingi, utekelezaji wa Azimio la Arusha. *(Makofi)*

Sasa muda wenyewe basi nilidhani kwa makomredi, kwa ndugu zetu wa Upinzani niweke sawa haya mambo mawili maana mambo kama haya hayakujibiwa, watu wanaweza wakadhani ni kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nilisema napongeza sana utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi, kwangu kule Jimbo la Newala, mambo mazuri kabisa. Lakini yale ambayo si mazuri nitayasema, mazuri ni Ilani ya Uchaguzi inataka *secondary school* kila kata mwaka 2010. Newala tuna kata 21 tumeshajenga *secondary school* 25 katika mwaka mmoja na nusu wa Serikali hii tumevuka malengo, Newala tunashida ya maji, mwaka jana Rais katupa shilingi milioni 800 kutengeneza miundombinu ya maji. Newala Halmashauri yetu ya Wilaya mambo yanakwenda vizuri tumepata hati safi, mwaka huu tumepata tena, tukapigwa shilingi milioni 500. Kwa sababu umepata hati safi chukueni shilingi milioni 500 fanyeni shughuli ya maendeleo na mimi na Madiwani wenzangu kule tuko macho kulinda hati safi. *Celtel* wanaongea sasa Kitangari, wanaongea Chilangala, Chuo cha Ukunga kile sasa hivi kimepandishwa hadhi, wanachukua *diploma,* siku hizi *diploma* umesoma ya wapi, Newala, jamani hakujakucha tu kumekucha. Tulikuwa tunashida ya umeme, *Mnazi Bay* sasa umeme pale Mtwara hauna mgao, wale mnaosema kwamba Serikali haijafanya kitu, njoo mtembelee kule, ila nilisema kwamba nieleze haya mafanikio tumeanza vizuri. Wale ambao mnadhani hatujaanza, basi subirini sisi tunakwenda sisi tunakwenda safari yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya kusema hayo nataka niwapongeze sana wapigakura wangu wa Jimbo la Newala, jinsi walivyoitika habari ya kujenga sekondari, tumeambizana sisi kwetu Newala, *priority number one* ukitaka uendelee *priority number* ni elimu, namba mbili ni elimu namba tatu ni elimu maana ukitaka wahandisi wa maji ni lazima wasome, ukitaka biashara si ni lazima wasome, ukitaka mashehe na mapadri si ni

lazima wasome, kwa hivyo nawapongeza sana, msimamo ndio huo na tutaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, nataka nichangie habari ya ulinzi na usalama, sisi Watanzania tumezoea kusema nchi yetu shwari, mimi nakubali, nchi yetu shwari kwa sababu hakuna watu wanaopigana na mishale, hakuna watu wanaopigana kwa bunduki. Lakini nchi yetu sio shwari barabarani nchi yetu sio shwari kutokana na ajali za barabarani, mjumbe mwenzangu mmoja wa Kamati ya Ulinzi na Usalama amejibiwa wiki mbili zilizopita kwamba ajali za barabarani mwaka 2005/2006 zilikuwa 33,977 watu 5,312 wamepoteza maisha, majeruhi 32,052.

Mimi kama mjumbe wa Kamati hiyo na Makamu Mwenyekiti, hali hii si shwari, Serikali lazima ichukue hatua, ajali zinasababishwa na mwendo wa kasi, wanapangiwa ratiba ya kuondoka Dar es Salaam, kila baada ya nusu saa, kwenda Mbeya – Dar es Salaam, kwenda Arusha lakini wale walioachana kuondoka muda wa nusu saa, wote wanafika Arusha na Mbeya muda mmoja, kwa nini hawana *time table? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mimi nasoma, mabasi yalienda kwa mfano yanakwenda *Itungi Port,* yanakwenda Arusha kuna *time table,* utaondoka Dar es Salaam saa fulani unatakiwa Moshi saa fulani, Chalinze saa fulani, ukifika kabla ya muda ule unapigwa faini wewe kwamba umekwenda mwendo wa kasi. Hivi kwa nini hatuziwekei ratiba magari haya, ili kama wameachana kuondoka Dar es Salaam kwa muda wa saa mbili, wafike Moshi saa mbili hiyo, nchi yetu shwari katika mambo mengine barabarani si shwari Watanzania wanakufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu daladala, Serikali lazima ichukue hatua ya kudhibiti daladala hasa Dar es Salaam. Sasa hivi Dar es Salaam maana ya kuwa na vituo vya mabasi haipo tena ajali nyingi za daladala Dar es Salaam zinatokea kwa sababu wanaokota abiria mahala popote wanapomkuta. Kwa hiyo, vituo vya mabasi havitumiki na ajali nyingi Dar es Salaam zinasababishwa na daladala, mimi naomba Serikali hili ilione lilifanyie kazi ili nchi yetu iwe shwari, sio tu katika mambo ya kupigana, bali pia lifanyiwe barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka nizungumzie tatizo la maji tena Newala nilieleza mwaka jana Newala, Tandahimba tuko katika *Makonde plateau what is a plateau arised flat peace of land,* tuko juu, hatuna visima vifupi, tunashukuru kama nilivyosema tumepewa shilingi milioni 800 mwaka jana tunaomba kazi ya ukarabati mitambo ile ifanyike haraka, tunaomba pia upande wa maji kule Newala mradi wa maji wa Mbwinji na Luchemo ilichukuliwa na mafuriko mwaka 1990 hakuna *replacement,* tunaomba Serikali ichukue hatua. Mradi wa maji Chiwambo ulijengwa na *CCT* ukakabidhiwa Serikali, unatumia dizeli tunaomba umeme, mitambo yake imechoka tunaomba ifanyiwe *complete overhaul* ili watu wa maeneo yale wapate kwa uhakika. *(Makofi)*

Lakini kubwa kabisa katika maji, tatizo la maji Newala sasa ni kubwa kabisa kwa sababu hatuna umeme, ili tupate maji ya kutosha Newala lazima maji yawe *pumped* Mkunya *10 hours consectively.* Sasa hivi tunapata mgao wa umeme kwa muda wa saa

nne, na wakati mwingine tunaletewa usiku, naiomba sana Serikali iharakishe kuunganisha umeme ule wa *Mnazi Bay* kati ya Nyangao na Ndanda kwa sababu ukishaunganisha Nyangao na Ndanda, umeme utafika Tandahimba, utafika Newala, utafika Kitangali, utafika Nachingwea utafika kila mahali, tatizo la maji litapungua.

Naomba sana Serikali ya CCM mtusaidie katika hili, Ilani ya Uchaguzi inasema mwaka 2010 upatikanaji wa maji vijijini iwe imefika asilimia 65, Newala, Tandahimba, upatikanaji wa maji asilimia 22 tu maana yake ni kwamba Serikali ya CCM lazima ichukue hatua za madhubuti kama majimbo mengine kupeleka maji mnatembea, jimbo la Newala, Tandahimba, lazima Serikali ikimbie ili tuwakute wenzetu na sisi tupate maji ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nihamie sasa kwenye korosho, kwanza kuishukuru Serikali imetufutia madeni *union* yetu ya *TANECU* na *MAMCU,* tunaiomba Serikali itekeleze ahadi yake ya kusaidia *union* zetu kununua korosho msimu huu. Korosho inayozalishwa Tanzania ni tani 60,000, viwanda vyetu vina uwezo wa kubangua korosho yote bila kupelekwa nje, tatizo wenye viwanda hawana fedha za kununua korosho kutoka kwa wakulima. Sasa kama kuna hiyo *guarantee export* mnayoisema, hivi mbona hamuwapi hao wenye viwanda vya korosho wanunue korosho zote kwa wakulima, wabangue zote hapa hapa ili tuwe na *added value* katika zao la korosho watu watapata ajira juzi tumempeleka Makamu wa Rais kiwanda kimoja pale Mtwara, akinamama 400 wakibangua korosho, wako kazini. Mipango mizuri ya CCM kwa wale ndugu zangu nawakumbusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine kwenye korosho tumepitisha sheria ya mgao wa *export levyl* asilimia 65 inakwenda katika Wilaya ambako korosho imenunuliwa, asilimia 35 ni ya *central government,* tumepitisha kwa mujibu wa sheria. Jambo linalosikitisha kwamba tangu sheria imeanza utekelezaji Serikali haijalipa hizi fedha kwa Halmashauri zinazohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiuliza unaambiwa Serikali imekuagizieni mbolea tulikuambieni hatuna uwezo wa kuagiza wenyewe mbolea, mimi naomba sana katika hili namuona Waziri Mkuu anacheka, ana *smile* amenielewa vizuri, pengine mwaka huu tupewe pesa zile za *export levy,* kila Halmashauri ipewe fedha zake.

Lakini lingine kwenye korosho, ni pembejeo Wizara ya Kilimo, Chakula na ushirika, ili tufanyisha semina namna gani wanatoa ruzuku kwenye mahindi, kwenye korosho tukaambiwa mpango unaandaliwa na semina mtafanyiwa mpaka leo hakuna semina tuliyofanyiwa hata mimi wapigakura wangu wakiuliza taratibu zikoje za ruzuku katika dawa za korosho sina jibu. Kwa hiyo, naomba hili la *export levy* tupewe wenyewe lakini pia kwenye pembejeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu inahusikana na maendeleo ya miji, nataka kusema mambo mawili kwenye maendeleo ya miji:-

La kwanza, miji yetu mingi sana sasa hatufuati *master plan,* mimi nilipokuwa mdogo ikiwa kuna maghorofa yamejengwa mahali lazima kuna *open space* watoto wanacheza cha ndimu, sasa hivi hakuna maeneo ya kucheza watoto, tumegawa viwanja vyote watoto wetu wanacheza wapi wanaokaa kwenye maghorofa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine, nataka nitoe mfano katika miji ambayo Waingereza wali-*plan* kabla ya kujenga ni Mtwara na Tanga. Ukitoka uwanja wa ndege wa Mtwara mpaka pale Kanisa la Wakatoliki *master plan* wanasema barabara ile *Tanu Road* ghorofa tupu.

Nenda leo Mtwara Mheshimiwa Waziri Mkuu vurugu tupu, *petrol station,* vibanda na kadhalika mnatuharibia mji wetu, wale mnaotoa vibali kinyume na *master plan,* tunataka Manispaa ya Mtwara iwe Jiji, tunataka kesho kutwa iwe Jiji. Sisi ni Wabunge wa *standards and speed*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanavamia *publicly,* hatuna maeneo ya kujenga Makanisa, Misikiti, viwanja vya kucheza watoto na kadhalika. *(Makofi)*

(*Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA:** Aha! Ya pili? Bado moja.
Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na ahsante sana yale mengine yaliyobaki nitayaandika. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kepteni George Mkuchika, sasa mwita Mheshimiwa Halima Omar Kimbau.

**MHE. HALIMA O. KIMBAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja hii iliyo mbele yetu, hoja ya Waziri Mkuu ambayo ameitoa vizuri sana na nina hakika tumeielewa sana na kwa maana hiyo sina sababu yoyote ya kusita kuiunga mkono mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea na mchango wangu napenda kwa masikito makubwa kabisa kuwapa pole wazazi wa mtoto wetu, mpenzi wetu, mwanamke kijana jasiri Mheshimiwa Amina Chifupa, kwa kutoweka duniani, kweli bado tulikuwa tunamuhitaji, lakini tunasema Mwenyezi Mungu ana uwezo zaidi kati yetu sisi tulimpenda lakini Mungu amempenda zaidi. Mwenyezi Mungu iweke Roho ya Marehemu mahali pema peponi na wale wote ambao tupo kwenye msiba huo Mungu atupe subira, *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine napenda kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kufanya ziara za mara kwa mara katika Mikoa yetu, nawapongeza sana kwani mimi naamini kuwa kuona ni bora kuliko kusikia maana hapa tunaongea wanasikia lakini wanapokuja kwenye Mikoa na Wilaya zetu wanaona. Kwa hiyo, naamini kule kote ambako walikwenda wakaona walichukua hatua za haraka kuliko kule ambako hawajaenda. Kwa hiyo, natoa wito kwamba waendelee

kufanya hivyo ili wafike kule kote ambako wameombwa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kushirikiana nao katika kuondoa matatizo ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Lakini kutokana na hilo la ziara mimi napenda kumpongeza Waziri Mkuu kwa jambo la peke yake. Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja Mafia, kauli aliyoitoa ilinipa faraja. Alisema kwamba siku zote huko nyuma akisikia habari ya Gati hata wakati Kanali Kimbau alipokuwa Mbunge alikuwa hamuelewi akizuia shilingi, hiyo ni miaka ya nyuma. Lakini baada ya kuja Mafia anasema sasa anamuelewa, sasa hii kauli mimi imenipa faraja kwamba nilikuwa shahidi wakati tukiongea habari ya Gati kipindi hadi kipindi na inawezekana kweli Waziri Mkuu alikuwa hatuelewi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo tu Kanali Kimbau lakini hata Mheshimiwa Mbunge Buji, mimi ambaye ni mwenzao nimeishi Mafia zaidi ya miaka 30. Sasa nashukuru kwa kauli hiyo nina imani kabisa na Waziri Mkuu kwamba sasa Gati litajengwa Mafia. Nakushukuru sana Waziri Mkuu kwa kauli hiyo na ni mategemeo yangu kwamba watu wa Mafia sasa watapata Gati. *(Makofi)*

Lakini siyo tu kwa kauli yake hata kwa ahadi ya Rais Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwamba katika ahadi alizozitoa katika Mafia mojawapo ni Gati na la pili ni Kiwanja cha Ndege. Sasa hapo napata pia imani kwamba Gati itajengwa kwa sababu Kiwanja cha Ndege sasa hivi kinajengwa kwa hiyo, nasema kwamba viongozi wa Chama cha Mapinduzi na Ilani ya Chama cha Mapinduzi haiongopi kabisa kwani hawa wote ni viongozi sahihi wa Chama cha Mapinduzi na wanatekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Nawapongeza sana tena sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niende kwenye Halmashauri zetu yaani TAMISEMI. Nashukuru wenzangu wamechangia kwa kirefu juu ya Halmashauri zetu lakini nawapongeza Halmashauri zote ambazo zinapata Hati Safi sasa hivi na hatimaye kuwawezesha wananchi wetu kupata ruzuku ya maendeleo na nina hakika hizi chache zilizobaki nao pia watapata Hati Safi kipindi si kirefu na hatimaye wote tupate ruzuku za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nina jambo moja, sasa hivi tumeanza kufanya huu utaratibu wa tathmini yaani *value for money* kutathmini hela za maendeleo zinavyotumika. Wengi wenzangu wameongea kwamba hazitumiwi vizuri kwa baadhi ya Halmashauri za Wilaya ni kweli hilo linafanyika kwamba utakuta fedha zinatolewa kwa madhumuni mazuri baadaye matokeo yake yanakuwa si mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi nina lingine la ziada ambalo linanipa taabu kuona kwamba tunafanya nini kwa kusaidiana na Ofisi ya Waziri Mkuu na TAMISEMI. Mbali ya kutotumia vizuri fedha kwa baadhi ya Halmashauri lakini pia kuna tabia moja ambayo inajengeka kwenye Halmashauri zetu kusema uongo, baadhi ya Halmadhauri wanaongopa, wanasema uongo. Sisi Bunge tuna sheria na taratibu kwamba Mbunge akisema uongo kuna adhabu inayotolewa, sasa je, hawa watendaji ambao wanadanganya Kamati za Bunge ambazo zinakaa kupitia mahesabu yao wakiangalia kwenye taarifa zao utakuta wameandika nyumba za walimu zimekamilika, zahanati

imekamilika, barabara imekamilika, lakini wakati Kamati hizi zikienda kwenye ziara kuona hivyo vilivyokamilika, inasikitisha. Ni uongo ulio dhahiri unaosemwa na watendaji hawa, unakwenda unakuta nyumba ya mwalimu haina dari, choo na badala ya vyumba vitatu inakuwa na vyumba viwili lakini mtendaji kwenye mahesabu na taarifa zake amesema kwamba nyumba ya mwalimu imekamilika.

Mheshimiwa Spika, unaambiwa barabara imetiwa changarawe unakwenda unaona mambo ya ajabu, mifereji imekamilika ukienda unakuta mifereji hakuna au ni michafu, matokeo yake mimi nilisikitika sana na nashukuru leo Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe wapo hapa ndani kwamba tulifika kwenye majumuisho baada ya ziara ya Mkoa wa Tanga, anasimama kiongozi, samahani. Anasema anaomba radhi kwa niaba ya wenzake kwa kuvunja amri ya nane mimi nikajiuliza amri ya nane ni ipi? Nikafuatilia kujua kwamba amri ya nane ni ya kusema uongo, yaani wanasikitika na wanakiri kwamba wamesema uongo. Lakini wanaomba radhi kwa kuwa wameungama, sasa mimi nasema hii haitoshi, na ninasema haitoshi kwa sababu huu Mkoa mmoja uliomba radhi na ukaungama na nina hakika kwa kauli zao hawatarudia kuongopa je, hizi Halmashauri nyingine ambazo zinaendelea kuongopa tunazifanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naomba wasifanye mambo hayo na naomba Wizara kupitia kwako Mheshimiwa Waziri Mkuu waone kwamba wale viongozi wenzetu ambao wanaongopea Kamati za Bunge basi wachukuliwe hatua zinazofaa. Nawapongeza sana Wizara sasa hivi wamejitahidi kuwaajiri watu wenye ujuzi na nina hakika basi wataendelea kuwaajiri na kuweka watu wa kweli na wenye uchungu wa maendeleo ya nchi hii, nashukuru sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kupitia huko huko kwenye Halmashauri zetu, sisi Waheshimiwa Wabunge nashukuru kupitia Wizara na kupitia Bunge lako Tukufu tunawezeshwa kutembelea miradi. Lakini baadhi ya Halmashauri Madiwani hawatembelei miradi, ukiuliza utasikia hela hawana, sasa mimi ningeomba sana zile mbinu ambazo Wizara imetumia kutuwezesha kufanya ziara kwenda kuona miradi basi waone na Halmashauri nazo wawawezeshe Madiwani kutembelea miradi yao ndani ya Halmashauri zao. Nina hakika wakifanya hivyo hata haya mambo ya kusema uongo yatapungua, mambo ya ubadhilifu yatapungua lakini leo Diwani anakaa miaka miwili hajatembelea mradi.

Kwa hiyo, hayo yanachangia pia kuona kwamba na wenyewe watendaji wanaweza kufanya wanavyotaka na kuwadanganya kama wanaweza kutudanganya sisi kwa nini wasiwadanganye Madiwani? Kwa hiyo, naomba hili liangaliwe kwamba wenzetu wawezeshwe na wao kwenda kutembelea miradi ambayo ipo ndani ya Halmashauri zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia katika kuwawezesha Madiwani naishukuru Serikali ya CCM imeweza kutukopesha magari sisi Wabunge na ninashukuru sasa hivi kwenye hotuba hii imeonyesha kwamba wataongezewa posho Madiwani wetu ambao wako huko kwenye Halmashauri zetu. Lakini mimi nasema hii posho ni ndogo waongezwe kiasi kidogo ifikie angalau shilingi 150,000/= lakini pia wawezeshwe

kukopeshwa vyombo vya usafiri kama siyo gari basi hata *Bajaj,* sisi tumekopeshwa magari kwa ajili ya kufanyia kazi na tumewezeshwa kuweza kufanya ziara zetu kama Wabunge katika maeneo yetu, sasa hawa wenzetu watakwendaje kwenye maeneo yao? Acha hizi ziara ambazo zinapangwa na Halmashauuri lakini hata ziara ambazo yeye kama Diwani anataka kwenda kuangalia mazingira ya Kata yake. Kwa hiyo, naomba Waziri Mkuu kupitia Wizara hiyo basi ione jinsi gani wataandaa utaratibu wa kuwakopesha vyombo vya usafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba kuendelea kuishukuru Serikali yetu kwa kutujengea kiwanja pale tunapoishi, mimi ninaongelea Mafia zaidi kwa sababu ndiyo ninapoishi kwa kutujengea kiwanja cha ndege na Waziri Mkuu hatasahau kufuatilia masuala ya Gati. Lakini pia tunamkumbusha Mheshimiwa Waziri Mkuu tena kwamba tuliomba ile jenereta ikitoka Mtwara ya umeme basi iletwe Mafia kwa sababu pale sasa hivi tuna mgao wa umeme jamani kila kitu tu tunagawana jamani, hata umeme Mafia ni tatizo kwa hiyo, nawaomba sana wakumbuke hilo lakini pia kutupatia Hakimu wa Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi juzi nimejaribu kufuatilia Mafia kuna wiki ya tatu watu wanaitwa Mahakamani kwenda kusikiliza kesi za Wilaya lakini Hakimu hajafika, kwa hiyo, watu wanabaki na matatizo yao kwa muda mrefu. Kwa hiyo, naomba sana tena sana Mafia ni Wilaya kama Wilaya nyingine lakini pia ina taabu zaidi kwa sababu ni Kisiwa, kwa hiyo ni matatizo ya usafiri lakini pia ni matatizo ya huduma. Kwa hiyo, tungeomba kupitia kwako Waziri Mkuu tupatiwe Hakimu wa Wilaya katika Wilaya ya Mafia kama ambavyo tumekuomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nashukuru Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kutupa shilingi milioni 14 kwa mara ya kwanza hifadhi zianze kwa ajili ya maendeleo ya Wilaya yetu. Hivyo nategemea kwamba huu ni mwanzo mzuri na nina hakika kuna nyingi tu za nyuma ambazo tunawadai hawajatupa lakini basi waone kwamba kila mwaka sasa hivi wanatenga fungu kutoka hifadhi kwa ajili ya Maendeleo ya Halmashauri yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nasema kwenye suala la mikopo siyo hii ya JK, ni ile ya nyuma ambayo Halmashauri zinatakiwa kuchangia *percent* fulani mpaka leo kila siku kuna madeni, madeni pande zote mbili. Kuna madeni Halmashauri hazijachangia mfuko lakini kuna madeni akinamama na vijana waliokopeshwa hawajalipa kwenye mfuko, sasa hili suala linachosha kila siku mnaliongelea sasa ifike mahali tuone tunafanya nini ili tufikie mwisho Mheshimiwa Waziri Mkuu. Si vizuri kuona kila siku tunaongelea madeni ambayo hayalipikia au madeni ambayo hayana uwezo wa kuweza kuwekwa sawa. Hawa akinamama wengine sasa hivi hawapo, vijana wengine miradi yenyewe ilishasambaratika na si makusudi lakini ni kwa sababu walikuwa hawana elimu ya biashara au elimu ya miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiit, lakini Halmashauri nyingine zimeshindwa, zinafika mahali wanakwambia wanapenda lakini hawana uwezo wa kuchangia lakini bado inaonekana tu kwenye vitabu, sasa tuandae utaratibu wa kuona kwamba haya madeni

kwa pande zote mbili yaani kwa akinamama na vijana waliokopeshwa basi yafikie mwisho lakini na kwa Halmashauri ambazo bado zinadaiwa kuchangia mifuko hii ifikie mwisho ili na sisi tuende kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo narudia kuwashukuru na kuwatakia kila la kheri na ninamtakia Rais wa Jamhuriya Muungano wa Tanzania apate raha zaidi katika mafanikio ya *Taifa Stars*, kwa sababu anataka raha basi naamini Mungu ampe raha, raha tu siyo ya michezo na raha ya maendeleo na maisha yake na raha ya yeye na familia yake *Inshallah* Mungu ampe yote anayoyata kwa nia njema pamoja na sisi tukimsaidia pia Mungu atupe raha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa mara nyingine tena ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Halima Kimbau, sasa mwita Mheshimiwa Yono Kevela na Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, ajiandae.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kwanza kuishukuru sana hii hotuba ya Waziri Mkuu aliyoitoa kwa kweli ina mwelekeo mzuri na ina dira na ndiyo Ilani ya Chama cha Mapinduzi tuliyokuwa tunaitegemea. Nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwapongeze sana wenzetu wa Upinzani walikuwa wanajitahidi kutoa hoja zao lakini yote walikuwa wanam-*support* Waziri Mkuu, kwa hiyo, tunawashukuru sana kwa kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nikupongeze wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi na Sekretarieti yote ya Bunge kwa kweli tunaipongeza kwa jinsi mnavyofanya kazi vizuri kwa umakini, tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa niaba ya wananchi wa Njombe Magharibi nichukue nafasi hii kuwapa pole sana ndugu zangu ukoo wa akina Chifupa na ukoo wa akina Mbanga kwa msiba mkubwa uliotupata kwa dada yetu Amina Chifupa, poleni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili nisisahau nianze kwa kuunga mkono hoja hotuba ya Waziri Mkuu kwa kweli mimi sina wasiwasi, naiunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kupongeza vile vile nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kunikumbuka. Zile barabara ambazo zilikuwa ni kero kwa muda mrefu yaani barabara za Ilembula - Kanamalenga - Usuka zinalimwa na zinatengenezwa vizuri sana. Vile vile nichukue nafasi hii kupongeza barabara ambazo zinalimwa sasa hivi kule Soliwaya - Lyamluki kule Kijombe Kata ya Wanging’ombe kwa kweli Serikali ya Chama cha Mapinduzi inafanya kazi nzuri sana. Halafu vile vile kuna barabara nyingine zinalimwa sasa hivi hizo ni barabara za Lusisi, Igima, Mlevela na Mhaji pia kwa kweli inanipa faraja kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunalalamika kwa kupindi kirefu sana kuhusu suala la umeme, umeme sasa hivi wa gridi umeshapelekwa kule Kidugala. Pale sekondari walikuwa wananilalamikia kwamba umeme utakwenda lini, sasa hivi umeme wa gridi umeshapelekwa Kidugala na siyo hapo tu tulikuwa na tatizo la umeme pale Wanging'ombe, Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kweli imepeleka umeme na *transformer* ipo kubwa tu kijiji cha Wanging'ombe sasa tunafikiria na Utiga watapata kwa sababu kuna *TAZARA* pale Wanging'ombe upelekwe umeme wa uhakika. Kwa kweli, naipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisisahau kuzungumza habari ya barabara ya *TANROAD* ile ya Iyai kwenda Luduga - Mandegu nayo imelimwa vizuri. Lakini pamoja na pongezi hizo nina ombi kuhusu suala la barabara zile za Saja, barabara za Kata ya Saja inasahaulika sana toka enzi za ukoloni barabara hazipitiki. Kuna vijiji kama Ikwilimambo hawajui barabara nzuri, Idenyimembe, Isimike, Itengele, Uhenga, Igenge, Igomba na Saja yenyewe ni tatizo kubwa kwani barabara hazipitiki, tunaiomba Serikali iangalie kwa jicho la huruma wale watu wapate barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba nataka nizungumze kuhusu suala la kilimo. Unaposema Mkoa wa Iringa au Wilaya ya Njombe moja kwa moja huwezi ukakwepa kuhusu suala la kilimo yaani mbolea, mbolea ya ruzuku ni tatizo pamoja na kwamba Serikali inajitahidi lakini ile mbolea kutokana na mahitaji yetu kwa sababu tuko kwenye *big four* haitoshelezi. Wapiga kura wangu wamenituma kwamba kule Njombe Magharibi hasa Wilaya ya Njombe tuna tatizo la mbolea, mbolea inafika kwa kuchelewa inapofika mwezi wa Desemba na Januari haiwasaidii, wakulima wanaomba ifike mwezi wa Agosti kwa sababu kuna kilimo cha mahindi na viazi, ikifika mwezi wa Agosti ndiyo wanasema mbolea inakuwa muafaka na iende mbolea inayotakiwa ile ya kupandia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo tumezungumza sana naona kama nitakuwa narudia rudia nalo ni suala la vipimo, hasa vipimo vya lumbesa watu wanateseka sana na lumbesa na hii inawatesa wakulima wa Njombe Magharibi na Mkoa mzima wa Iringa wanateseka sana na wengine wanaweza wasielewe lumbesa ni nini. Ni vile vipimo vya magunia ambayo yanakuwa yana kitambi, kitambi kinakuwa kikubwa watu wananyonywa na wafanyabiashara kwa hiyo, ipelekwe mizani na kuwe na usimamizi mzuri, wenzetu askari wajitajidi kadri ya uwezo wao wahakikishe kwamba hiyo lumbesa inakomeshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri tumepata Mkuu mpya wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya wako makini sana kwa kweli wanachapa kazi vizuri wakisaidiana na Mkurugenzi. Kwa hiyo, kwa kweli hali ni nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalotaka kuzungumzia ni katika upande wa kilimo nalo ni suala la mazao. Mahindi kule yako mengi sana hayauziki kwani bei ni kidogo sana. Wamenituma na kuna meseji zinakuja nimekwenda pale Lusisi nimepanda Lwilanzi wananiuliza mahindi yako mengi tunashindwa kwa kuuza, soko la mahindi

limeshuka tunaomba Serikali iangalie uwezekano wa kuweka soko la uhakika kweli pale Makambako kuna sehemu ya kuuzia mahindi lakini mwaka huu sehemu kubwa walikuwa wanakimbilia Ludewa na siyo Njombe.

Kwa hiyo, tumepata shida watu wana mahindi, wanashindwa kusomesha watoto kwani mahindi yanauzwa kwa bei ya juu lakini mahindi yanauzwa kwa bei ya chini sana. Kwa hiyo, tunaomba Serikali muangalie upande wa Njombe hali siyo nzuri tunaomba mazao yauzike tupate soko la uhakika na mipaka ifunguliwe ya nchi za nje watu wapate kuuza mazao kwa bei nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalotaka nizungumzie ni kuhusu zao la alizeti, hili zao la alizeti ni zao la biashara na ni zao la muhimu sana. Zao hili linatoa mafuta ya kupikia tena hayana madhara yoyote ukilinganisha na mafuta mengine, sasa zao la alizeti kila nikisoma hotuba ya Waziri Mkuu sioni zao la alizeti kama linazungumzwa popote. Hata katika mipango ya Wilaya na Mikoa tunaona hili zao la alizeti linasahaulika, ukisema Njombe ina maana unazungumza alizeti, alizeti ni zao muhimu kama korosho lakini watu wamelisahau hawaliundii bodi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba Serikali kwa kweli iangalie kuhusu zao la alizeti ni zao la muhimu na kama tukifanya kazi vizuri tukaliweka katika mazingira mazuri hili zao la alizeti linaweza likawa mkombozi mkubwa sana katika Wilaya ya Njombe, Mkoa mzima na sehemu nyingine zinazolima alizeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alizeti hii inaitwa *Sunflower* sasa kwa nini hatuiundii bodi? Hatulifanyii mikakati. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali iangalie kwa jicho la makini hili zao tusilipuuzwe ni zao muhimu sana, linaweza likatukwamua katika uchumi. Watu wakopeshwe mitaji, walime mashamba makubwa ya alizeti na ikiwezekana kijengwe kiwanda kikubwa cha alizeti.

Kwanza mimi nichukue nafasi ya pekee kumpongeza Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya, watu wanampigia kelele wanasema amekopa hela nyingi, sasa mnataka akope mtu mweupe? Mwenzetu anapokopa mweusi tunamlalamikia, mizengwe mingi, mnataka mtu mweupe? Amejenga kiwanda kikubwa sana kule Rukwa, vijana wetu wamepata ajira, wananchi wameondokana na umaskini, Rukwa ilikuwa pembezoni lakini watu mnamlalamikia, mimi sielewi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, au mlitaka akope shilingi mbili au tatu? Sasa kupata shilingi bilioni sita tu mnamlalamikia je, wanaojenga majengo kule Canada mbona hamuwalalamikii? Tena wanachukua uchumi humu humu. Kwa hiyo, mimi kwa kweli nampongeza sana Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya kwa ujasiriamali na wengine tuige mfano kwake na twende kujifunza kwake na nachukua nafasi hii huenda pengine na mimi nikakopa shilingi bilioni 10 nijenge kiwanda cha alizeti, sasa mkisikia ni Yono mnaanza kupiga kelele tena. Kwa hiyo, kwa kweli hapo naipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuangalia ujasiriamali kwa Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, tunachotakiwa ni kumuunga mkono siyo kumpiga vita. *(Makofi)*

Pia nataka nizungumzie kuhusu suala la mradi wa maji. Mimi nichukue nafasi hii kupongeza Shirika la Italia linaitwa *Akra,* hili Shirika ni la Serikali ya Italia, limetuletea maji ikishirikiana na Serikali ya Chama cha Mapinduzi, mradi ni mkubwa sana unaitwa mradi wa Towe Mwiramba una thamani ya shilingi bilioni 3.5 siyo milioni ni shilingi bilioni 3.5. Kuna vijiji 14 vimefaidika na huu mradi sasa watu wakisema kwamba Ilani ya Chama cha Mapinduzi haitekelezwi, mimi siwaelewi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na tatizo la maji lakini Serikali imetuletea maji kwa kusaidiana na wafadhili na nichukue nafasi hii kumpongeza sana *Father* Kamilo naye amekuwa mstari wa mbele na bega kwa bega akishirikiana na Serikali katika kuleta huu mradi wa shilingi bilioni 3.5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji ambavyo vimefaidika nitavitaja kwa haraka haraka, vijiji hivyo ni Usalule, Igagala, Ulembwe, Nyumbanyitu, Mlevela, Igima, Mhaji, Lusisi, Lulanzi na Mtwango kwenye kijiji cha kaka yangu Mheshimiwa Jackson Makwetta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisije nikawa nimekosa fadhila, kuna Shirika lingine la wenzetu wa Kibena yaani *Kibena Tea Factory* nao wanatusaidia sana katika Jimbo la Njombe Magharibi na hususan Wilaya ya Njombe na Mkoa wa Iringa, wanatusaidia sana kwenye nyanja za kijamii hasa kwenye elimu, maji na shughuli mbalimbali. Kwa kweli, hawa *KTF* wanahitaji pongezi kubwa sana na Serikali iangalie uwezekano hata wa kuwasaidia kupunguza kodi kwa sababu wanaisaidia sana Serikali kwenye utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la afya. Kwa kweli siyo siri mambo yamekuwa ni mzuri sana na ninaipongeza Serikali kwa huu mpango wa kuanzisha Zahanati katika kila kijiji na kuanzisha kwenye kila kata vituo vya afya. Sasa pamoja na hizo pongezi nilikuwa naishauri sana Serikali ianzishe mikakati ya kufufua vyuo vya uuguzi yaani vya Ukunga na vya Waganga Wasaidizi, vyuo hivi vipo siyo kwamba havipo ni suala la kuvifufua tu. Nikizungumzia uuguzi hata kwenye hospitali za misheni vipo vyuo, tuviimarishe, tusaidiane na Serikali pale Ilembula kuna vyuo vizuri vinatoa *diploma* na hata *certificate,* lakini vikakosa wanafunzi kwa hiyo, tusaidie kuvifufua na kuimarisha vile vyuo vilivyopo ili Zahanati hizi tunazojenga katika kila kijiji kusiwe na matatizo ya wakunga, manesi na hata watumishi wengine. Kwa hiyo, hapo naipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitazungumzia suala la dawa ya kulevya. Hizi dawa za kulevya kwa kweli hawa watumiaji na wauzaji tunawalea tu yaani kama tukiwa *serious* tatizo la dawa za kulevya siyo tatizo kwa kweli, mimi naweza nikajitolewa kwamba katika miezi mitatu ya kwanza tunaweza tukawakomesha kabisa kusiwe na dawa za kulevya. *(Makofi)*

Mimi kwa jina naitwa Yono siyo kwamba pengine ni jina ambalo ni geni, kama tukiamua kuwavalia njuga nadhani katika kipindi cha miezi mitatu ya kwanza watapata joto ya jiwe. Kweli Marehemu Mheshimiwa Amina Chifupa alikuwa anapiga kelele sana kuhusu dawa za kulevya lakini mimi sina uwezo wa kuzungumza sana kama mwenzangu,

lakini nina uwezo wa kutekeleza na tukakomesha kabisa hii biashara ya dawa za kulevya kwa sababu tunawafahamu ila sasa tunalindana na kuoneana aibu na hii ni nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona muda umekwisha naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yono Kevela, nakushukuru sana. Baada ya Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, atafuatia Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro na Mheshimiwa Suleiman Kumchanya, ajiandae.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

Kwanza kabisa kwa niaba ya vijana wenzangu na mimi mwenyewe natoa pole kwa familia ya Mheshimiwa Amina Chifupa, nitamkumbuka sana kila siku asubuhi tulizoea kuamkiana na tulikuwa tunaitana dogo, dogo kila tulipoonana; na tulikuwa na zamu ya kuamkiana kila tunapoonana asubuhi. Kwa kweli nitamkumbuka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia naomba kwanza nimshukuru Mungu kwamba niko upande huu wa Upinzani na ninaweza nikachangia mawazo yangu kwa huru kabisa bila kuingiliwa na mtu yeyote. Nakumbuka kabisa wakati tunaapa tulisema tutailinda Katiba ya nchi. Vile vile katika suala zima la utawala bora, naamini kwamba ndiyo maana kuna mihimili mitatu ambapo kuna *Judiciary*, *Executive* na *General Assembly* ambalo ni Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nitaongelea upande wa Bunge na nitaomba nisome Ibara ya 63(2) (a) na (b). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kunukuu: "Sehemu ya pili ya Bunge itakuwa ndiyo chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka kwa niaba ya wananchi kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii." Ibara ndogo ya tatu, inasema: "Kwa madhumuni ya utekelezaji wa madaraka yake Bunge laweza (a) Kumuuliza Waziri yeyote swali lolote kuhusu umma katika Jamhuri ya Muungano ambayo yapo katika wajibu wake. (b) Kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bunge wa kila mwaka wa Bajeti." Naomba niishie hapo ingawa baadaye nitaomba kunukuu tena kifungu kidogo (e). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnaweza kushangaa labda kwa nini nimeanza kusoma Ibara hiyo, lakini naamini kabisa kwamba kila mhimili una kazi zake na una madaraka yake kama yalivyoonyeshwa kwenye Katiba ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba nitoe masikitiko yangu ya dhati na nitaomba radhi Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kama baba yangu. Mheshimiwa Yussuf

Makamba ni kama baba yangu pia, lakini nitaomba radhi kwa hilo kwa sababu lazima nilisema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vyombo vya habari tarehe 23 Juni, 2007 ilionyeshwa kwamba Waziri Mkuu pamoja na Mheshimiwa Yussuf Makamba ambaye ni Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi waliwaonya Waheshimiwa Wabunge ambao wanaongea na kutoa hoja zao hapa Bungeni kwa kuona kwamba labda wanaikosoa Serikali. Lakini mimi naamini Bunge si hili jengo ni Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Wabunge hawana dhamana yoyote, dhamana yao ni kutoka kwa wananchi na kila mtu amepigiwa kura aje atetea wananchi wake. Mbunge anapokuja na kuongea suala lolote kuhusu Jimbo lake, naomba asikilizwe kwa sababu anatimiza wajibu wake Kikatiba. Naomba niishie hapo nadhani Serikali italifanyia kazi hili na ninathibitisha kwa kutumia gazeti hili la Tanzania Daima. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. BATILDA S. BURIAN):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 50. Mheshimiwa Mbunge anazungumzia jambo zito sana hapa. Kwanza, kumhusisha Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Mbunge ambaye ndiye Katibu Mkuu wa CCM katika masuala ambayo hana uhakika nayo; na kwa uhakika si kweli. Sisi tumekanusha suala hilo, lakini Mheshimiwa Mbunge anazidi kulisema na kulinukuu hilo gazeti. Naomba atoe ushahidi wa Mheshimiwa Mbunge aliyeitwa na kuonywa bila hivyo namwomba afute maelezo yake hayo aliyoyatanguliza. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI:** Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu alichokisema ni sahihi, si kila kiandikwacho kwenye gazeti ni sahihi. Baada ya kupata maelezo hayo ya upande wa Serikali kwamba jambo hilo si sahihi. Je, Mheshimiwa Mbunge unaweza kuliweka sawa sawa ili uweze kuendelea kuchangia?

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Lakini mimi nimeongelea hili kwa sababu halikukanushwa na Waheshimiwa Wabunge humu ndani wanatumia magazeti. Kwa hiyo, lilikuwa ni angalizo tu kama Mtanzania wala si kwa nia yoyote mbaya. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonekana Mheshimiwa Mbunge hasomi magazeti. Mimi nimekanusha na imeandikwa kwenye magazeti kwamba hakuna Serikali iliyomwita Mheshimiwa Mbunge na kumkaripia. Hakuna ushahidi wowote ule. Naomba anunue magazeti asome.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Inawezekana labda sikuliona na nilikuwa nimeshaandaa kutoa hili angalizo. Kwa hiyo, naomba nifute usemi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema hivyo labda inaonyesha kwamba nilitaka kutimiza wajibu wangu Kikatiba.

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, usiendeleze mjadala huo baada ya hatua ile ya kufuta usemi wako. Sasa endelee kuchangia mambo mengine.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niendelee kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niende moja kwa moja kwenye mchango wangu. Tangu nakua mpaka leo nchi yetu bado ni maskini na kweli jambo hili linanisikitisha sana; na kila mara tunaambiwa nchi yetu ni changa. Sasa hivi mimi kweli sijafikisha miaka 30, lakini siwezi kupita barabarani nikaambiwa huyo mtoto ni mchanga. Sasa kinachonisikitisha zaidi ni taarifa ya Mheshimwa Dr. Juma Ngasongwa katika hotuba yake, naomba ninukuu ukurasa wa 83 inahusika na misingi na malengo ya uchumi jumla na maendeleo ya jamii kwa kipindi cha muda wa kati wa 2007/2008 hadi 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ninukuu: "Pato la Taifa halisi litakua kwa asilimia 7.3 mwaka 2007, asilimia 7.7 mwaka 2008, asilimia 7.9 mwaka 2009 na asilimia 8.1 mwaka 2010." Huu ninaona kabisa ni mwendo wa kinyonga kwa sababu tunatakiwa tu-*aim higher*. Mwanafunzi anaposema kwamba anataka apate "A" ni kweli ata-*struggle* apate ile "A". Lakini akisema anataka apate "C" anaweza akapata "C" au "D".

Kwa hiyo, angalau tujitahidi kuwa na fikra mbadala kuangalia ni jinsi gani tutakavyoongeza pato letu. Kwa kuongeza hizo *zero point one*, *zero point three* ili uchumi uweze kukua naona kwamba ni kiasi kidogo, tujitahidi kwa kweli ingawa tunasema kwamba nchi yetu ni maskini. Lakini vile vile tuna rasilimali za kutosha ambazo tunaweza tukazitumia kututoa hapa tulipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka katika historia Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, alisema kwamba tunahitaji mambo manne ili tuweze kuendelea, la kwanza, ni watu, na tuko zaidi ya watu milioni 35, naamini kabisa tukipewa elimu ya kutosha, tukawezeshwa, kila mwananchi akajua wajibu wake katika nchi yake anaweza akatumika vizuri. Rasilimali watu ikitumika vizuri tunaweza tukajitahidi kujiondoa katika hali ya umaskini kwa sababu kila mtu atakwenda katika Sekta ile kulingana na jinsi alivyowezeshwa kielimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende haraka haraka kwenye ardhi, tunayo ardhi zaidi ya kilomita za mraba laki tisa na zaidi na humo kuna rasilimali nyingi yakiwemo madini, maji, mito, wanyamapori na vyote hivyo vikitumika vizuri vinaweza vikatuondoa katika maskini huu ambao tunao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nashangaa kidogo kwa mfano, Tanzania ni nchi pekee inayotoa *Tanzanite,* ila katika vyombo vya habari maana yake tunaambiwa tusome kwenye vyombo mbalimbali, kwenye *Internet* inaonyesha kwamba Kenya ilipewa tuzo kwa kuuza *Tanzanite*, *South Africa* inaongoza kwa kuuza *Tanzanite*, lakini *Tanzanite*

inatoka Tanzania. Tujitahidi kujirekebisha kidogo ili rasilimali yetu iweze kuitumika vizuri na ituwezeshe kutukwamua mahali ambapo tulipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mfano kama *Pound* ya Uingereza iko *based* au imethaminishwa na dhahabu na ndiyo maana iko *strong,* lakini kule hawana hata machimbo ya dhahabu. Sisi shilingi yetu inaendelea kuporomoka kila siku, hebu tujiulize labda sababu ni ipi na tujitahidi kuweka misingi ambayo itatusaidia ili shilingi yetu isiendelee kuporomoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo hilo suala la ardhi tunayo ardhi ya kutosha itakayotusaidia katika kilimo, lakini kabla ya Uhuru mpaka leo jembe linalotumika ni la mkono, kilimo bado ni duni, pembejeo ni za bei ya juu, kilimo kinaonekana pia hakina tija kwa wakulima. Ingawa vile vile katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji alionyesha jinsi watu walivyojiajiri; na ni asilimia 81 inaonekana watu wamejiajiri kwenye kilimo, lakini bado ni maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo hicho ndicho kinachotusaidia sisi kulisha Taifa, ingawa bado wanategemea mvua, lakini tujitahidi tukiinue kwa vitendo na si kwa maneno kama ilivyo kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua juhudi zinafanyika, lakini ziongozwe kidogo angalau kuanzishwe Vyama vya Ushirika vitakavyowasaidia hao wakulima ili wafikie hatua ya kujipangia bei ya mazao yao, kodi ndogo ndogo kwenye mazao zipunguzwe, miundombinu ya vijijini hasa barabara ziweze kutengenezwa angalau wakulima waweze kusafirisha mazao yao mpaka kwenye soko. Vile vile naiomba Serikali ishirikiane na sekta binafsi kuhakikisha kwamba inafanikisha hayo kwa sababu wananchi kusema kweli hali zao ni duni. *(Makofi)*

Naomba niendelee kwenye suala lingine, pamoja na kuimarisha kilimo tujitahidi vile vile kuhakikisha kwamba tunaanzisha viwanda vidogo vidogo kwa ajili ya usindikaji wa matunda angalau hata kule Tanga. Kwa sababu tunakunywa *juice* kutoka Afrika Kusini na Uarubuni. Mfano, Uarabuni ni nchi ambayo ni ya ukame. Kwa hiyo, angalau tujitahidi kwa sababu kilimo vile vile kinaenda na viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hayo mambo manne, lakini bado kuna suala la siasa safi na uongozi bora. Katika hali ya siasa naona kwamba hali siyo mbaya sana kwa sababu tuna amani na utulivu hata Mheshimiwa Waziri Mkuu amethibitisha hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile mimi naona kwamba bado kidogo katika suala la uongozi au tuseme utawala na utendaji. Kwa sababu hata hapa Bungeni tunapouliza maswali mara nyingi tunajibiwa vuta subira, vuta subira, na kila siku unaambiwa vuta subira. Kwa sababu hata mimi nimeingia hapa Bungeni na kabla hata sijaja hapa Bungeni na tangu hata nikiwa mdogo najua kabisa kwamba Waheshimiwa Wabunge wakiingia humu ndani hasa kutoka Kigoma walikuwa wanaomba barabara na mpaka leo mimi nikisimama vile vile naikumbusha Serikali itujenge barabara. Wakati wananchi kule

wanalipa kodi na ni wajibu wa Serikali siyo mpaka sisi tuombe ni wajibu Serikali kuitimizia jamii yake kwa sababu inalipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango ya Serikali inaonekana iko mingi ya kututoa hapa tulipo, lakini naomba nguvu kidogo iongezwe. Kwa mfano, tuna MKUKUTA, MKURABITA, MKUMBITA, *Tiger Plan, vision 2025,* mipango iko mingi kwa kweli, lakini imeandikwa vizuri sana kwenye makaratasi ila utekelezaji unakuwa mdogo. Labda ni kwa sababu asilimia 42 ya Bajeti inategemea zaidi kwenye misaada na mikopo. Lakini tujitahidi kidogo kwa sababu tuna rasilimali za kutosha tunaweza kujitoa hapa tulipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini pia katika utawala bora na uongozi bora kuna mambo ambayo yanatakiwa yaonekana wazi. Katika uongozi bora naamini kabisa uongozi ambao unakuwa na uwazi unaowashirikisha, unaotimiza ahadi zake, unaokubali changamoto na unaokubali ushauri unaweza kidogo ukatutoa hapo tulipo. Kwa hiyo, naomba Serikali iongeze juhudi kwa hapo, siyo rahisi ndiyo kwa kiongozi au uongozi kuwa na hayo yote, lakini angalau yaani jitihada ziongezwe kutokana na dhamana ambayo wanayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hayo manne pia yanahitaji *political will* au utashi wa kisiasa ili tuweze kuyatimiza. Uzalendo na vile vile uwajibikaji kwa kila mtu ili tuweze kutimiza hayo mambo manne. Lakini vile vile utashi wa kisiasa bado unaonekana ni mdogo na haujaweza kutosheleza katika kutimiza hayo, ndiyo maana mpaka leo labda tuko hapo. Huo ni mtazamo wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naona kwamba kuna ubinafsi bado, uzalendo pia hautoshi, maadili vile vile hayatoshi kwa wafanyakazi. Nakumbuka hata mwaka jana Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake alisema kwamba: "Kila mtu acheze ngoma inayopigwa kwa *style* moja anayoitaka yeye." Lakini *style* hiyo inaonekana bado kuna watu wanaocheza vibaya ndiyo maana taarifa ya *CAG* ilionyeshwa kwamba fedha nyingi zimepotea au hazieleweki ziko wapi. Kwa hiyo, naamini kabisa ili waweze kucheza ngoma, ule mdundo anaotaka yeye lazima wale watu wachukuliwe hatua ili waliobaki sasa labda kwa mwaka huu wahakikishe kwamba hawatarudia yale ambayo wameyakosea au hawatacheza ile staili tofauti na yeye alivyokuwa anataka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala hilo nasema bado kuna watendaji wanacheza *style* tofauti na Mheshimiwa Waziri Mkuu anavyotaka. Mikataba mingi bado inaonekana haijaweza kurekebishwa ingawa Rais mwenyewe alisema kwamba mikataba itaweza kurekebishwa kutokana na kwamba wananchi wanalalamika na mikataba inaonekana haina tija. Sasa kuna mikataba mingine ambayo wameendelea kuingia, kuna baadhi ya mikataba kama ya *Richmond* ambayo sasa hivi imeuzwa kwa *Dowans* imeleta maneno mengi. Lakini nilikuwa naomba kwamba taarifa yake iletwe Bungeni angalau iondoe zile hisia mbaya kwa wananchi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sina tatizo nayo, lakini naomba kama Ibara ya 63(3(e) inavyosema kwamba: "Bunge lina wajibu wa kupitisha mikataba yote." Kwa hiyo, nilikuwa naomba kidogo hilo suala pia liangaliwe ingawa tunaambiwa kwamba tutatoa siri za biashara.

Lakini yale masuala muhimu naomba tungeweza kuletewa Bungeni tukaweza kuyajadili. Nadhani hata hilo Mheshimiwa Rais alisema kwamba mikataba itaangaliwa upya. Naomba kweli hiyo ahadi itimizwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siamini ndoto ya kusema kwamba utandawazi wa sera ya uchumi wa soko huria unaweza kututoa hapa tulipo hasa kwa kubinafsisha madini yetu au mali zetu kwa Mashirika ya nje. Tuangalie mfano tu wa Zaire ambayo sasa inaitwa Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo. Walianza kuchimba madini siku nyingi sana lakini mpaka leo yale mashirika yanaenda kunufaisha kwao badala ya nchi husika. Kwa hiyo, tuangalie tusiwe vipofu, tuangalie mifano mingi ipo hata Angola, *situation* ni kama hiyo hiyo. Kwa hiyo, nilikuwa na angalizo kidogo hebu tuangalie Geita, turudi katika taarifa ya mwaka 2005 ya umaskini, inaonekana ni Wilaya maskini na ya mwisho. Sasa tuangalie pale kuna maliasili nyingi na pale kuna machimbo yanaendelea. Sasa kwa nini Wilaya ya Geita iwe Wilaya ya mwisho kwa umaskini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye mchango wa jumla kwa sababu sina uhakika kama nitapata nafasi katika Wizara nyingine. Nikienda moja kwa moja katika Wizara ya Nishati na Madini, naomba tuangalie katika suala la umeme, mwaka jana tulitengewa shilingi bilioni 10, sijajua zimefikia wapi, ulikuwa ni mradi wa umeme wa gridi ya Taifa kupitia Tabora. Sasa naomba kujua umefikia wapi na mpaka sasa tunaanzisha mradi mwingine wa umeme wa kutoka Malagarasi. Kwa hiyo, naomba kujua hiyo miradi itaenda namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kwenda haraka haraka naomba niende Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujua mpaka sasa hivi Serikali inatumia fedha kiasi gani katika kupangishia nyumba watumishi wake. Mfano mdogo tu kwa Mahakimu wa Tabora wanakaa *Orion Tabora Hotel* na kwa kipindi cha miezi sita tumepiga mahesabu maana yake tangu tarehe 6 Mei, 2007 walikuwa bado wanakaa hotelini. Kwa hiyo, nifanye hesabu kwa muda wa miezi sita, labda tuchukulie wanakaa *suit* Hakimu mmoja akikaa kwenye *suit* ni shilingi120,000 kwa siku 30 ni shilingi 3,600,000 kwa miezi sita ni shilingi milioni 21,600,000 kwa watu wote watatu sasa ni shilingi milioni 64,800,000.

Sasa tujiulize nchi inapoteza fedha kiasi gani kwa tatizo la uuzaji wa nyumba uliofanyika katika awamu iliyopita, kwa sababu hii ni Serikali inayoendelea. Nadhani majibu yatakuwepo na naweza kutusaidia kutufahamishia ni kiasi cha fedha kimetumika mpaka sasa hivi kuwalipia watumishi nyumba wakati zilikuwepo. Kwa hiyo, Serikali inapofanya maamuzi, mimi naomba iangalie madhara ya baadaye kwa sababu inakuja kuwa *cost* kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kengele haijanigongea, naomba kuuliza kuhusu miundombinu. Mheshimiwa Waziri Mkuu nakumbuka mwaka jana aliitetea Wizara hii kwa kusema kwa kuanzia miaka hii mitatu barabara ya Kigoma - Nyakanazi itajengwa na ile ya kupitia Tabora. Naomba kujua ni lini barabara hiyo itaanza kujengwa na ile ya kupitia Tabora itakamilika lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye Wizara ya Mazingira, naomba kumuuliza Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, ule mpango wa *Lake Tanganyika* wa Mazingira umefikia wapi kwa sababu alitwambia tukawahamasishe wananchi, nilijitahidi kuwahamasisha wananchi kuanzia Kagunga mpaka vijiji vyote vya Kando ya Ziwa. Lakini wanatwambia sisi ni waongo mbona hawajaona chochote? Maana yake waliambiwa kwamba ule mradi utawatoa katika hali ya umaskini, akinamama wakajiunga katika vikundi, wavuvi watapewa mashine za kuangalia samaki wako wapi. Sasa sisi tunaonekana ni waongo, naomba hizo taarifa ziweze kutolewa mara kwa mara angalau tuwe tunapata cha kuwajibu wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naomba niende Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kama kuna mpango wa kujenga hospitali mpya, naomba Kigoma Vijiji isisahaulike jamani, wanatumia hospitali moja tu ya Mkoa ya Maweni, akinamama wengi wanafariki wakiwa njiani wakitoka vijijini kupelekwa hospitali hasa wale wanaotaka kujifungua na wengine wanajifungulia njiani na watoto wengine wanakufa.

Kwa hiyo, naiomba sana Serikali pamoja na kwamba ni wajibu wake, lakini naomba tuikumbushe kwamba katika hayo ituangalie jamani. Maana yake ahadi zimekuwa ni nyingi, sasa tunashindwa tuwaambie nini wananchi. Ndiyo maana hapa Waheshimiwa Wabunge wengi wanaomba waambatane na Mawaziri kwa sababu inakuwa kila ukienda unaulizwa maswali ili wakayajibu wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naomba niishie hapo. Nadhani muda wangu umenitosha. *(Makofi)*

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii nami kuchangia hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijafanya hivyo, nami ningependa kuungana na Waheshimiwa Wabunge kutoa salamu za rambirambi kwa msiba mkubwa uliotupata kwa kumpoteza ndugu yetu, Mheshimiwa Amina Chifupa. Mwenyezi Mungu awape subira wazazi, ndugu na wapendwa wote na ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, *mic* yako isogelee kidogo ili uweze kusikika vizuri zaidi.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Napenda kuchukua fursa hii kumpongeza kwa dhati sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wake, Makatibu Wakuu wake na viongozi wote wa Wizara pamoja na taasisi na Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kwa kazi nzuri waliyoifanya na kwa hotuba nzuri iliyowasilishwa. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imeonyesha jinsi gani Serikali ya Awamu ya Nne, imefanya jitihada za kuitafsiri kwa ufasaha mkubwa kabisa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005. Ndani yake humo sera zimetafsiriwa, mipango imepangwa vizuri, mikakati imetekelezwa vizuri kiasi kwamba hata changamoto kubwa tulizozipata za ukosefu wa mvua, ukame, kupanda kwa bei ya mafuta na mafuriko yote

hayo hayakuweza kuyumbisha uchumi, uchumi ukaendelea katika hali nzuri; na kutokana na hatua nzuri zilizoelezwe humu ndani katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuna matumaini mazuri sana kwamba tutaendelea na kasi kubwa na kuweza hata kupita kile kiwango cha asilimia 10 ya wastani ya ukuaji wa Pato la Taifa ifikapo mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango hiyo mizuri imewezekana kutekelezwa kwa sababu ya umahiri mkubwa sana wa viongozi wakuu wetu wakiongozwa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Waziri Mkuu na viongozi wengine ambao wamekabidhiwa nyadhifa za kuongoza Serikali ya Awamu ya Nne. Sasa katika hili tumeona wazi kwamba yapo mengi ambayo yanaweza kufanyika kufikia maendeleo yanayotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikichukua mfano wa kutoka *Management Science* kazi kubwa za uongozi ni kuanza kupanga, pili ku-*organize*, tatu, kuweka *staff*, nne, ku-*direct,* tano, *contro*l, sita, *motivation*. Katika hili mipango imekuwa ni mizuri sana na kama vile tumeweka dira na mwelekeo mzuri. Mambo ya *direction* Waziri Mkuu hotuba yake ni kama vile zege ya jamvi katika msingi wa nyumba ni msingi mzuri sana. Kinachotakiwa sasa hivi ni Wizara nyingine na taasisi nyingine katika kutekeleza hayo inavyotakiwa ili tuweze kupata mafanikio yanayotakiwa.

Kwa hiyo, nikichukua ujenzi wa nyumba tayari tumepata ramani nzuri, tayari tumepata msingi mzuri, kinachotakiwa sasa na sisi wengine wote kushirikiana ili hiyo nyumba nzuri na imara tunayotaka kuipata tuweze kuijenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika haya yote, masuala makubwa ambayo tunatakiwa kufanya ni kuboresha zaidi suala la *stuffing function*, *direction* na *control*. Katika sehemu kubwa Waziri Mkuu ameeleza inabidi kuchukua hatua thabiti za kuhakikisha kwamba maboresha yanaleta matokeo yanayotakiwa. Mpaka sasa Bajeti na mipango iliyopo na mingi ya mikakati hii iliyopo kwa bahati mbaya haiteremki mpaka chini kabisa ikawafikia wananchi ingawa sera ni kupeleka madaraka kwa wananchi na uongozi shirikishi, lakini hapo katikati mambo hayo yanaishia kwenye ngazi ya Halmashauri ikizidi sana ni baadhi ya Kata na vijiji lakini vingi havijahusika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, iko haja ya kutazama upya mfumo huo na kuona kwamba watendaji wanaowekwa ni wale watendaji ambao wanaweza kufanya hili vizuri. Kwa hiyo, katika maboresha siyo tu mafunzo wapewe hao, lakini vile vile mafunzo wapewe wanavijiji ili waweze kuelewa mikakati mbalimbali iliyopo, mifuko mbalimbali iliyopo ili waweze kuibua kero na kuzitekeleza vizuri na hao watekelezaji wakawa wanazitekeleza kwa ufanisi mzuri. Sasa suala la kukuza ufanisi na tija ni suala la msingi. Hili linaweza kufanyika iwapo kutakuwepo na utaratibu mzuri wa utekelezaji na utekelezaji huo unaweza kuwa mzuri iwapo kutakuwa na utaratibu wa ushindani rasmi. Tulipokuwa kwenye Mkutano wa *ALART* Taifa mwaka jana ilipendekezwa kwamba ni vizuri pawepo na utaratibu wa ushindani kuanzia kwenye Kaya, Vitongoji, Vijiji, Kata, Wilaya, Mikoa ishindane kwa kuwekewa malengo na kuwekewa vigezo vya utekelezaji wale watakaoshinda wapewe zawadi na wale wanaoshindwa waadhibiwe wao

wenyewe badala ya kuadhibu Halmashauri nzima au wananchi ambao hawana makosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru hilo limefanyika na nashukuru limeanza vizuri baada ya Mheshimiwa Rais kuwaita wahusika wote siyo tu katika semina elekezi, lakini pia katika mikutano maalumu baada ya kupata taarifa ya *CAG.* Nafikiri hilo kama litafanyika vizuri mambo yataenda vizuri. *(Makofi)*

Sasa baada ya hapo, ningependa kuzungumza kidogo kuhusu masuala yetu ya Wilaya ya Mkinga. Wananchi wa Wilaya ya Mkinga wanatoa shukrani nyingi sana kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kujua matatizo yake na kuigawa Wilaya haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nieleze kwamba pamoja na kuwa Kaskazini, lakini Mkinga ni Wilaya ya pembezoni kwa maana zote za pembezoni. Pembezoni kwa maana kwamba inapakana na nchi jirani ya Kenya, pembezoni kwa maana ya uchumi. Kimaendeleo ipo nyuma sana bado. Sasa kwa mantiki hiyo inahitaji rasilimali nyingi sana ili iweze kupata kasi ya maendeleo inayotakiwa. Majibu ya Mheshimiwa wa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI leo asubuhi alipomjibu Mheshimiwa Herbert Mntangi katika swali lake ni kwamba Halmashauri mpya hazitarithi rasilimali au mali kutoka Halmashauri za Wilaya mama, limenitia hofu sana, kwa sababu sisi Wilaya ya Mkinga hatuna chochote mpaka sasa na Bajeti haionyeshi kama tutapewa fedha za kutekeleza mambo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri ipo haja ya kutazama suala hili upya na kuona vipi ama tutapewa vifaa kutoka Wilaya ya Muheza ambayo ilikuwa Wilaya mama au tutaongezewa fungu la kuweza kupata vifaa hivyo.

Pili, matatizo mengine ni kama yalivyoelezwa juzi na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, kama ambavyo alisema kwamba miradi hiyo ya maji haijatekelezwa siyo tu kwa sababu ya matatizo ya urasimu wa Benki ya Dunia, lakini inatakiwa Halmashauri iundwe itekeleze hayo. Halafu ndiyo hatimaye iweze kufanya hivyo. Sasa utaratibu wa namna hiyo nafikiri hautufai sana kwa Wilaya hiyo. Naomba utazamwe upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuchukua fursa hii kutoa shukrani nyingi sana kwa Serikali kwa jinsi ambavyo imechochea maendeleo katika Wilaya yetu. Suala la elimu ni suala ambalo tumepata mafanikio makubwa sana. Mwanzoni mwa mwaka 2006 tulikuwa na shule za sekondari tatu tu, hadi mwanzoni mwa mwaka huu tumekuwa tayari na shule za sekondari 14 na nyingine mbili zinajengwa. Kwa hiyo, hayo ni mafanikio makubwa sana, naipongeza sana Serikali na nawapongeza sana wananchi kwa ushirikiano wao na napenda kuchukua fursa hii kusema kwamba wale wanaosema kwamba CCM haijafanya lolote au Ilani ya CCM haijafanya lolote hawasemi kweli, waaibike kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tumepata msaada mkubwa katika kujenga zahanati na huduma nyingine mbalimbali. Madaktari wanakuja, walimu wanakuja,

natumaini jitihada zitafanywa waje zaidi. Sasa tatizo kubwa tulilonalo sasa hivi sisi ni miundombinu. Miudombinu licha ya kuwa hafifu, mafuriko yaliyotokea hivi karibuni yaliharibu sana. Naamini kwamba Bajeti hiyo tuliyopitisha na ambayo imeelekeza kwamba tuwe na mfuko mkubwa zaidi itaangalia na kusaidia zile barabara zetu za Halmashauri ambazo zimeharibika. Lakini kuna mawili makubwa na mazito. *(Makofi)*

Moja, Mheshimiwa Waziri Mkuu tunamshukuru alivyotutembelea Wilayani kwetu na akaona matatizo ya barabara, lakini barabara ile ambayo inaunganisha Kasera Makao Makuu na sehemu zingine za Wilaya haipo na hiyo ni kero kubwa sana kwa wananchi na Mheshimiwa Waziri Mkuu najua jinsi gani wananchi walivyoeleza kero hiyo kwa hasira kubwa. *N*aamini kwamba hatua thabiti zitachukuliwa ili barabara hiyo iweze kutengenezwa ili kusaidia kusukuma mbele maendeleo na kuwafikia wananchi katika huduma nzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, donda kuu katika masuala ya miundombinu ni barabara ya Tanga - Horohoro. Kabla sijazaliwa na baada ya kuingia Bungeni hii imekuwa ni kero kubwa. Wananchi wanaipigia kelele sana. Tumekuwa tukipewa ahadi kila siku itajengwa, tukaambiwa inafanyiwa upembuzi yakinifu, tunakaambiwa inafanyia *design* na mambo chungu nzima. Alama za "X" kwenye nyumba zimewekwa zaidi ya miaka mitano iliyopita, baadaye miaka miwili iliyopita imewekwa alama "NR". Wananchi wanababaika hawajui nini la kufanyika. Barabara inazidi kuwa mbaya na utalii tunataka kuufanya unashindikana na jitihada nyingine za kufanya zinakwama kabisa. Safari hii nimefuatilia tena kwenye Wizara nikaambiwa labda *MCC* huenda wakatoa fedha kwa hilo.

Mheshimiwa Waziri Mkuu ningependa kusisitiza kwamba hili ni kero kubwa na linatia aibu sana kwamba katika nchi zote za Afrika Mashariki barabara ya Kimataifa ambayo inaunganisha nchi mbili na ambayo haijawekewa lami peke yake ni Tanga - Horohoro. Sababu haifahamiki ni nini? Sasa tunapenda tupewe uhakika au baada ya Bunge hili niongozane na Waziri akawaeleza wananchi kwa nini barabara hiyo inaachwa siku zote na lini itatengenezwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni *Tanga Develompement Corridor,* Wilaya ya Mkinga ni sehemu ya *Tanga Development Corridor* na matumaini makubwa ni kwamba chini ya *Tanga Development Corridor* tutaweza kupata maendeleo mengi ya shughuli mbalimbali za uchumi na utalii. Lakini katika mipango, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu haijaeleza lolote juu ya *Tanga Development Corridor*. Hatujasikia lolote habari ya Bandari ya Tanga, hatujasikia lolote habari ya Reli ya Tanga*,* Anga - Musoma, hatujasikia lolote habari ya utengenezaji wa bandari ndogo za Moa, bandari ndogo ya Kwale na bandari ya Pangani. Haya mambo kwa nini yanakuwa hivi ambapo tunazungumzia *Development* ya upande mwingine. *(Makofi)*

Tunajua kwamba haya yakifanyika itawezekana vilevile ule mradi wa *NOTRON* kuja na vilevile kufaidisha Wilaya ya Mkinga na Wilaya zingine za Tanga. Sasa, tunaomba masuala hayo yapewe uzito unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maji pamoja na kuwa na mabonde na vilima vingi kule kwetu bado tuna matatizo makubwa sana ya maji. Ningeomba suala hilo lipewe uzito mkubwa bila kukawia zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Uwezeshaji wananchi, tunashukuru kwamba Serikali ya Awamu ya Nne, imetengeneza sera nzuri, mikakati mizuri pamoja na mifumo mingi mizuri sana.

Kama alivyosema pale awali jitihada kubwa zimefanywa kuwahamasisha wananchi na wananchi wengi wamehamasishwa. Kuhusu Mfuko wa Uwezeshaji wajasiriamali tumetengeneza vikundi vingi sana.

Lakini mpaka sasa hivi vikundi hivyo havijaweza kufaidika kwa sababu ya utaratibu na wakati mwingine tuliambiwa kwamba fedha zimekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama fedha zimekwisha Mkoa wetu wilaya nane, sasa hizi wilaya saba ndizo zimemaliza hizo fedha? Nashauri pawe na utaratibu mzuri wa kugawa fedha hizi ili wananchi wote katika wilaya zote waweze kufaidika kwa usawa, pasitokee wengine wanapata na wengine wanakosa.

Vile vile katika uendelezaji wa Wilaya hii tunashukuru sana kwa kazi kubwa iliyofanywa na Serikali kwa kutoa fedha za kujenga Wilaya yetu. Tayari majengo ya boma na majengo ya nyumba za wafanyakazi waandamizi yamekwishafikia hatua nzuri sana.

Tunashukuru vilevile.......!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge kengele ya pili.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Awali ya yote naomba kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kutuchagua jana kwenda kuwawakilisha katika msiba mkubwa tulioupata wa ndugu yetu, tunaomba kutoa salamu kwamba wafiwa wamefarijika sana na kuweko kwetu katika msiba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, wakati nikiwasilisha hotuba yangu ya Bajeti hapa, Waziri wa Fedha alinukuu maneno yangu niliyosema kwamba "Hotuba yetu ilikuwa na mapungufu." Tulikiri mapungufu kwa takwimu na maandishi, naomba kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba bado tunaendelea kukiri…….!

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Kuhusu Utaratibu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia Kanuni ya 43(7), na naomba niinukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kila mmoja anaelewa kwamba sisi hapa Bungeni tunakwenda kwa mujibu wa Kanuni. Kanuni Namba 40(7) inazungumza kama ifuatavyo, "Bila ya kuathiri masharti ya Katiba au kanuni hizi, Mbunge yeyote aweza kupendekeza jambo lolote lijadiliwe Bungeni."

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani sana, Kanuni ya 43(7). "Mbunge yeyote hatoruhusiwa kufufua jambo lolote ambalo Bunge lilikwisha kuliamua ama katika Mkutano huo uliopo au ule uliotangulia isipokuwa kwa kufuata masharti ya Kanuni 44(2)."

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri wa Fedha na hotuba ya Waziri wa Mipango ilikwishaamuliwa hapa Bungeni tena kwa kura na sisi na wao walipiga kura. Sasa leo tunaanza kufufua tena ina maana Waziri wa Fedha tumlete tena hapa ajibu yale?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako? (*Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haroub anachokisema ni kwamba Kanuni ya 43(7) inasomeka ifuatavyo. "Mbunge yeyote hataruhusiwa kufufua jambo lolote ambalo Bunge lilikwisha kuliamua ama katika Mkutano huo uliopo au ule uliotangulia isipokuwa kwa kufuata masharti ya Kanuni ya 44(2) ambayo yenyewe inasema, "Kwamba taarifa ya hoja ambayo kwa maoni ya Spika ina lengo la kujaribu kutaka lifikiriwe tena jambo ambalo lilikwisha kuamuliwa na Bunge katika kipindi cha miezi 12 iliyopita kabla ya kikao kinachoendelea halitakubaliwa na Spika isipokuwa tu kama ni hoja ya kutaka uamuzi wa Bunge uliokwishafanyika ubadilishwe."

Mheshimiwa Hamad Rashid unasemaje?

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naona tunasema vitu viwili tofauti.

Mimi sizungumzii hoja iliyoamuliwa ndani ya Bunge, nazungumzia *statement* inayonihusu mimi Mbunge, haijaamuliwa na Bunge. Ni *statement* inayonihusu mimi Mbunge! Naomba mwongozo wako kama nazungumzia hoja inayonihusu mimi Mbunge, sizungumzii uamuzi wa Bunge!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, unaweza kuendelea lakini uwe makini na vifungu hivyo tulivyovisema.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwamba ninachozungumza ni kwamba kwa upande wetu sisi tunakubali suala la kukosolewa kwa sababu tuna upungufu wa kibinadamu, hatuna ukamilifu. Kwa hiyo, tunakubali kabisa na haya ni maneno sahihi kwamba yapo. Hatuna uzoefu kama wenzetu, tuna upungufu wa uzoefu na tutaendelea kujifunza. Tunasema tunataka tukiri tu kwamba si tusi kwetu kwamba tumesema hilo kwamba lionekane ni tusi hapana! ni kitu ambacho tunakikubali tuna upungufu kama binadamu na wenzetu ambao ni wakamilifu tutaendelea kujifunza kutoka kwao. Hilo nilikuwa nikitaka kuliweka bayana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, Benki Kuu ni chombo cha Muungano na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake ametaja mambo ya Muungano katika ukurasa wa 10, haidhuru mengine mengi ameacha, mimi nilifikiri ataeleza habari ya mafuta Pemba wamefikia wapi, hakusema chochote na mazungumzo mengi yamefanyika, nafikiri atatujibu baadaye. Lakini nasema Benki Kuu ni chombo cha Muungano, Zanzibar ina asilimia 11.02. Kwa hiyo, maamuzi yote yatakayotolewa juu ya Benki Kuu Zanzibar ilikuwa na haki nayo kujua hatima ya maamuzi hayo.

Benki Kuu katika kikao chake cha mwaka 2003 wakati kinazungumzia matengenezo ya Benki Kuu walipanga kutumia kama dola za Marekani 37 milioni kama mradi wa Benki Kuu. Hatimaye gharama zikaanza kuongezeka na kukawa na Kikao cha Ushauri cha baadhi ya Wanachama wa Baraza la Mawaziri na baadhi ya Mawaziri hao wakakataa kwamba gharama zisiongezeke na ile ile bajeti ya mwanzo iendelee. Lakini kwa sababu ya utaratibu wa kiutawala basi amri ikatolewa itaendelea. Sasa sisi tuna mambo matatu ambayo tunataka Serikali itusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mmetoa tamko kusema kwamba kuna *External Auditor* atakayekuwa-*appointed* kufanya uchunguzi. Uchunguzi inaouzungumzia Serikali ni uchunguzi wa *External debts*. Sisi tunachosema ni kwamba upotevu katika Benki Kuu haupungui dola za Marekani 800 milioni, unahusu ujenzi wa jengo lenyewe. Katika *Hansard* ya Waziri wa Fedha alisema ni Dola milioni 108 kutoka Dola milioni 37 za kwanza mpaka Dola milioni 108 na leo tuna taarifa ya Dola milioni 340. Tunazungumzia *value for money of that building*, huwezi ukamchagua Mkaguzi kumwambia nenda katuangalilie *external debts* ukaacha *areas* nyingine ambazo sisi tumesema zina upungufu mkubwa ndani ya matumizi ya Benki Kuu. Hiyo ni sababu ya kwanza kwamba huyu *external auditor* hatotusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Benki Kuu imekuwa ikifanyiwa uchunguzi wa hesabu zake kwa kutumia *external auditors*. Nimezipitia akaunti zao zote hakuna hata pamoja wameonyesha kama kuna ubadhirifu au uharibifu katika Benki Kuu! *That is why* tumefika mahali tunasema *the only instutition* itakayosimamia matumizi ya wananchi, haki za wananchi, wavuja jasho, ni Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ndiyo tukasema tuunde *select committee* ya Bunge na taarifa yake ije Bungeni.

La tatu, taarifa inayotoka kwa *Auditor General* ni taarifa ya Serikali na Rais ana maamuzi kabisa kwamba je niipeleke kama ilivyo au lipi na lipi nipunguze, si taarifa ya Bunge. Tunachotaka hapa ni Taarifa ya Bunge kama chombo na kwa mujibu wa Ibara ya 63 ya Katiba kinalipa madaraka Bunge kuisimamia Serikali. Kwa hiyo, bado tuna hoja yetu ya msingi kwamba sisi tunaona kwamba hakuna sababu yoyote ya Serikali kukataa kwamba tufanye uchunguzi wa kina ili tujue matumizi yote ya Benki Kuu. Nataka kuwaambia Waheshimiwa Wabunge hili si la itikadi. Pale sasa hivi tumekuwa ndio pakacha letu; ndio chungu chetu. Wakulima wa pamba, karafuu, nazi, wavuvi, chote tunachokipata tunakipeleka pale. Kama pale panavuja, ni nini hatima ya nchi hii? Nini *role* yetu sisi kama Wabunge kusimamia mapato ya wananchi wa nchi hii? Nasema pana tatizo la msingi lazima tuli-*address* kama lilivyo. Kuja na kauli ya Serikali ya kusema kwamba watatafuta *external auditor* tena akakague *account* moja tu ya *external debts* hamjatusaidia hata kidogo wala hatujawasaidia Watanzania. Hatujawasaidia Watanzania hata kidogo! Pana matatizo ya msingi lazima tuyakubali. Tuhuma ya dola 800 milioni si ndogo. Sasa wewe ukapate dola 300 tu, inatosha kujenga hoja hapo. Lakini nasema kuwa Serikali haiwezi kufanya hivyo. Mimi nafahamu *sensitivity* ya Benki Kuu, wala usifikiri sifahamu pamoja na kwamba tumeambia hatuna uzoefu, tunao uzoefu kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa *sensitivity* ya Benki Kuu, lakini naelewa vilevile tatizo la wananchi wa Tanzania, maskini wa Mungu wanaokaa juani na kuchuma karafuu wakaanguka, kahawa, wakaumia, korosho na kadhalika halafu mapato yao yatumike ovyo hilo hatuwezi kulikubali hata kidogo hata kama kuna *sensitivity* ya aina gani! Kwa hiyo, sisi tunafikiri bado hakujajengwa hoja. Nasema la msingi hizi taarifa za Serikali zina matatizo sana pamoja na kwamba tunaambiwa sisi hatuna uzoefu.

Mwaka 1965 Bunge hili lilipitisha Sheria, *"An Act to amend the Interim Constitution of the United Republic of Tanzania,"* tarehe 10 Juni, 1965. Hii tarehe 10 Juni imekuwa *assented* na Mheshimiwa Abeid Aman Karume na saini yake hii hapa. *Another law* ya *Exchange Controls Ordinance,* tarehe 10 saini ya Mzee Karume haipo pale lakini imeandikwa kwa *typewriter* Abeid Amani Karume, hii ni sheria kweli? *This government*!

Hii *document* nimeipata kwenye *CD* tuliyopewa na Bunge. *CD* ya Bunge ndiyo nimeikuta hii. Nikikuuliza Mwanasheria Mkuu hii ni sheria kweli ambayo ilikuwa *assented*; hii moja kasaini siku hiyo hiyo moja, Bunge hilo hilo moja limepitisha hiyo; hii moja *assented* na saini yake iko hapa, *I don't know* kama *it is a vague signature anyway*! Hii nyingine saini yake ni *typed*. Halafu mnatuambia nyinyi mnakwenda Benki

Kuu mkatafute watu wengine, tunataka Bunge hili lichunguze kama hali ni hii *how do you trust,* kama kweli Serikali itatuletea kitu kwa uadilifu hapa ndani, *this is the situation*! Kama unataka nizi-*table,* nitazi-*table* hapa.

*(Hapa vielelezo husika vilionyeshwa kwa Wabunge)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezitoa ndani ya *CD* ya Serikali. Ni sheria "A*n Act to amend the Interim Constitution of the United Republic of Tanzania 10th June, 1965*. Imekuwa *assented* na *Vice President of the United Republic of* Tanzania, Mheshimwa Abeid Amani Karume, *Act No. 21 of* 1965. Natoa mfano upungufu uliopo ni mkubwa tu. Sheria Namba 22 *of* 1965 imekuwa *signed* na Mheshimiwa Abeid Amani Karume huyo huyo lakini kwa *typewriter not in his signature*. Na sheria zote nimezipitia, nimekuta kuna *assent* ya Rais kwa mkono, *these are only things I have seen,* ambayo imekuwa *typed*. Bado tunasema kuna matatizo, nasema tuna matatizo ya msingi tunahitaji kuyakabili na moja ni kwamba mimi nimeitoa kwenye *CD* ya Serikali. Wabunge wote tumepewa zile *CD* jamani, sikupewa peke yangu, nendeni mka-*down load* mkatazame mtazikuta tu, sio siri! Lakini nasema kama mmefanya kosa kuzitia mle *it is not our mistake*. Mtu yeyote mwingine aki-*read* ata *read* vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ni kwamba ikiwa tumefikia *level* hii *my own argument* je, tutaamini vipi kama *Central Bank* itakayokabidhiwa *external auditors* hizo taarifa nazo zitachunguzwa na kuletwa kwa usahihi hapa ndani ya Bunge, *that is our argument*. Ikiwa kama *level* ya kisheria tumefikia hapa, *legislature* ambayo itatumika tumefikia hapa, *how could we believe* au *could we trust* kwamba huyo *Auditor* atakayechaguliwa huko ataweza kueleza maudhui ambayo tunayatazama. Kwa maana hiyo mimi nasema muda wangu ulipotea pale lakini unanipigia kengele, sasa bado tunashikilia ni muhimu kwa Bunge hili kuwa na *select committee* kwa sababu maeneo tunayoshutumu ni mengi. Hilo lilikuwa ni jambo moja nilitaka kulisema.

Lingine tuliambiwa kwamba hatujui kusoma vifungu. Namwomba Waziri Mkuu atakapokuja aniambie *employment allowance* ya sh. 475,000,000 mchanganuo ni nini? Akaunti zako zote nyingine nimeona mchanganuo, sikuona kwenye *employment allowance* mchanganuo wa matumizi yake ni nini, naomba utusaidie.

La tatu, tumeambiwa tunausoma mwongozo wa CCM, tunausoma sana. Ukurasa wa 25, unajua utakapokuwa una uzoefu lazima ujitahidi kusoma. Kifungu cha 125(d) kinasema, "Kuongeza kasi ya Wizara za Serikali kuhamia Dodoma kwa kuwa sasa Serikali inajenga nyumba nyingi za kuishi watumishi". Tulikuwa na Wizara tano Dodoma, mwongozo unasema kuongeza kasi, Ilani inasema kuongeza kasi. Sasa ni kuongeza Dodoma ni kuongeza Dar es Salaam? Waziri Mkuu tufafanulie. Ulikuwa na Wizara tano leo unajenga majumba Dar es Salaam, unajenga Ofisi Dar es Salaam, tuambie je, unatekeleza kweli maneno ya Ilani? (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba tena vilevile Waziri Mkuu atakapokuja atuambie juu ya mazungumzo na suala la Zanzibar hasa suala la mafuta. Mlifanya vikao

vingi na mpaka leo hamjaja na *statement* yoyote, tungependa kujua maamuzi yamefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi)*

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya Waziri Mkuu. Ili nisisahau naanza moja kwa moja kwa kuunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nipeleke salamu zangu za rambirambi kwa rafiki yangu Hamisi Chifupa kwa kufiwa na kijana wetu Amina Chifupa, Mwenyezi Mungu amuweke mahali pema peponi. (*Amin)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba historia ya nchi hii iandikwe. Nilizungumza hapa kipindi kile, naomba somo la historia liwe la lazima mpaka Vyuo Vikuu, wenzetu wanafanya hivyo matokeo yake ndiyo haya watu wanakuja kuzungumza hapa kana kwamba nchi hii hivi ilivyo ndivyo ilivyokuwa kabla ya uhuru. Leo ndani humu kuna Maprofessa, Kuna Ma-*Doctor* wenye digrii mbili mbili, moja moja, diploma, nasema hivi kabla ya uhuru tulikuwa hatuna Chuo Kikuu. Chuo Kikuu kile kimejengwa na TANU, Chama cha Mapinduzi. Ukifika mahali unasimama unasema hakuna kilichofanyika katika nchi hii ni dhambi, unawadanganya na kuwaonea Watanzania. Yote hayo yanayofanyika sasa hivi ni kwa sababu ya Sera ya Chama cha Mapinduzi. Tusidanganyane hapa, kupinga ina maana kila kitu ukipinge tu, ukweli kubali. Ndiyo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Dodoma hii ilikuwa vumbi tupu kabla ya uhuru. Dar es Salaam mpaka tunapata uhuru kulikuwa na makuti. Mji mchafu, leo mnazungumzia habari za maghorofa, jamani huo sio upinzani hata kidogo, naomba tusizungumze vitu visivyoeleweka, Chama cha Mapinduzi kinafanya kazi yake. Naomba somo la historia liandikwe, vijana wetu waijue nchi yetu ilikotoka, wenzetu wanafanya hivyo. Ukienda China pale usipofaulu historia Chuo Kikuu hawakuthibitishi kama umepata digrii ili kutunza heshima na nguvu za nchi yao. Nilitaka nianze nalo hili. *(Makofi)*

Kama nilivyoanza kuzungumza niliunga mkono asilimia mia moja hotuba hii ya Waziri Mkuu. Pia napenda kuipongeza Serikali kwa juhudi zake za kueneza elimu katika nchi yetu, nasema hivyo kwa sababu leo hii takribani kila Kata kuna shule ya sekondari. Kule kwangu kuna Kata zifuatazo: Chiwata, Sindano, Lipumbulu, Mnadhira, Mkululu, Mkundi, Marika, Chiungutwa, Mbuyuni, Lulindi, Namalenga, Nanjota, Mchauru, ni Kata mbili tu ambazo hazina shule ya sekondari, Chama cha Mapinduzi, kimefanya kazi yake.

Walionituma ili kuboresha haya wanasema hivi katika kanda ya Kusini kwa sababu tunategemea korosho ili tuweze kuwalipia watoto wetu maana sasa hivi wana mwamko mkubwa wa elimu , watu wa Kusini hawataki mchezo hata kidogo! Wanaomba Wizara ya Elimu itakapokuwa inatoa awamu ya pili ya matokeo basi kwa Kusini kule na

hasa ikizingatia kwamba Mheshimwa Rais amezungumzia upendeleo kwa mikoa ya pembezoni, ukifika mwezi Januari yale majina yote yawe yamekwishatoka ili wananchi wawe na uwezo wa kulipa ada.

Mkichukua katika utaratibu wa kawaida wa mikoa mingine mtaendelea kuwalaumu kwamba hawapendi elimu hata kidogo. Mimi Mbunge wao wa Jimbo la Lulindi, naomba Serikali ilifikirie hili kwamba katika mikoa ya Kusini ukifika mwezi Desemba/Januari majina yote yawe yamekwishatoka ili wananchi wale wawe na uwezo wa kulipa ada na kama mwananchi hana atakwenda kukopa kwa mwenzake aliyeuza korosho ili watoto waende shule, hilo ombi la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwa sababu ya huo huo ukweli wa kuwa pembezoni, wanaomba idadi ya walimu iongezeke katika shule zetu za sekondari, wapelekwe walimu wengi kule. Si haki hata kidogo unakwenda katika shule unakuta mwalim mmoja tu wa sekondari, wanawaombeni sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ongeza idadi ya walimu katika shule za sekondari, kule sasa hivi wana mwamko wa kusoma. Nawaombeni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine wanasema hivi, kwa sababu katika bajeti ya elimu mwaka huu pesa ni nyingi sana, na mimi nawapongeza kwa hilo, wanaomba kuweka mgao ama pesa kwa ajili ya kujenga maabara ili wapatikane wanasayansi. Shule ya Sekondari isipokuwa na maabara haijakamilika bado. Leo hii tuna matatizo ya vijana wanaochukua masomo ya sayansi, kwa hiyo, watu wa jimbo la Lulindi hili wanalifahamu, wanawaombeni sana kwa kuwa pesa zimepatikana nyingi safari hii tunaomba sana sana eneo la maabara mlifikirie.

Nyumba za walimu zijengwe, wao wanasema hawana matatizo hata kidogo, wako tayari kutoa nguvu zao kama walivyotoa katika kujenga shule za sekondari kila Kata na mimi ni shahidi mzuri tu. Nimetembelea karibu shule zote na nguvu za wananchi zimetumika. Kwa hiyo, nawaombeni Wizara ya Elimu haya niliyoyaeleza myazingatie ili na sisi kule Kusini tupate elimu iliyokamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kilimo, kama kawaida, msimu uliopita zao la korosho lilipigwa pigwa mateke, halikununuliwa vizuri. Pamoja na msimamo wa Serikali na wadau wote wa korosho wa kukubaliana bei ya korosho lakini wanunuzi walitupiga chenga. Tunaomba msimu huu hayo yasitokee na yeyote yule ambaye atakiuka kununua korosho kwa bei iliyokubaliwa achukuliwe hatua mara moja ili wananchi wa Kusini waweze kuondoa umaskini. Hapo hapo *export levy* kama alivyozungumza kaka yangu Mkuchika tunaomba mturudishie wenyewe ni 6.5, turudishieni tuitumie wenyewe. Tuna uwezo wa kuagizia mbolea, tunaomba sana kwa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nataka nizungumzie bandari ya Mtwara. Juzi tumezungumza hapa msongamano uliokuwepo katika bandari ya Dar es Salaam na ucheleweshaji wa uondoaji mizigo katika bandari ya Dar es Salaam. Tunasema bandari ya Mtwara ina uwezo mkubwa wa kupunguza msongamano wa kutoa mizigo haraka

haraka kwa faida ya nchi hii, ina uwezo wa kuhudumia shehena ya kawaida tani laki nne kwa mwaka, lakini mpaka hivi sasa tani hizo hazitumiki. Bandari ina uwezo wa kufikia tani 750,000 kwa mwaka kwa kuongeza vifaa vya kupakia na kupakua mizigo, lakini hivi sasa haitumiki hiyo.

Bandari ya Mtwara ina ghati yenye urefu wa mita 385 na kina cha asili *natural tip water* cha mita 9.85, meli mbili kubwa zenye urefu wa mita 175 kila moja inaweza kuhudumiwa ghatini kwa wakati mmoja. Vilevile eneo linalotia nanga lina uwezo wa kuegesha meli sita kwa wakati mmoja zikisubiri nafasi ya kupakuliwa. Hivi tunababaika nini na Dar es Salaam, kila siku Dar es Salaam, kila siku Bandari Salama, bandari hii ipo! Naiomba Serikali itoe kauli rasmi kwamba sasa bandari ya Mtwara itatumika kuondolea mizigo yetu katika nchi yetu hii na itaongeza ufanisi na itaendelea kupendwa na wale ambao wanataka kuikimbia bandari ya Dar es Salaam kwa sababu ya urasimu na ucheleweshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa katika kukuza uchumi naomba sana Serikali za Mitaa ziongezewe fedha ili ziwe na uwezo wa kujenga barabara za vijijini ambako kuna mazao. Kule kwetu wakati mwingine unashindwa kwenda kuchukua korosho kwa sababu barabara ni mbovu, unashindwa kwenda kununua nyanya kwa sababu barabara ni mbovu, unashindwa kwenda kuchukua ufuta, karanga, nyonyo kwa sababu ya barabara mbovu na mazao haya ndiyo yanayoweza kujenga uchumi katika nchi yetu. Naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu ongeza pesa katika Serikali za Mitaa ili wawe na uwezo wa kujenga barabara zitusaidie katika kukuza uchumi kwa kuchukua mazao yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupanga ni kuchagua. Tutakuja kila siku hapa tunalalamika uchumi hauendi kumbe uchumi tunao, mazao tunayo. Tunachokizungumzia hapa ni miundombinu. Tugeuke! Miundombinu hii sio mijini tu, twende vijijini ambako tunalima mazao ambayo sisi yatatusaidia kuuza nje tukapata fedha za kigeni, mazao ambayo yatatusaidia kuanzisha viwanda vidogo vidogo, na kwa maana hiyo yatatusaidia kuongeza ajira katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena , naunga mkono hoja hii asilimia mia moja. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Suleiman Kumchaya. Waheshimiwa Wabunge tutaishia hapa, hapo na jioni tutakuwa na Mhe. *Eng.* Stella Manyanya, Mheshimwia Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma na Waheshimiwa wengine mtajiangalia katika orodha itakayokuwa imebandikwa katika ubao wa matangazo. Kuhusiana na tangazo la kutembelea maonyesho ya biashara Dar es Salaam, kuna neno moja tu sikuliongeza, kwamba mwaliko ule uliosomwa hapa wa Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara ni kwa gharama zako mwenyewe. Basi baada ya hapo naomba kusitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 leo jioni.

*(Saa 07.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Job. Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano kuhusiana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Msemaji wetu wa kwanza ni Mheshimiwa *Eng.* Stella Manyanya, atafuatiwa na Mheshimiwa Bahati Ali Abeid na Mheshimiwa Shoka pia ajiandae.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hotuba hii nzuri sana ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na napenda pia nitumie nafasi hii kumpongeza kwa kuwa inagusa hali halisi ya maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wenzangu kutoa pole kwa familia ya Mzee Chifupa kwa kuondokewa na mtoto wao ambaye alikuwa Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Amina Chifupa.

Mheshimiwa Amina Chifupa ameelezewa sana katika magazeti, katika vyombo mbalimbali na katika uhalisi wa mazingira ninalo wazo kwamba tunao viongozi wengi ambao wamefanya mambo makubwa katika nchi yetu lakini tunakosa historia yao. Mara ya mwisho tulipokuwa katika Mkutano wa Uongozi pale Bagamoyo tukiwa na mama Jitto Ram tulikubaliana kwamba ni vyema sasa kukawa na nafasi ya kuandika historia na vitabu vya kuwaenzi viongozi wetu ambavyo vitakuwa na mafundisho kwa wanaokuja. Kwa hiyo, naomba hilo lifanyiwe kazi ili huyu binti ambaye amefanya kazi vizuri sana tuweze kumuenzi katika kuendeleza kazi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo naomba nizungumzie kidogo suala la familia. Sasa hivi kuna matatizo mengi ya kifamilia yanayoendelea. *Violance* kwa mapana yake, sasa tumejifunza katika nchi yetu hatuna vituo vya *Counselling*. Mtu anapopatwa tatizo anachukuliwa kama ni mtu ambaye hawezi hata akarudi kama mtu wa kawaida. Tunasahau mazuri yote na kuyaweka mbele yale mabaya, matokeo yake tunajikuta tumeharibu familia, tumesababisha matatizo chungu mbovu kutokana na *pressure* zinazotoka nje ya familia.

Kwa hiyo, naomba suala hilo litiliwe mkazo na tuweze kuona ni jinsi gani tunanusuru familia zetu katika kuziwekea maeneo ambayo wale ambao wanakuwa wamepata matatizo ya kifamilia wanaweza wakapata *counselling* na hivi kufanya nyumba zao kuwa imara badala tu ya kuishi kwa kutegemea redio mbao mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu ametembelea Mkoa wa Ruvuma siku ya Uwekezaji, wajasiriamali, wale wachimbaji wadogo wadogo, walikuwa wamemwomba namna ya kuweza kuwasaidia hususan kwa upande wa nyenzo

na jinsi ya kuendeleza shughuli zao na masoko. Kazi hiyo alikuwa ameikasimu kwa marehemu Mzee Akukweti , bahati mbaya ametutoka Mungu amrehemu. Lakini pia Wabunge wa Ruvuma tumekuwa tukifuatalia na tumeona kwamba matatizo hayapo Mkoa wa Ruvuma tu yapo pia hata katika maeneo mengine. Lakini kuna shirika letu la *STAMICO* ambalo lina wataalamu wa kutosha sasa hivi baada ya shirika hilo kuwepo katika msururu wa kufungwa yaani *specified companies* kwamba wataalamu wengi wapo kwenye likizo zisizo na malipo lakini Shirika hili lingeweza kuwa ni mwavuli wa hawa wachimbaji wadogo wadogo.

Pia kulikuwa na Ripoti ya Dr. Kipokola ambayo ilikuwa imetathimini sera ya madini pamoja na hatima ya *STAMICO*. *STAMICO* itaweza kusaidia sana kwa sababu kwanza mpaka sasa kuna *raw materials* nyingi tunazoziagiza nje ambazo zingeweza kuwa *provided* na hawa wajasiriamali wadogo wadogo. Kwa mfano, maeneo ya Mtwara pale kuna *limestone* na wakati huo huo kuna gesi ambayo inaweza kuzalisha mpaka megawati 300. *limestone* inaweza ikatengeneza *cement* kwa kuweka kiwanda eneo lilelile. Lakini maeneo ya Kilwa na maeneo mengine kunapatikana *gypsum* ambayo ni *raw material* kwa ajili ya *cement*. Kwa hiyo, naomba sana *STAMICO* iangaliwe upya ili tuweze kuitumia *STAMICO* kama chombo cha kuweza kuendeleza hawa wachimbaji wetu wadogo wadogo kwa kuwakopesha au kuwapa mitambo ya kuchongea baadala ya kila mmoja ku-*invest* kwenye mitambo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa si mwingi wa subira, kama sitatoa shukrani za dhati Serikali kupeleka umeme wa gridi Mkoa wa Ruvuma. Kwa mara ya kwanza katika miaka 45 baada ya uhuru tunategemea kupata umeme wa gridi ya Makambako-Songea. Kwenye bajeti nimeona tuna shilingi bilioni 9.5, fedha za kigeni lakini wakati huo huo hata barabara sasa hivi ya Masasi-Tunduru-Songea-Mbamba *Bay* bado ina fedha za kutosha hata kama haitakuwa lami lakini kama hawa wenzetu watafanya kazi vizuri itapitika kwa kutumia hiyo lami nyekundu ambayo ni kifusi.

Napenda kutoa angalizo kwa Serikali kuwa Mkoa wa Ruvuma ni Mkoa wenye rasilimali nyingi sana, ardhi yake ni nzuri, tuna madini mengi kama dhahabu, *gemstone* za aina mbalimbali kama *Alexandria* na mambo mengine mengi. Lakini siku zote tumekuwa nyuma kidogo kwa sababu ya kukosa miundombinu. Katika *investment report* ya mwaka 2004 inaonyesha wazi *investment* katika Mkoa wa Ruvuma ni kidogo sana ukilinganisha na mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Shinyanga, Arusha na Kilimanjaro. Kwa hiyo, tunaomba sana kwa wenzetu wawekezaji waelewe kwamba tunavyozungumza ni kwamba tayari matayarisho ya kuwekeza huko yapo isiwe tena mchezo wa yai na kuku kipi kimeanza. Umeme unaenda na ninyi njooni muanze ku-*book,* sehemu ya kuwekeza hakika Ruvuma ni mahali pazuri kwa kuwekeza.(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niongelee kuhusu kuwashirikisha wananchi katika shughuli mbalimbali za maendeleo na kiuchumi. Katika ukurasa wa 68 kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, amezungumza sentensi ifuatayo, nanukuu: *"If you want a brighter view of life help someone else to find the solution of his/her problem"* Na mimi naongeza, nasema hivi, *Give a man a fish and you feed him for a day. Teach him how to fish and you feed him for a life time."* (*Makofi*)

Hiyo nimeinukuu kutoka kwa *Mr. Steven R. Covey* kwenye kitabu chake cha *Principle Centred Leadership.* Lakini pia inaongezwa kwenye vitabu vya *Better Yourself.* Nasema hivi, kuna msemo unasema, *The power of positive thinking* na kuna msemo mwingine unasema, *The power of Appreciation* na msemo mwingine unasema *Create Powers within ourselves*. Nasema hivyo kwa sababu tumekuwa na hali ya kubeza yale ambayo tumefanikiwa. Tukisikiliza upande wa pili unakuta wanasema nyinyi mnawaambia wajenge, wananchi wanapoteza nguvu zao, hivi hao watoto ni wa nani? Watoto ni wetu sisi wenyewe, sasa unataka Serikali ifanye kazi peke yake kwa sababu zipi?

Tumeona kabisa kwamba ongezeko letu la watu ni kubwa sana ikilinganishwa na mipango yetu. Sasa tunataka rasilimali watu ambao ndio wengi katika nchi hii ilale isitumike inavyostahili! Tunaanza kuleta maneno ya fitina tuhujumu, ni uhujumu ambayo ni mbaya sana kwa sababu ni hujuma ya kisaikolojia; ni hujuma mbaya kuliko hujuma ya pesa kwa sababu inadumu kizazi hadi kizazi, inaleta chuki miongoni mwetu. Naomba mbadilike muwe na mtazamo ambao unalenga katika kuwezesha kumfanya mtu atambue rasilimali zinazomzunguka aweze kuzitumia na kuzigeuza kuwa utajiri. Tusiwadanganye kwa kuwapa pipi kwa kuwadanganya kwamba tutawapa ada za watoto wakati hatuwawezeshi ku-*articulate resources* walizonazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusisitiza hilo, kwa sababu wenzetu mnasoma sana, sisi tunasoma kidogo, tunachukua yale tu yanayotusaidia. Vilevile Bwana *Covey* anasema hivi, *"Most People are turned off by motivational speakers who have nothing more than to share than entertaining stories mingled with motherhood and apple_pie platitudes.* Akaendelea akisema yaani hawa watu wetu sasa, "*They want more substance; they want process. They want more than asprin and a Band-Aid for acute pain. They want to solve their chronic problems and achieve long-term results."* Kwa hiyo, tuelewe kama kweli tuna nia ya kuwasaidia wananchi wetu sio tu kwa kuwapa *aspirin*, sio tu kwa kusema kwamba basi tu-*charge* kodi hivi au tuachane na ku-*charge* kwenye mafuta. Mafuta ndiyo njia pekee ya kumshirikisha kila mwananchi kuweza kulipia gharama zinazoongezeka.

Hakuna mtu wa kusema mimi ni maskini, maskini nani anapenda umaskini? Kwa nini wewe unang'ng'ania kumwita mwenzako maskini, mwache mtu atambue mwenyewe. Lakini vilevile nasema kwamba kuna suala la kukataa makongamano/warsha ninyi mnataka kuwafungia wenzetu wafanye kazi bila kujua kinachoendelea katika dunia hii. Narudia tena kwa maneno kiasi maana yake mjifunze kutoka kwa wengine.

Huyu huyu anasema , tena yeye ni mwalimu, alikuwa anafundisha watu sasa walipoitwa siku hiyo kwenye warsha watu wakawa wanafikiria wataambiwa kitu gani. Anasema hivi, *"I once spoke to a group of senior executives at a training conference and discovered that they were bitter because the CEO had forced them to come and sit for four days to listen to a bunch of abstract thoughts. They were part of paternalistic, dependent culture that saw training as an expense, not an investment. Their organization managed people as things."* Kwa hiyo, hatuwezi kuendelea kuwasimimia watu wetu au

kuongoza watu wetu kama vitu. Lazima tuwasimamie kama watu wanaoelewa kwa kuwahitaji na wenyewe kuweza kutoa mchango ambao utasaidia nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu pia nimeuweka pia kwa maandishi na ni mrefu sana. Kwa hiyo, kwa sasa nataka nikufahamishe kwamba nimechangia pia katika suala la uanzishwaji wa miji ambao nimeona ni jambo zuri. *CDF* nimeona ni jambo zuri lakini pia naomba SUMATRA isiwaachie wafanyabiashara wakaendelea kupanga bei zao. Tuombe watufanyie kazi ili waweze kutangaza bei ya mafuta ama sivyo hawa wenzetu watakuwa wanawatumia kwa kuwaambia kwamba mnaona bei zimepanda! Tufike mahali lazima tusimamie ili bei zetu ziweze kuwa zile zinazowezesha kutokana na gharama halisi ya uendeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nasema kwamba Chama Tawala kina nia njema na watu wake na humu si sehemu ya kufanyia kampeni ila mkiziomba tunayo majibu lakini tusubiri mwaka 2010. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi kunipa nafasi hii kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kabla ya yote na mimi niungane na wenzangu kwa kutoa pole kwa familia ya Mheshimiwa Amina Chifupa na Mwenyezi Mungu atawajalia Wazee wake aweze kuwapa subira kwa kipindi hiki kigumu na pia Mwenyezi Mungu aijalie Roho ya Mheshimiwa Chifupa ailaze mahala pema peponi Amin!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na watalaamu wake ambao wameandaa hotuba hii nzuri yenye mwelekeo wa maendeleo kwa taifa letu. Mimi sina tatizo hata kidogo na hotuba hii lakini mchango wangu niuelekeze kwenye wastaafu. Kama tunavyojua watanzania walio wengi wanapoajiriwa Serikalini au wanapoajiriwa kwenye sekta mbalimbali binafsi hufanya kazi kubwa ya kuhakikisha kuwa wanaleta maendeleo kwa uzalendo mkubwa katika nchi yao. Lakini tatizo linakuja mara tu baada ya kustaafu baadhi ya wananchi ambao hupata taabu sana kwa kupata kiinua mgongo chao kwani huchelewa mpaka kufikia miaka mitatu, mwananchi wa kipato au ngazi ya chini haijapata kiinua mgongo chake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi nina mfano tosha wa askari ambaye aliniripotia na baadae nikamwona Naibu Waziri wa Usalama wa Raia ili aweze kumsaidia askari huyu kupata kiinua mgongo chake baada ya kukaa muda mrefu bila ya mafanikio. Lakini jitihada hizi hazikuweza kuzaa matunda kwani mpaka leo mstaafu huyu ana miaka mitatu hajalipwa kiinua mgongo chake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninavyojua mfanyakazi anapokaribia kustaafu ndani ya miezi sita, basi hufanyiwa taratibu zote ambazo zinapaswa kufanywa kwa mstaafu ili anapostaafu kusiwe na kufuatilia, panda shuka bila ya kuzaa matunda. Nasema hivi kwa kuwa tunawapa kazi kubwa au tunawapa mateso makubwa wastaafu wanapotoka Zanzibar kuja Dar es Salaam na kufuatilia mafao yao mara kwa mara na wakati huo wanakuwa hawana kipato chochote kwani mfanyakazi wa ngazi ya chini

anakuwa hana mradi mbadala baada ya kustaafu kuweza kumpatia mafao au kumpatia kipato chochote kile cha kumwendeleza maisha yake.(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu aliangalie hili ili kama wapo wastaafu wengine kama huyu ambaye ninamjua mimi waweze kupatiwa mafao yao au viinua mgongo vyao ili waweze kujikidhi haja ya maisha yao ya kila siku kwani Serikali inapomcheleweshea kumpa mafao mstaafu inamsababishia matatizo makubwa yeye na familia yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine niuelekeze kwenye *TASAF*. Sina budi kutoa shukrani kwa *TASAF II* kule Zanzibar. Lakini pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa Watendaji wa Mfuko huu; wanafanya kazi kubwa wakishirikiana na wananchi kuibua miradi lakini pia miradi hii inatekelezeka na tunaiona na mafanikio makubwa tumeyapata kwani miradi hii inaonekana wazi wazi kuwa kweli ina azma ya kumkomboa mwananchi na kumtoa kwenye usingizi mzito ambao tulikuwa nao.Lakini kama nilivyosema sina mchango mkubwa kwenye hotuba hii, kwani hotuba hii ni nzuri. Nataka nimuulize Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuna uwezekano mkubwa wa kujenga ofisi zisizopungua 40 za Wabunge je, ofisi hizi zitafika mpaka Zanzibar na kama zitafika basi zitakuwa ngapi na zinaweza kufika kumi? Kwa kweli nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jinsi anavyofanya kazi kubwa ya kuhakikisha kuwa wananchi wa Tanzania wanapata maendeleo makubwa Awamu hii ya Ari Mpya, Kasi Mpya na Nguvu Mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, sina tatizo hata kidogo na Hotuba ya Waziri Mkuu, naomba sasa niiunge mkono kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante.(*Makofi*)

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi jioni hii niweze kutoa maoni yangu japo kidogo. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia tukiwa wazima kufikia jioni hii sote hapa katika Bunge. Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, vilevile napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru na wewe mwenyewe kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuongea.

Baada ya shukrani hizo, vile vile napenda nichukue fursa hii nitoe pole kwa kifo cha Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia ambacho kilitokea juzi ambapo kifo hiki kimetugusa Wabunge wote. Kwa kweli Mheshimiwa Chifupa alikuwa ni mtu wa watu wote hakujiweka wa mtu mmoja au baadhi ya vikundi. Kwa kweli tunamshukuru sana na Mwenyenzi Mungu amlipe kheri na amjalie aingie katika pepo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti baada ya hapo, na mimi napenda nichukue fursa hii kuwapongeza viongozi wangu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed pamoja na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, kwa maoni yao ya kutaka kuundwa kwa Tume ili tuweze kuchunguza namna fedha za Serikali kwenye Benki Kuu zinavyotumiwa na sikubaliani na kuwa tulete *External Auditor* kutoka nje aje atufanyie mahesabu yetu. Kwa hiyo, mimi hapa nawaunga mkono viongozi wangu.(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo napenda nichangie kwenye posho za Madiwani na hapa nimnukuu Mheshimiwa Waziri Mkuu, natofautiana naye kidogo tu kwa mpango. Mheshimiwa Waziri Mkuu katika Hotuba yake anasema: "Vilevile kutokana na majukumu mengi waliyonayo Waheshimiwa Madiwani Serikali imekubali kuongeza posho zao kutoka shilingi 30,000 hadi shilingi 60,000 kwa mwezi kulingana na uwezo wa Halmashauri." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu, mimi sikatai posho hizi lakini naona ni ndogo kwa Waheshimiwa Madiwani. Wewe mwenyewe umesema wana majukumu mengi. Hivi kwa nini Serikali yetu inaona taabu kuwaongezea posho nzuri Waheshimiwa Madiwani ambao huwa tunawatumia kwa shughuli zetu. Mnasema kuwa Madiwani injini ya maendeleo ya nchi na sisi Wabunge tunapokuwa hatupo, tupo huku Bungeni nafasi zetu zile tunawaachia Waheshimiwa Madiwani na kazi zetu nyingi wanatufanyia kule.

Sasa kunakuwa na uzito gani kuwapa fedha nzuri Waheshimiwa Madiwani na badala yake tunatoa fedha nyingine. Nitatoa mfano mdogo. Kuna fedha nyingi sana zimetengwa kwenye fungu ambalo ni la Idara moja, zaidi ya shilingi bilioni 20 kwa matumizi ya kawaida, lakini tunaona shida kuwatengea fedha za kutosha Waheshimiwa Madiwani. Hili nasema kwa uhakika kwa sababu nina takwimu na hilo fungu ninalolisemea nalijiua, napendekeza Waheshimiwa Madiwani na wao tuwaangalie tusijiangalie sisi Wabunge na wafanyakazi wengine tu, na wao ni wafanyakazi wenzetu. Tunasema kuwa Madiwani si waajiriwa lakini tunawaajiri watu wengine.(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena nimnukuu Mheshimiwa Waziri Mkuu sehemu hiyo hiyo. "Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitenga fedha za kuwalipa mishahara maafisa watendaji wa vijiji na mitaa. Hadi mwezi Desemba 2006, Maafisa Watendaji wa Vijiji wapatao 9,716 kati ya Watendaji wa vijiji 10,392 ambao wanapaswa kuwepo kulingana na idadi ya vijiji walilipwa na Watendaji wa Mitaa 1,512 kati ya Watendaji 1,755 nao walilipwa. Aidha, wale ambao bado hawajalipwa taratibu za ajira zao zinakamilishwa." Mwisho wa kunukuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa tunaajiri mpaka Watendaji wa Vijiji lakini tunawaacha nyuma Waheshimiwa Madiwani. Sasa mimi nasema Madiwani hatuwatendei haki, siku zote tunawasifu tu lakini haki hatuwatendei. Sasa mimi napendekeza kuwa Waheshimiwa Madiwani japo hatutaki kuwaajiri kama wafanyakazi wengine lakini tuwape posho nzuri. Halafu hiyo posho yenyewe nayo inategemea ukusanyaji wa Halmashauri, ikiwa Halmashauri haina uwezo wa kukusanya ina maana madiwani pale watakuwa hawapati posho zao. Sasa mimi nasema Madiwani hatuwatendei haki na Mwenyezi Mungu huko mbele atatuuliza Wabunge wote kwa sababu ni sote kwa jumla tukiamua kuwatetea Madiwani hapa Serikali nayo itatusikiliza. Kwa sababu mambo mengi tunayoyasimamia nayo Serikali inatusikiliza. Kwa hiyo nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuungane na wenzetu Madiwani na wao angalau wapate posho nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea zaidi naomba nimnukuu tena Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusiana na ofisi za Wabunge. Tunatofautiana wala hatuhoji kwa ubaya. Mheshimiwa Waziri Mkuu anasema, "Serikali inatambua umuhimu wa Waheshimiwa Wabunge kuwa na ofisi zenye hadhi kwenye Majimbo yao ya Uchaguzi kwa kuanzia

Serikali imetenga fedha zitakazowezesha kujenga ofisi 40 za Waheshimiwa Wabunge kwa vile Serikali ina mtandao wa ngazi mbalimbali hadi vijijini jukumu la kujenga na kutunza Ofisi hizo litakuwa ni la Halmashauri za Wilaya." Hapa napo natofautiana naye tena. Ni kweli jambo ni zuri lakini sisi Wabunge ni wa pande mbili. Sasa sisi Wabunge wa Zanzibar ukitenga fedha ukisema zijengwe ofisi 40 kwa njia ya Halmashauri ya Wilaya ina maana sisi Wabunge kutoka Zanzibar umetutenga hujatuingiza kwenye fungu hili. Sasa mimi natoa pendekezo kuwa ofisi zijengwe hizo hizo 40 lakini fedha iliyotengwa ni shilingi bilioni moja mimi naifahamu. Sasa hizi shilingi bilioni moja tugawiwe na sisi wa Zanzibar, tujengewe ofisi, msijenge huku bara kwa sababu nchi hii ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa hiyo, napendekeza kuwa ofisi 30 zijengwe huku bara na 10 zijengwe Zanzibar. Zanzibar ofisi 6 zijengwe Unguja na 8 zijengwe Pemba. Kila Wilaya ipate Ofisi yake, na hizi fedha zihamishwe kwenye Halmashauri zipelekwe kwenye mfuko wa Bunge. Sasa mnapotuambia kuwa Waheshimiwa Wabunge kutoka Zanzibar tujengewe ofisi kutoka Ofisa ya Waziri Kiongozi mnakwepa majukumu yenu!

Sisi hatuwezi kujengewa ofisi kutoka Ofisi ya Waziri Kiongozi kwa sababu sisi mwajiri wetu ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hatufanyi kazi kwenye ofisi ya Waziri Kiongozi, sasa mnapotuambia tujengewe kutoka Ofisi ya Waziri Kiongozi, hatujengewi! Kwa hiyo, tunaomba na sisi Wabunge kutoka Zanzibar tujengewe ofisi na fedha hii ya mwanzo iliyoanza kutoka na sisi tupewe tuanze kujengewa ofisi. Na mkiamua kujenga sisi wa Zanzibar tunaweza kupata ofisi mara moja. Mara hii mkitujengea kumi na mara nyingine tena mkiweka kumi na mara nyingine tena kumi baada ya muda mchache tutakuwa tumeshamaliza. Sasa na ninyi huku Bara mtaendelea kuongeza ofisi zenu na wakati huo huo Wabunge wengi huku bara ofisi wanazo. Lakini sisi Zanzibar hatuna ofisi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba hili uliangalie tena. (*Makofi*)

Vilevile nikiendelea kuchangia, sasa nitaingia katika sehemu ya maafa. Sehemu ya maafa sisi Wapemba mnatutenga, tunapokuwa na maafa mnatuacha nyuma. Nina mifano mingi Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba mnisikilieze. Hivi karibuni lilitokea tatizo katika Jimbo la Mheshimiwa Mnyaa. Alipata matatizo, kwenye Jimbo lake ilinyesha mvua kali na upepo ukasababisha baadhi ya mazao kuharibika, na akaandika barua hapa kuomba asaidiwe. Lakini hakupata msaada na barua hiyo ilikuwa kwenye ofisi yako Mheshimiwa Waziri Mkuu hata kumjibu hukumjibu. Yaani ungemjibu ukasema kuwa suala hili linatoka Zanzibar, ukalijibu tungesema angalau umemtendea haki lakini hata kujibu hukujibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuondoke hapo, njoo kwangu mimi mwenyewe ninayezungumza. Jimboni kwangu kulitokea matatizo ya njaa, na njaa siyo kitu cha ajabu inaweza kutokea sehemu yoyote. Katika Ulimwengu, tunasema duniani si peponi, wakati wowote mtu anaweza akapatwa na tatizo. Kwa hiyo, Jimbo langu lilifikwa na njaa na baada ya kufikwa na njaa, tukatoa taarifa kwenye vyombo vya habari.

Baada ya kutoa taarifa kwenye vyombo vya habari, Mkuu wa Mkoa kule kwetu Kaskazini Pemba, alisema kuwa hawa hawana njaa, isipokuwa tatizo lao ni siasa tu! Naomba mnisikilize vizuri! Tukaambiwa kuwa ni tatizo la siasa, lakini wakati huo huo sisi tunaambiwa kuwa tatizo letu ni siasa, lakini watu wake wa CCM akawa anawapenyezea penyezea chakula kidogo kidogo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema tuna matatizo, mtusikilize. Mimi Mbunge kwa kupitia Kiongozi wangu wa Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, tulimwandikia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tukamwomba awasaidie watu wetu wale waliokuwa na njaa na kwa sababu yeye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hahusiki na sehemu moja tu, ni wa wote, tukamwomba atusaidie chakula kwa wale waliokuwa na matatizo. Lakini kwa masikitiko makubwa, miezi mitatu hatukujibiwa barua ile.

Baada ya kuwa sijajibiwa, nilipokuja nikaonana na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Maafa na Kampeni dhidi ya UKIMWI, Mheshimiwa Dr. Luka J. Siyame, nikaonana naye na nikamwomba atusaidie. Akaniambia Mheshimiwa subiri nawasiliana na Waziri Mkuu ili twende tukaone hiyo hali". Nikamwambia, "sawa, nipo tayari angalau twende tukaione tu ile hali tujue vile ilivyo, japo tusifanye chochote, lakini ile hali tuijue vile ilivyo". Tukakubaliana pale, tukakaa wiki mbili Dar es salaam, sikupata majibu. Tukatoka tukaja hapa, nikamwambia "Mheshimiwa vipi lile suala tumefikia wapi?" Akaniambia wewe vuta subira tu, unajua tena Mawaziri wako kwa kuvuta subira! Nikaendelea kuvuta subira, mpaka mwisho kipindi kile cha Bunge kikaisha, subira ikamalizwa, sikupata msaada wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasema kuwa mnatutelekeza tunapokuwa na matatizo. Hiyo Ofisi yako mwenyewe, sasa leo nataka nikuulize Mheshimiwa Waziri Mkuu, hivi ni wewe au ni Mheshimiwa Siyame aliyekuwa akinipiga danadana? Mimi nataka nijue tu! Mheshimiwa mmoja hapa leo alisema kuwa ili tuweke kumbukumbu, na mimi nataka tuweke kumbukumbu nijue wewe ndiye uliyewakatalia wale Wapemba waliokuwa na njaa au ni Naibu Waziri wako? Hilo nataka unijibu, ikiwa hukunijibu, tutashikana kwenye vifungu, *Inshallah*! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea na mambo hayo ya maafa, tarehe 14, kuna jamaa zetu Wapemba walitoka Pemba kwenda Tanga, bahati mbaya walizama na chombo. Chombo kiligonga mwamba, kikatoboka, kikaingia maji. Wakatoa taarifa, kwa bahati nzuri walikuwa na simu wakapiga simu Tanga. Walipopiga simu Tanga kuwaambia jamaa zao, "jamani tumepatwa na matatizo!" Wakapeleka taarifa Polisi na o wakasema hawana mafuta, wale jamaa zao wakasaidia kupata mafuta. Wakatoka na chombo, walipofika mbele wakaona kuna giza, wakasema, "bwana maboya hayawaki na kumekwishakuwa usiku," kwa hiyo, hatuwezi kwenda kule. Hawakwenda, wakawaacha watu kule baharini wakazama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nasema ingelikuwa ni watu wengine, lazima wangesimamiwa watu wale wangekwenda. Lakini kwa sababu ni Wapemba, walinyamaza kimya, wakarudi majumbani wakalala mpaka wakatoka Wapemba

wenyewe, wakaenda wakawafuata jamaa zao. Walipofika, tayari baadhi ya watu walikuwa wamekwishafariki. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hiyo, na sisi Wapemba ni wenzenu, msitutenge! Na haya yote yanayosababisha kuwa sisi Wapemba tunachaguana, ni kututenga tu, ingekuwa hamtutengi, na sisi ingekuwa hawatuwatengi!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu! Kanuni ya 50. Mheshimiwa Mbunge, jambo analolizungumza hapa, naona kwa kweli siyo la kweli, ni dhana na hana uthibitisho. Hakuna mtu yeyote na wala Serikali haiwezi kuwatenga Wapemba na sisi wenyewe katika Serikali na mimi binafsi nimeolewa huko Pemba. Kwa hiyo, hatuwezi kuwatenga Wapemba, ni Watanzania kama Watanzania wengine. Naomba Mheshimiwa Mbunge afute kauli yake kwa sababu kwa kweli inaleta dhana mbaya katika Serikali yetu ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru Mheshimiwa Waziri wa Nchi. Ni kweli kabisa, Serikali hii haimtengi mtu yeyote, hata Waheshimiwa Wabunge kutoka Pemba mtashuhudia hili. Mheshimiwa Shoka, ni fursa kwako kuweka sawa sawa masuala ya Muungano.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninayoeleza yote ni ya kweli. Kama mnaona si ya kweli mnataka ushahidi mwingine, mimi kusema nimeishayasema. Kwa hiyo, nafuta lakini mmekwishayasikia. Naendelea na sehemu nyingine; naendelea na suala la Tume ya Kurekebisha Sheria.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shoka! Kaa kidogo! Maneno uliyoyazungumza ni mazito sana ya jamii moja ya nchi yetu kuonekana ikitengwa kana kwamba katika nchi hii kuna ubaguzi! Kwa hiyo, kama umeyafuta, yafute, lakini usiweke tena ujanja ujanja, vinginevyo nitakutaka ukae moja kwa moja! Nafasi yako, Mheshimiwa Shoka!

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafuta! Lakini, si wameishasikia! Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelelea kuhusu Tume ya Kurekebisha Sheria. Tume ya Kurekebisha Sheria ina sheria nyingi ambazo tayari imekwishazifanyia kazi, lakini hazijaletwa hapa Bungeni ili tukazifanyie marekebisho zikawa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nasema hivi, huo uzalendo tunaoutaka ni pamoja na kuwawekea wananchi wetu sheria nzuri. Kuna sheria kama Sheria ya Ndoa, Sheria ya Mirathi, kila siku zinapigiwa kelele kwenye redio na ziko tayari. Tayari kwenye Tume ya Kurekebisha Sheria, zilisharekebishwa, sijui zinakwama wapi baina ya Wizara ya Katiba na Sheria au kwenye Baraza la Mawaziri! Huko ndiko kunakokwamisha mambo ya sheria. Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nasema wakati umefika, mjitayarishe kufanya kazi haraka haraka, ile sera yenu mliyosema “Ari Mpya” na “Kasi Mpya”, muifanye humu, tuione! Msituambie kwa maeneo tu! Kwa hiyo, nategemea kuwa Sheria hii ya Mirathi pamoja na Sheria ya Ndoa tutazipata haraka iwezekanavyo.

Naendelea! Kuna jambo ambalo nataka nilizungumze, sijui kama nitapata wakati. Jambo lenyewe ni kuhusu kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi Mkuu Tanzania Bara. Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili limekuwa la muda mrefu, wananchi wanalihitaji kwa muda mrefu, lakini naona mpaka leo halijamalizwa. Sasa sijui ni lini suala hili litakamilishwa? Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, mwaka jana alipokuwa akizungumza kwenye bajeti yake, alituahidi hapa na tulikuwa na tamaa. Nilikuwa nimnukuu, lakini maneno yake ni marefu na muda sina tena. Alisema kuwa suala hili limo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi na ni kweli. Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaomba tupatiwe jawabu!

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe shukrani kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia jioni ya leo. Lakini pia nami nianze kwa kutoa rambi rambi zangu kwa familia ya Marehemu Mbunge mwenzetu, Amina Chifupa. Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. Amina!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo naomba nianze kwa jambo moja. Lipo jambo hapa linasemwa sana, hili jambo la *BoT*. Mimi leo nimeamua niseme ambavyo nimefarijika sana na Serikali leo ilipotoa kauli hapa Bungeni. Waziri wa Fedha amesisitiza kwa mara ya pili. Alisema wakati wa bajeti na leo amerudia tena. Hili mimi leo limenipa faraja kubwa na nitasema ni kwa nini. Kwanza, nimefarijika kwa sababu huu ni utamaduni mpya wa kufanya *scrutiny*, Serikali kujichunguza. Utamaduni huu ni wa kujivunia. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ukienda vizuri, Mheshimiwa Rais alipopata Ripoti ya *Auditor General* aliileta, watu wakaijadili tena kwa uwazi mpaka kwenye Halmashauri zetu. Maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba huyu ni Rais ambaye yuko tayari Serikali yake ijadiliwe inavyofanya mambo yake. Huu ni uwazi wa hali ya juu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili suala la *BoT*, Serikali kwa *standard* ile ile imeona kuna jambo, imeamua kulipeleka kwa *Auditor General* wetu ambaye ni *Independent*. Sijui kama wenzetu wanalifahamu! Na *Auditor General* ameamua kutafuta Mshirika wake ili wasaidiane kulichunguza jambo hili. Jambo hili mimi kwangu ni faraja sana. Maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba ili kuwe na uwazi na ukweli, na wameamua kulipeleka likafanyiwe uchunguzi hata kabla ya Wabunge hatujaongea hapa ndani. Kwa hiyo, Serikali ilitambua, ikaanza yenyewe kulifanyia kazi. Lakini wenzetu wamekuja wanataka kudhani wao wanaweza wakaifundisha Serikali yetu kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, nawaeleza ndugu zangu kwamba Serikali inachotaka kufanya hapa ni kutaka kuona *justice* inatendeka. Lakini, suala la pili ambalo ni matokeo ya hizo ripoti: Kwanza, ripoti yenyewe kwa kushirikisha *International Firms* ambazo ziko *credible*, maana yake Ripoti hiyo itakuwa *credible*. Itakuwa *credible* kwetu, itakuwa *credible* kwa wananchi, itakuwa *credible* kwa *Development Partners* wetu kwa sababu suala la *BoT* ni *very sensitive, unless* wenzetu hawalifahamu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la muhimu zaidi ambalo linanipa faraja zaidi ni kwamba kwa mara ya kwanza Serikali imeamua yenyewe kusema *we have nothing to hide*, watu waje wachunguze! Sasa wenzetu wanakuja hapa, wanasema tuunde *select committee*, ya nini? Serikali imekwishaanza kuchunguza *unless* mniambie hiyo Ripoti itakapokuja kwamba hatuikubali *then* tujadili suala la *select committee*. Tunalijadili leo la nini? Linafanyiwa kazi tayari! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine muhimu zaidi ambalo ningependa ndugu zetu tuelewane, wenzetu wa Upinzani kila wanaposimama hapa ndani anaongea akim-*refer Auditor General*. Kila wanapotaka kuongea ubaya wa Serikali, wanam-*refer Auditor General*. Lakini leo Mheshimiwa Hamad Rashid amesema na nitamnukuu hapa kwamba hizo *Report* za *Auditor General* ambazo zimei-*clear BoT* hazikubali. Lakini zile *Report* zinazosema Serikali imekosea hapa, wanazikubali. Sasa hizi ni *two paradox!* Mimi ningependa watuambie wao sasa wanamkubali yupi, maana huyu *Auditor General* ambaye atasema Serikali hapa kulikuwa hakuna *Voucher*, ndiye watam-*refer* hapa.

Lakini *Auditor General* akisema hesabu za *BoT* ni nzuri, hawamkubali kwa sababu ha-*suit their interest!* Sidhani kama ndiko tunaenda huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka niwaambie jambo moja, baada ya *Enlon saga* ya Marekani, hakuna *Auditor* yeyote anayeweza kuleta *Report* ambayo hawezi kuitetea, hayupo! *unless* hii *profession* hatuifahamu vizuri. Lakini nataka niwaambie *Report* ya *Auditor* yeyote kwa sasa, kwa sababu ukileta *Report* ambayo huwezi kuitetea, kesho unafutwa kwenye hii *Industry*! Na mimi nikataka kusema wenzetu tunaelewana hili? Na haya mambo ya mikataba, mikataba yote, sijui kama wenzangu wanajua!

Mkataba wa ujenzi wa Barabara, ukisha u-*peg* kwenye *Dollar*, haiwezekani mwisho wa siku ulipe hela ile ile, haiwezekani! Sababu ziko *very clear*, kuna *Inflation*, kuna *exchange rate variation*, hizo zipo tu. Katika Mikataba ipo! Sasa sijui wenzetu wanatumia *clause* zipi? Kwa hiyo, nataka kusema jamani ninachoomba kwa Serikali ifanye kazi yake, ilete ile *Report* tuione! Hili ndilo mimi naiomba Serikali *otherwise* mimi siyo muumini wa kuunda hiyo *select committee*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa na mimi niweze kuchangia kwenye bajeti ya Waziri Mkuu. Tumesema tunataka kupeleka madaraka Wilayani. Mimi ningeomba sana tulifikirie upya suala la Elimu na Afya. Suala la Elimu, ni vizuri liwe na *custodian* mmoja. Waziri wa Elimu awe *responsible* kwa Elimu katika nchi hii. Lakini ukiniambia Waziri wa Elimu anafanya hapa, nusu watafanya watu wa TAMISEMI, kwa vyovyote vile hatuwezi kwenda pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba Waziri wa Afya linapokuja suala linalohusu afya la nchi hii, tujue tunamkamata nani, tujue tuna-*measure performance* ya huyo mtu namna gani. Huu ndio ushauri wangu, ningeomba jambo hili tuliangalie namna ya kuliweka pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nataka nichangie, kuna suala la kitu kinaitwa *Revenue Ratio v/s GDP*. Ningeomba Serikali na kwa kweli Waziri wa Fedha ametuambia juzi. Ni matumaini yetu mwaka huu wa fedha tutakusanya *18% Ratio* ya *Revenue* yetu *v/s our GDP*. Hilo ni jambo zuri sana *towards* kwenda kujitegemea, na hilo kwa kweli nampongeza sana Waziri wa Fedha. Sasa ningeomba Waziri wa Mipango aje na Mipango yetu vizuri ambayo ajue *Investment* zetu tunazielekeza wapi sasa ili tuweze ku-*meet* hiyo *target*. Ikiwezekana ile *Revenue Ratio* yetu iondoke kwenye asilimia 18 mpaka 30, na tunaliweza hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu katika bajeti yake, ukurasa wa 65 ameongelea changamoto na nitamnukuu hapa, anasema, "Tuna changamoto kubwa ya kukuza uchumi kwa kasi kubwa. Kwa mujibu wa wataalamu ili kuondoa umaskini kwa haraka zaidi, kiwango cha ukuaji wa pato la Taifa kinatakiwa kisipungue asilimia 7 hadi 10 kila mwaka". Maneno mazuri kabisa! Sasa ninachotaka Waziri wa Mipango ayaingize haya kwenye mipango na aingize kwenye mipango tunafanya *Investment* zetu wapi! Kiasi kidogo tunachopata, lazima tuangalie vitu gani vitafanya ili *Economic Growth* ije. Mimi *always* nimekuwa *very clear*, kitakachotuokoa hapo, kwanza ni lazima *Private Sector* ikue. *Private Sector* ndiyo *engine* ya *growth* ya *economy*, na kazi ya Serikali ni kuwawezesha *Private Sector* waweze kufanya vizuri. Wanawawezeshaje? Hatuwezi kufanya vizuri bila umeme, hata tungefanyaje, hatuwezi ku-*industrialize* hizi nchi bila umeme. Kwenye ile *Index* ya nchi zinazokua kiuchumi, unaangalia na *energy* inayotumika. Kwa hiyo, lazima tukubaliane, tuwe tunaambiana kila baada ya mwaka tuone ongezeko la *energy* tunayoitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni *infrastructure*. Lakini, *Infrastructure* hizi lazima tuzijenge kule ambako kutatuletea uchumi wetu. Tunataka ama hatutaki, kwa kweli kwa jografia ya nchi yetu pesa zinazoweza kuokoa nchi hii ziko *DRC*, ziko Burundi, ziko Rwanda. Kwa hiyo, barabara ya kutoka Dodoma mpaka Kigoma kupitia Manyoni – Itigi – Tabora – Kigoma, hili halina mjadala ni *crucial Road*, Reli ni *crucial*, Viwanja vya ndege ni muhimu. Tunataka kukuza *tourism*, hatuwezi kukuza *tourism* bila viwanja vya ndege. Kwa hiyo, mimi naomba sana wenzetu, wanasema kupanga ni kuchagua. Tuamue tujipange tuhakikishe tuna-*invest* vizuri kwenye hayo mambo ili uchumi wetu uweze kukua, kwa sababu lazima tufanye jambo ambalo wanasema lina -*multiply effect,* ni ya muhimu sana katika *economy*. Uchumi wa jografia kwangu mimi ni ajenda muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matarajio yangu sasa tujipange ili tuweze kupambana na changamoto hizi ambazo Waziri Mkuu amezisema ili tuweze kufika huko tunakotaka kwenda. Baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupewa nafasi hii. Lakini kwanza kwa niaba ya wananchi wa Makete naomba niungane na Wabunge wenzangu wote kutoa rambi rambi kwa familia ya marehemu Amina Chifupa na kuwaomba tu kwamba wakati huu mgumu washikamane vizuri, wawe karibu, Mungu atawajalia na atawapa nguvu nyingi wataweza kutokana na hili janga kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashangazwa sana ninapoona kwamba mtu huwa hataki kukubali ukweli. Wakati ulipofanyika uchaguzi Marekani mwaka 2000 mpaka kesi ikaenda mahakamani na baada ya Rais *Bush* kushinda, nakumbuka *Al-Gore* alimpigia simu kukubali kushindwa na kumuunga kwamba wataijenga Marekani kwa pamoja. Sisi Watanzania tunashindwa kuwa na aina hiyo ya utawala mzuri kwamba baada ya uchaguzi, kinachobaki ni kuijenga nchi kwa pamoja. Na hata baada ya uchaguzi ule baada ya *Al-Gore* kushindwa sikuwahi kumwona kwenye majukwaa akipinga sera na utekelezaji wa sera za Marekani, wakati wote wameungana na wamekuwa wakijenga ile nchi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashindwa kuelewa ni vipi wenzetu leo hii wanashindwa kuona mafanikio tuliyoyapata, kwa mfano, kwenye elimu. Labda nitolee mfano wa jimbo langu la Makete. Makete tulipokuwa tunakwenda kwenye Awamu ya Nne, tulikuwa na shule 6 tu za sekondari. Hizo shule zilikuwepo katika Awamu ya Kwanza ya Pili na ya Tatu. Lakini, Awamu ya Nne kwa mwaka mmoja na nusu, tumeweza kujenga shule zingine 7. Kwa hiyo, sasa hivi tuna shule 13 katika Wilaya ya Makete na tuliweza kuchukua wanafunzi wote waliofaulu 2014 na nafasi zikabaki. Sasa ni vipi wenzetu wanashindwa kutambua haya mazuri, wanakuwa wanaleta vigezo vya kwamba hili halipo, lile halipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kwamba kwa msomi mzuri, mwelewa mzuri, lazima uwe muungwana wa kuunga yale mazuri yote ambayo wenzako wanayafanya, ndipo unaweza kujenga hoja. Hata kama unafanya *research*, lazima utambue *research* za wenzako zilizofanywa katika eneo lile ili uweze kujenga hoja ya kuendelea mbele.

Kwa hiyo, ninawaomba tu wenzangu kwamba tukubaliane kwamba kwa hili, Chama Tawala kupitia Serikali wanachapa kazi vizuri na nadhani tunakwenda vizuri kabisa. Tuungane, tujenge nchi yetu vizuri kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naomba nichukue fursa hii pia, kwa sababu Awamu ya Nne wanafanya kazi nzuri sana hasa katika eneo la mazingira, sisi Wana-Makete tumeweza kupata *Kitulo National Park* kama mmeona nimesambaza vipeperushi vya hiyo Mbuga. Lakini nataka nitumie nafasi hii kuwaasa na kuwasihi wananchi wangu wa Makete wanaokaa eneo la Kikondo kwamba ni vizuri wakatii agizo la Serikali la kuondoka na kuacha vyanzo vya maji pale viendelee kushamiri. Kwa kufanya hivyo, watakuwa sio tu wametimiza agizo la Mkuu wa Mkoa lakini pia watakuwa wametimiza agizo la Makamu wa Rais ambalo alilitoa mwaka jana. Wote mnakumbuka hapa. Lakini vilevile watakuwa wameisaidia Makete kupata maendeleo haraka kwa sababu tutaanza kuitumia Mbuga hii kwa kuleta watalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie nafasi hii basi kuwakaribisha Wabunge wote. Hii ni *National Park* ya aina ya pekee ambayo ina maua mazuri, ina ndege wazuri, ina *Livingstone Hills*, ina *landscape* nzuri. Ninawaomba sana mkipata nafasi mkaribie kule pamoja na Mawaziri wote, na ingefaa kama ninyi mkitangulia, basi

nadhani hata Wabunge wanaweza wakawaunga na wakafika kule Makete kuangalia hii mbuga nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutumia nafasi hii pia kuamini kabisa kwamba juhudi za Waziri wa Maliasili na Utalii, basi zitahusisha mbuga hii kutangazwa katika vyombo vya habari vya Marekani vya *CNN* na nchi zingine na hivyo tutapata watalii katika hii tunayoiita *Serengeti of Flowers*, Bustani ya Mungu. Na hivyo hata yale mabonde ya Kyela yataweza kuonekana kwa sababu ukiwa *Livingstone Hills* unapata utalii wa aina yake pamoja na kule Matema *Beach*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hilo, nataka kujielekeza kwenye suala la barabara. Kwanza, nataka kuipongeza Serikali, haya yote ni kwa sababu ya Serikali ya Awamu ya Nne imekuja na mikakati ya vipaumbele. Haya mambo huko nyuma hayakuwepo. Leo tunaongea tunakubaliana kwamba katika nchi yetu lazima tuwe na ajenda ya elimu namba moja, kuna ajenda ya miundombinu, vitu ambavyo ndio msingi katika maendeleo yetu. Kwa hiyo, wametutengea shilingi bilioni 218. Hizi ni hela nyingi ukilinganisha na za mwaka jana ambazo zilikuwa shilingi bilioni 85. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu hapa ni kuwa kama ukiangalia zaidi ilivyosomwa hata kwenye bajeti, tuna shilingi trilioni 3 za kwetu na 3 za nje. Sasa ukizitumia zile za nje ambazo ni za misaada kutengenezea barabara, basi ina maana utakuwa huna hela za kufanyia matengenezo kwa baadaye. Kwa hiyo, ninapendekeza kwamba tujenge utamaduni kwamba zile hela ambazo tunazikusanya kwenye ushuru wetu wa ndani ndio zielekezwe kwenye miundombinu ya barabara kwa sababu unapojenga barabara kwa hela za msaada au kwa mkopo, ilikwishajitokeza miaka ya 1970, tulichukua hela za mikopo tukajenga barabara, lakini yale madeni tukawa hatujalipa mpaka 1990 wakati barabara zimeharibika, lakini tunaendelea kudaiwa madeni.

Kwa hiyo, ninadhani tujenge huo utamaduni wa kutenga zile hela ambazo tunakusanya sisi wenyewe, ziende kwenye barabara kama ni *sustainable source* ambayo inaweza ikajenga barabara lakini vilevile ikafanya matengenezo na hivyo barabara kupitika wakati wote. Hilo ni pendekezo langu. Na zile hela za misaada basi zielekezwe kwenye sehemu zingine kama za Elimu ambazo kama utajenga darasa, utajenga, maabara, nadhani *maintainence* yake haiwezi kulingana na *mauntainence* ya barabara. Hilo ni kuhusu barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuamini kwamba kwa kuwa kiwango hiki ni kikubwa kimeongezeka zaidi ya mara mbili, nadhani barabara zangu za Makete, safari hii zitatengenezwa kwa ubora na zitaweza kupitika. Kwa mfano, tumekuwa na barabara ya kutoka Njombe mpaka Makete ambayo ni kilomita 110, mwaka huu iliharibika sana ilikuwa haipitiki. Wananchi wengi wako vijijini, tumesema ni aslimia 80 wako kule. Sasa hawa watu wanatumia muda mwingi kwenda kutafuta huduma kwa sababu usafiri haupatikani. Kwa mfano, toka Makete mpaka Njombe ni kilomita 110, lakini wakati wa masika watu walikuwa wanatozwa shilingi 15,000/=. Linganisha na kutoka Dar es alaam

mpaka Dodoma ambako kilomita 500, bei ya tiketi ni shilingi 10,000/=. Kwa hiyo, wale watu tunazidi kuwadidimiza kwa umaskini walionao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, kuna kipande cha barabara toka Njombe mpaka Kipengele, kilomita 40, ambacho kipande hicho hakina udongo wowote wa kifusi ambao unaweza ukasaidia kutandaza pale. Sasa inakuwa maajabu wenzetu Wahandisi unakuta wanazoa udongo, wanausambaza huo huo kama kifusi. Kwa hiyo, naomba kuwe na utaratibu wa kutafuta vifusi vizuri vya kuweka sehemu kama hizo ili barabara ziweze kupitika.

Bidhaa zilipanda sana Makete kwa sababu ya barabara mbovu. Siyo hiyo tu, ili tuweze kutumia vizuri hii *Park* yetu, basi tunahitaji barabara nzuri kutoka Chimala – Matamba – Kitulo *National Park*. Barabara zote wakati wa masika huwa hazipitiki. Kwa hiyo, nataka niamini kwamba safari hii kwa sababu Serikali imeweka vipaumbele na miongozo ipo, nina hakika kwamba hili tatizo litatatuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niamini vilevile kwamba kuna *Equation* ya kiuchumi inayosema kwamba *Road Investment* ni sawa sawa na *Transport Improvement*, lakini vilevile ni sawa sawa na *Economic Development*. Mimi nadhani tukifanya vile, tukawekeza kwenye barabara, basi tuna-*improve* usafirishaji na hivyo tutajenga uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongelee kuhusu Sekta ya Nishati na Madini na hapa ni kwenye usambazaji. Ombi langu ni kwamba sisi Makete tumepata umeme wa gridi ya Taifa mwaka 2003. Lakini mpaka leo hii ule umeme haujasambazwa mahala popote pale, uko mjini tu. Hata sehemu za karibu kama Mpangala, hawajapata umeme.

Ni kweli tuna matatizo ya fedha, lakini kwa nini tusiwe na mikakati ambayo inaweza ikaonyesha kabisa kwa wananchi kwamba sisi nchi yetu ni kubwa, mahitaji ni makubwa, lakini safari hii tunaanzia sehemu hii, tutamalizia na sehemu hii ili ratiba ikionekana, basi wananchi wakiona wanaamini kabisa kwamba baada ya miaka miwili/mitatu, sehemu zao kama za Tandala watapata umeme, au sehemu zingine zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kubaki kimya na kuendelea kusema pesa hazitoshi, nadhani linakuwa siyo jibu ambalo ni zuri kwa wananchi kuhusu suala la umeme. Kwa hiyo, naomba wale wote wanaohusika watoe ratiba.

Lakini vilevile waweze kuelekeza nguvu kupeleka umeme sehemu ambao zilikuwa zimeahidiwa huko mwanzoni, lakini pia sehemu ambazo zimepitiwa na milingoti ya umeme kama vile Ujuni, Nkenja na sehemu zingine kama Kinyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia suala la madini. Kweye madini, mapendekezo yangu ni kwamba wachimbaji wengi wamekuwa wakichimba wakisema kwamba wanafanya utafiti. Napendekeza kwamba kwenye kipengele cha ku-*review* mikataba kuwe na kipengele kinachoonyesha muda wa utafiti, kwa sababu hata anayesoma digrii lazima ina mwisho wake, huwezi ukasoma digrii miaka 10/20.

Kwa hiyo, naamini kabisa kwamba hata utafiti una mwanzo na mwisho ili watu waweze kuanza kufaidi matunda yake. Hii nasemea kwa madini yanayochimbwa Makete, *Platinum* ambayo mpaka sasa hivi wananchi hawapati faida yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka vilevile nichukue nafasi hii kuongelea suala la UKIMWI ambalo sisi wana-Makete linatusibu sana, na hapa nataka nichukue nafasi hii wale wote ambao wanatusadia Makete, *NGOs* zote pamoja na mashirika ya nje.

Lakini ninachowaomba ni kwamba kwanza, zile *NGOS* tuziombe zipitishie taarifa zake kwenye Halmashauri ya Wilaya ili tuweze kujua wanapeleka wapi hiyo misaada na ili wakija wengine nao tuwaongoze waende sehemu zingine.

Lakini la pili, nataka niwaombe wadau wote kwamba ni vizuri tukatafsiri UKIMWI Makete kwamba ni tatizo lake ni umaskini. Kwa hiyo, ningeomba juhudi zielekezwe katika kuwaletea wananchi wa Makete maendeleo. Hizi juhudi zingine zinaonekana ni nzuri, tunashukuru sana. Lakini tukiri kabisa kwamba tatizo la UKIMWI chanzo chake ni umaskini tuwasaidie vipi wananchi wa Makete basi tuwapelekee maendeleo na tuwapelekee vipi? La kwanza muhimu ni elimu na miundombinu ya barabara.

Baada ya hayo machache nashukuru kwa kunisikiliza. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia machache niliyonayo katika bajeti hii ya Waziri Mkuu. Lakini pia napenda tu niungane na Wabunge wenzangu kwa pamoja kuipa pole familia ya Mzee Chifupa na Mungu ailaze mahali pema Peponi roho ya Marehemu. Amin.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri kwa uelewa wangu mdogo ninachojua ni kwamba Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunapokuja hapa tunatakiwa tuihoji Serikali, itujibu hoja zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini labda tu ningependa kuwaambia Wabunge wenzangu kwamba, hoja zangu za leo ninazochangia nafikiri sihitaji kujibiwa na Mbunge mwenzangu, yupo Waziri Mkuu na timu yake wanatakiwa kunijibu ninachosema. Hii ninaamini kwamba Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete alikuwa na sababu za msingi kuwaweka viongozi wetu hawa. Mimi naamini kuwa wana uelewa mkubwa na uwezo mkubwa wa kuweza kujibu maswali yetu. Lakini kitendo cha kujibu maswali watu wengine hii inaweza kuwapa hata maswali watu wengine na mashaka kwamba labda hawawezi kujibu maswali yetu. Sasa ifikie mahali tujue tumetumwa na nani, tumepimwa na wananchi kuja kuihoji Serikali, siyo kusaidia Serikali kujibu maswali. Mimi nafikiri Wabunge wenzangu tuungane pamoja kuihoji Serikali. *(Makofi)*

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Kuhusu utaratibu. Naomba kutumia haki yangu katika kifungu namba 50 (8) (e). Tuko hapa Bungeni tunaongozwa na na kanuni zetu. Yeye mwenyewe anakubali kwamba Wabunge wote ni sawa na tuna haki sawa. Kanuni zetu zinaturuhusu anapozungumza mtu yoyote akiwa mwana-CCM mwenzetu, akiwa Mpinzani, tunayo haki kutumia kifungu kwa mujibu wa Kanuni. Kanuni namba 50 (8) (e) inazungumzia kutumia lugha za kuudhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lugha hii ni ya kuudhi. Kama kweli wewe Mbunge umetumwa Jimboni kwako, tetea Jimbo lako, tetea nchi yako, usimzuie Mbunge haki yake kwa mujibu wa Kanuni. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Meryce, alichosema Mheshimiwa Masoud ni kweli kwamba kinachofanyika hapa kwa Wabunge wote ni kuchangia hoja, atakayejibu mwisho ni Mheshimiwa Waziri Mkuu, mtoa hoja mwenyewe. Kwa hiyo, kila anayeongea hapa anachangia. Tafadhali endelea, lakini epusha ile lugha nyingine. *(Makofi)*

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa umahiri wako mzuri. Lakini pia nataka kutaarifu kwamba sijapoteza *point* zangu kwa sababu *target* yake ni kwamba…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Meryce huwezi kubishana na kiti endelea kama una hoja nyingine.

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kupoteza muda naomba ukumbuke zile dakika zangu. Ningependa kwenda moja kwa moja kwenye suala la kudhibiti UKIMWI. Nilipokuwa nikisiliza Hotuba ya Waziri Mkuu, alizungumza vizuri sana juu ya mikakati Serikali iliyonayo ya kuweza kushughulikia suala la kudhibiti UKIMWI. Ni kweli kabisa amesema kwamba Serikali iko tayari kutoa misaada katika asasi za Serikali, sekta binafsi na hata Halmashauri nyingi ambazo tayari zimekwishaathirika kutokana na hali halisi inavyoonyesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini labda ningependa tu kusema kwamba imefikia mahali hata fedha hizi zinazotolewa kuelekea katika maeneo husika, inakuwa ni tatizo kufanya kazi. Serikali ina mikakati mizuri lakini labda waingilie kati ili kudhibiti kwa uhakika zaidi suala hili la UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa tu kuishauri Serikali kwamba ifikie mahali wajaribu kufuatilia wanapokuwa wametoa fedha hizi za kwenda kudhibiti UKIMWI, je, zimefika mahali panapohusika au ili mradi tumeelezwa mahali hapa kwamba fedha imetolewa? Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri ifikie mahali fedha zinapotolewa na Serikali ifuatilie zile hela zimekwenda zimewafikia walengwa ili lile kusudi lililokusudiwa liweze kukamilika. *(Makofi)*

Lakini vile vile ningependa kusema kwamba, hata vituo vinavyolea watoto yatima kwa sasa hivi, kwa kweli vimekuwa ni tatizo kubwa. Tatizo lake ni moja, imefikia mahali sasa hivi imekuwa ni biashara tu. Hata mimi nikitoka hapa, nikatengeneza

nyumba nikawa na vitanda vyangu 10 nitakusanya watoto kumi nitakuwa nao pale nitatengeneza mihutasari yangu vizuri na kisha nitakuja kuomba kwamba sasa mimi nina kituo cha kulea watoto yatima. *(Makofi)*

Lakini siyo kweli, ukichunguza na bahati nzuri kuna maeneo fulani pale Dar es Salaam, kuna sehemu moja nilikuwa nikipita nikienda Bungeni kuna mahali nikakuta wameanika shuka za watoto yatima. Ni jambo la kusikitisha. Ukiziangalia zile shuka hata wewe mwenyewe huwezi ukaipigia deki. Sasa ifikie mahali ufanyike ufuataliaji katika vituo kuona vinafanya kazi namna gani. Kama mimi tu mtu wa kawaida, mtu mdogo tu nimeona, sijui wale wanaotoa fedha wanafanyaje jinsi ya kufuatilia hizi fedha na kuhakikisha kwamba wanafanyakazi vizuri na kwa makusudi yaliyokusudiwa kwa ajili ya hizi fedha! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kusema kwamba pia hawa watoto wanapokuwa wanalelewa katika vituo hivi wajaribu kuendelezwa katika maisha yao ya baadaye. Kwa mfano, mtoto anapokuwa ameanza shule Serikali ijaribu kumwangalia, mtoto anapomaliza Darasa la Saba Serikali ijaribu kumwangalia na hata wakati mwingine imsaidie basi kuendelea na elimu yake ya Sekondari ili iweze kumjengea mazingira mazuri ya baadaye. Sio kwamba imuache hapo hapo alipo, hataweza kuendelea mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nashauri kwamba hawa watoto wajaribu kuendelea kuangaliwa baadaye ili waweze kuwa na maisha mazuri wasiishie pale pale tu kwenye vituo vya watoto yatima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka hapo, naomba niingie kwenye hizi fedha zilizotolewa kwa ajili ya wajasiriamali. Tulipopata taarifa hii kwa kweli tulifurahi sana kwa sababu Watanzania wote walijua kwamba sasa wamepata msaada. Ni kweli kabisa hizi fedha zilitolewa na namshukuru hata Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, wakati anatamka hilo tamko katika Mkutano wetu wa *RCC.* Nilikuwepo akasema fedha zimekwishafika na tayari Wilaya zote zimekwishagawiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi nashindwa kuelewa hata pale nilipo, hivi hizi fedha zilikuwa zimewalenga watu gani? Tamko linasema wajasiriamali, lakini wajasiriamali ni akina nani? Unajua ukifuatilia vizuri hizi fedha unakuta watu waliopewa fedha ni watu ambao wanajiweza. Mama Ntilie hakupata hizi fedha, Serikali imetoa maelekezo watu waunde hata vikundi watengeneze *SACCOS*, lakini nataka niseme katika eneo ninalotoka Wilaya ya Maswa, kwingine siwezi kusema kwa sababu sina ushahidi, lakini kusema kweli Watanzania waliotegemea kupata hii mikopo hawakupata kama ilivyokuwa imekusudiwa. *(Makofi)*

Sasa nilikuwa naishauri Serikali hebu wajaribu kuangalia zile fedha zinapokuwa zimefika kule inakuaje? Utaratibu ukoje? Wanapokuwa wanatoa maelezo hapa, basi yafanane na utekelezaji unaokwenda kutekelezwa kule. Isije ikafikia mahali tamko linatoka hapa, ikifika kule yanatokea mabadiliko lawama zinarudi kule wanakotoa fedha. Kumbe utaratibu ulikuwa ni ule ule. Mimi nilikuwa nafikiri ifikie mahali Watanzania wanapoambiwa kitu wafafanuliwe kwamba fedha ikitolewa inatolewa kwa staili zipi,

wajipange kujua kwamba hizo fedha zinatolewa kwa njia hiyo ili waweze kutimiziwa haja za mioyo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikufurahia kuona kwamba watu waliopata hizo fedha mtu anakwenda kama mmoja anapata hiyo fedha mara moja lakini watu wanahangaika wanatengeneza *write up* na nini, lakini hakuna wanachokipata. Lengo la Serikali lilikuwa ni zuri mno. Nilikuwa nafikiri kwamba wakati mwingine au hata sasa kama inawezekana wajaribu kuangalia hizi fedha, kusema kweli haziwajafikia walengwa kama ilivyokuwa imekusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nikimbilie kwenye suala posho za Madiwani. Posho za Madiwani kwa kweli mimi kwanza mara ya kwanza nilipofikia lile tamko haraka haraka kabla sijaangalia wakati wanasema kwamba watapata Sh. 60,000/= mimi nikifikiri kwamba zinatolewa maeneo yote, wanakwenda kupewa angalau pamoja na kwamba hazitoshi. Kumbe inasemekana hivi inategemea na uwezo wa Halmashauri. Sasa unajua kuna Halmashauri nyingine Waheshimiwa Wabunge wanaogopa kusema humu, bahati sisi tunamshukuru Mungu tunaweza kusema, mwingine anaogopa kusema. Kuna Halmashauri nyingine wanapata fedha za ajabu. Hawa wanafanyaje kama uwezo wa kutoa ile Sh. 60,000/= hawana? Kwa sababu kuna watu ambao hata ile Sh. 30,000/= walikuwa hawajaweza kuipata kwa sababu Halmashauri ina uwezo mdogo. Sasa Serikali inasema juu ya hawa Madiwani wanawasaidia vipi? Kwa sababu Madiwani wanatusaidia sisi tunapokuwa huku wanafanya kazi. Sasa ili na sisi tuonekane tunashirikiana nao, tunaomba Serikali iingilie kati iwasaidie Waheshimiwa Madiwani, wana matatizo makubwa mno! *(Makofi)*

Lakini bado mimi nasema hata Sh. 60,000/= haitoshi. Afadhali ingekuwa hata Sh. 100,000/= kidogo afadhali, tungefunga macho tukasema Mungu saidia jamani uchumi wetu upande angalau kuja kufikia mwaka kesho wafikishe hata Sh. 150,000/=. Lakini sasa hiyo Sh. 60,000/= basi kama imeshakuwa hivyo wasaidiwe na wale wengine ambao Halmashauri hazina uwezo angalau wapate kwa pamoja. Tunaomba Serikali iingilie kati iweze kusaidia hili suala la Madiwani hawana mahali pa kusemea. Lakini imefikia mahali kwa kuwa wana wawakilishi, basi tunaomba isikie sauti zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nitakwenda kwenye eneo linalohusu mambo ya rushwa. Nimemsikia Waziri Mkuu, ana mikakati kweli! Kweli akisema amesema! Mikakati ya rushwa ni moto moto! Lakini mikakati ya rushwa hatutaweza, mishahara ya watumishi ni midogo. Siyo kwamba nafundisha, naomba nieleweke ninasema kwamba mishahara ni midogo.

Sasa mtumishi anasomesha, analipa umeme, analipa maji, anavaa nguo ya kwenda kazini, anataka kiatu cha kisasa, ana simu inataka dola, wewe unampa hii hela unafikiri ataacha kutafuta fedha kweli? Lazima atafute fedha. Haitoshi! Fedha ni ndogo ndugu zangu! Ukiangalia maeneo mengine ambao fedha zao ni nzuri, rushwa ipo, lakini ni kidogo sana mpaka uitafute. Lakini kwetu inatafutwa kwa sababu haitoshi. Hata

ningekuwa mimi angalau nitang'ang'ania angalau chochote kipatikane watoto wangu waweze kupata kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa umahiri wake mzuri na kazi yake anavyoifanya inavyokwenda vizuri, hebu ajaribu kuangalia hizi fedha jamani, hawa watu wanawasaidiaje? Mshahara mdogo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakwenda kwenye suala la miundombinu. Mikakati ya miundombinu ni mikubwa mno. Ninajua kwamba kazi inakwenda vizuri na inatia moyo na mimi ninachotaka kusema ni Wilaya yetu ya Maswa jinsi ilivyo. Wilaya yetu ya Maswa tulikuwa tunaomba TAMISEMI ijaribu kuingilia kati hizi pamba zinavyouzwa, wanapomaliza kununua, njia za kupitisha zile pamba ni tatizo. Magari yanakwama, hakuna sehemu ya kupita. Namwomba Waziri Mkuu ajaribu kuisaida Serikali ya Mitaa ili angalau tuweze kuangalia tunafanyaje. Mheshimiwa Pinda, hebu jipapaseni ili mjaribu kuangalia mnafanyaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningejaribu kusema na ile barabara ya kutoka Mwanza – Mabuki - Jojilo – Malampaka – unakwenda Maswa – Bariadi – mpaka Mwanuzi, ile barabara ina matatizo. Mheshimiwa Chenge amekwisha! Hebu jaribuni kufikia mahali mumwokoe mwenzenu huyu, harudi tena ile barabara isipotengenezwa! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nirudi kwenye suala la afya. Suala la afya ningependa kusema labda Serikali ijaribu kufikiria hizi zahanati zinazoanzishwa ni nzuri kweli na tunashukuru mno na hata mimi eneo langu ikiwepo ninapenda, lakini je, hizi Zahanati zina Madaktari? Uzoefu nilionao mkishatengeneza, hizi Zahanati na mimi nikiwemo nazitengeneza ni zangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachomoa madaktari walioko Wilayani, tunawashusha huku chini, sasa pale Wilayani nani anayebaki? Kwa sababu ndiyo *system* hiyo. Wanasema punguza wawili, punguza watatu warudi wakati Wilaya haitoshi, wale wahudumu hawatoshi, watalaam ni wachache, lakini tunapokuja sasa tunachukua pale tunashusha huku chini. Je, pale panabaki na nini? Mimi napenda Zahanati, hebu naomba hili jambo angalau mjaribu kulifanya 2010, mna wasiwasi gani? Mtarudi tu, kazi zenu zinaonekana kama zinafaa, kama hazifai basi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dakika moja sasa ambayo imebaki, napenda niongelee suala moja la ujumla kwa ruhusa yako, linalohusu vyeti vya kuzaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila Mtanzania aliyezaliwa katika nchi yake ni haki yake kuishi nchini na ni haki yake kupata kazi na ni haki yake kusoma. Imefikia mahali hivi vyeti watu wanashindwa kwenda shule, wanashindwa kwenda *JKT* kwa ajili ya hivi vyeti. Serikali inasemaje? Ni kwa nini isisaidie hivi vyeti vikatoka bure badala kutolewa kwa fedha. Mtu mwingine wa mjini anajua maana ya cheti ni nini, lakini mtu wa kijijini hajui ni cha nini.

Mtoto anapofikia mahali pa kwenda shule anashindwa kwa sababu mzazi hakujua maana ya cheti. Kwa nini msihamasishe hivi vyeti mkawapa wananchi kwa kuokoa maisha ya watoto wao ya baadaye? Hivi vyeti jaribuni kuvitoa bure.

Mheshimiwa Waziri Mkuu ndugu yangu, umefanya mambo makubwa, tunajua kazi yako, ni mchapakazi mzuri, mimi najua hilo. Hebu wasaidie hivi vyeti bure, mtenge fungu la kumsaidie yule mwananchi wa kijijini asiyejua maana ya cheti ni nini! Mtoto akitaka kwenda shule anashindwa kwenda, huko Maswa wanasema yale *(alizungumza Kisukuma)*. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa huyo mtoto ataharibikiwa kwa sababu mzazi wake hajui. Naomba Serikali ijaribu kuwasaidia hawa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Huyo ni Mheshimiwa Mercy Emmanuel, amemfurahisha Mwenyekiti kwa mambo mawili. Kwanza vazi lake la kijani, lakini la pili Mwenyekiti hakujua kumbe ni mwanawane Mkandamizaji. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nami kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja ya Waziri Mkuu iliyopo mbele yetu. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahuwataala* aliyetujalia uzima na afya njema. Lakini naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliotangulia kutoa pole na rambirambi kwa kifo cha Amina Chifupa Mpakanjia ambaye alifariki juzi. *Inshallah* Mwenyezi ailaze roho yake mahali pema Peponi. *Amin!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina machache sana ya kuzungumza. Lakini kwanza kabisa nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwapongeza viongozi wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashind Mohammed na Dr. Wilbrod P. Slaa kwa jinsi ambavyo wameonyesha umahiri wao kwenye kuiongoza Kambi yetu. Nawaambia kwamba wasichoke waendelee na sisi tuko pamoja nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niende kwenye hoja moja kwa moja nami nigusie kwenye matumizi mabaya ya fedha za Serikali. Kama kuna ambalo Watanzania linawakera, basi ni matumizi mabaya ya fedha za Serikali. Kama kuna jambo ambalo linawakera zaidi ni pale ambapo baadhi ya wale ambao wanatumia fedha hizo wakawa wanaendelea kutamba Mitaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu cha hotuba ya Waziri Mkuu ukurasa wa 66 amegusia, nami naomba ninukuu kwa ufupi kwa haraka haraka.

"Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine iliyoko mbele yetu na ambayo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amesisitiza ni nidhamu ya matumizi ya fedha za Serikali. Serikali inakusanya fedha kwa njia ya kodi na misaada mbalimbali. Fedha zote ni mali ya wananchi wa Tanzania na lazima zitumike kwa kuzingatia kanuni na taratibu za fedha. Serikali inawajibika kwa wananchi ambao ni

walipa kodi na wafadhili wanaotupatia misaada kuhakikisha kuwa fedha zao zinatumika kwa maendeleo ya nchi hii na hazifujwi." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali tuliyopata hivi karibuni kwa mwaka wa fedha ulioishia June 30, imeonyesha kuna mapungufu makubwa. Kwa vyovyote iwavyo kwa sababu sisi Wabunge ni wajibu wetu kuihoji Serikali, basi tunapenda na tunaendelea kuhoji Serikali tuelezwe kinagaubaga jinsi ya mapungufu hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi hatutasita kuhoji Serikali hata kama tuna vidhibiti kama hivi ambavyo wengine wamesema sio vyema kuvitumia, lakini sisi tutaendelea kuvitumia kwa sababu vimeletwa na Serikali na nimpongeze Rais Jakaya Mrisho Kikwete ambaye ameharakisha suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niende moja kwa moja kwenye Kitengo cha uhakiki wa mali. Ningeomba nipate maelezo kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, kwenye upungufu wa fedha ya Sh. 39,975,000/=, yaani taarifa ya samani na vifaa visivyokuwepo katika orodha au *ledger*. Mheshimiwa Waziri Mkuu anapotingisha kichwa, bila shaka naona amenifahamu vizuri nidhamu ya matumizi ya fedha za Serikali kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, hii ni yake anasimamia yeye. Lakini pia kwenye Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa nako kuna mapungufu ya Sh. 919,701/=. Ni ofisi yake, anasimamia yeye. Kwa sababu anasimamia yeye na kwa sababu yeye ndiyo Kiongozi wa Shughuli za Serikali, nafikiri wakati akifanya majumuisho atamweleza Mbunge wa Mtambile kulikoni! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee. Kuna taarifa ya vifaa visivyo na uthibitisho wa kupokewa, Ofisi ya Waziri Mkuu Sh.7,480,000/= na ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kuna Sh. 7,455,650/= nako yeye ndiyo msimamizi. Bila shaka anaelewa hili, tunaomba atupe maelezo wakati wa majumuisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usichoke kunisikiliza na hili naomba uniruhusu taarifa ya vifaa visivyo na udhibitisho wa ununuzi Ofisi ya Waziri Mkuu Sh. 13,606,708/= lakini Msajili wa Vyama vya Siasa nako kuna Sh. 2,128,000/=. Hayo ni mapungufu mengine ya fedha. Hizi ni fedha anasimamia mwenyewe Waziri Mkuu. Kwa kuwa ni mtu mzima na hicho ni kilemba, kwa hiyo, kama kilemba kikionekana kwenye kutingatinga tuna hofu na Wizara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taarifa ya utoaji wa vifaa visivyoingizwa vitabuni. Ofisi ya Waziri Mkuu kuna mapungufu ya Sh. 17, 799,940/= lakini kwenye Msajili wa Vyama vya Siasa nako kuna Sh. 1,212,560/=. Nimalizie kwa haraka haraka bila kuathiri masharti ya muda wangu, taarifa ya utoaji wa vifaa visivyo na stakabadhi, Ofisi ya Waziri Mkuu kuna mapungufu ya Sh. 5,057,200/=. Kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kuna mapungufu ya Sh. 4,478,500/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hii Wizara, Ofisi anasimamia mwenyewe Waziri Mkuu na kwa kweli haya ni mapungufu na tutake tusitake Mheshimiwa Waziri Mkuu haya mapungufu yaonekane yanafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Kwa kuwa huko nyuma kulikuwa na maelezo ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyatoa hapa Bungeni na rafiki yangu juzi aliyasema Mbunge wa Simanjiro - Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, alimnukuu Waziri Mkuu kwamba: "Ambaye hawezi mdundo wa awamu ya nne atupishe." Sasa ningemwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa mapungufu haya hizi ni Wizara anazozisimamia yeye. Ni lini hawa watatupisha atueleze kwa sababu hizi ni fedha za Watanzania walipa kodi maskini ambao kwa vyovyote vile wanahitaji fedha zao zitumike vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nataka nijikite huko huko, kuna malalamiko mengine na Waheshimiwa Wabunge mara nyingi wamekuwa wakieleza hapa kwamba kuna mapungufu makubwa ya fedha kwenye Halmashauri, nako ukienda mapungufu yake basi kidogo yanakuwa na lugha ya virojaroja. Waheshimiwa Wabunge mara nyingi wamekuwa wakinung'ung'unika hapa kuhusu nidhamu ya matumizi ya fedha, Serikalini nako sio shwari, masurufu yasiyorejeshwa kwenye kitabu hiki kikikubwa nako nanukuu: "Kwenye Halmashauri zifuatazo 16, kuna mapungufu ya fedha Sh. 862,993/=. Nasema, hiyo ni hatari, fedha za walalahoi."

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna mapungufu kwenye malipo yaliyofanywa bila kumbukumbu sahihi, kuna Halmashauri 46. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu mwenyewe yupo hapa na bila shaka wakati wa majumuisho atanieleza kuna mapungufu ya fedha Sh. 2,403,092,747/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie, kwenye hati zilizokosekana nako hali sio shwari, wasomi wamefunzwa namna ya kutunza hati lakini leo tumeambiwa hati zimekosekana, kuna mapungufu ya fedha Sh. 1,934,574,846/=. Tutakwenda wapi? Tusidanganyane. Kwa hali hii hatutafika! Tuna mipango mingi, tuna MKUKUTA, MKURABITA, MKUMBITA, 2010, ngapi ngapi lakini hatutafika. Hizi fedha inavyoonekana zimekwenda kwenye MKUKUBI, fedha zinatoka kwenye MKUKUTA zinakwenda kwenye MKUKUBI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, MKUKUBI ni istilahi mpya ambayo walalahoi wenyewe wamelitoa baada ya kuona fedha zao hazitumiki vizuri kwenye Halmashauri na kwenye Serikali kuu. Yaani Mkakati wa Kukuza Uchumi na kupunguza uchumi binafsi. Kwenye MKUKUBI ziko hizi fedha. Kwa vile Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema hapa kwamba: "Ambaye hawezi mdundo wa awamu ya nne atupishe," nina imani, lakini wakati akifanya majumuisho atueleze. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo lilikuwa angalizo langu la kwanza. Naomba kwa vyovyote iwavyo kwa hali hii bila shaka na ninavyomjua Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyo msikivu basi nahisi atalifanyia kazi vizuri kabisa hasa ukitilia maanani siku za nyuma tulikutana katika mambo ya Mzakwe na nini akaweka sawa na *Alhamdulillah* Mungu akubariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee na suala la Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF).* Hili ni jambo zuri, wananchi wameibua miradi yao mbalimbali, lakini swali, je, miradi hiyo itakamilika lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2006/2007 Serikali ilitueleza hapa kwamba itahakikisha miradi yote ambayo haikukamilika yaani *TASAF I* itakamilishwa. Jimboni kwangu Mtambile wameniambia mara hii huwezi kuvuka bahari ukafika Pemba kama hujaeleza Bungeni suala zima la barabara kutoka Kangani kuja Mtambile au Mtambile - Kangani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ambayo *TASAF* waliifanyia marekebisho ilikuwa ina kifusi katika maeneo mengi. Lakini kwa bahati mbaya matengenezo ya *TASAF* baada ya matengenezo yao waliondoa kifusi na wakabakiza udongo. Nasema hali ni mbaya sana kwenye barabara hii. Barabara hii imeanza vijiji vya Mjimbini kwenye Shehe ya Mjimbini - Tanga barabarani - Tanga Mkwajuni - Kangani - Skuli mpaka kufika Kangani Sokoni kuelekea kwenye daraja Fufuni mpaka Jimbo la Mkanyageni la Mheshimiwa Mnyaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata wale wananchi wa Kuukuu ambao nao waliibua mradi na wakaahidiwa kwamba wao barabara yao itatengenezwa, basi nako vile vile hakuna ahadi iliyotekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa ni kwamba barabara ilikuwa ina kifusi kwa muda mrefu inapitika vizuri, lakini *TASAF I* ikaondoa na Serikali ikaahidi hapa kwamba litatekelezwa hilo kwa kuweka kifusi, nasema hatutawatendea haki wananchi wa Jimbo la Mtambile, hatutawatendea haki wananchi wa Vijiji vya Mgimbini, Tanga na Kangani na Kuukuu. Kwani hili ni Serikali ambayo wao wenyewe waliahidi watatekeleza. Ni imani yangu, ushauri wangu kwa sababu mimi sijui ni kigezo gani ambacho kilitumika, kwa vile mwaka jana tuliambiwa hili, kwa hiyo sijui kama kigezo gani kilitumika ambacho kuna maeneo mengine yalifikiriwa, lakini Jimbo langu la Mtambile mimi halikuonekana. Lakini najua na Mheshimiwa Hawa A. Ghasia ambaye alitoa hii mwaka jana *inshallah* ninavyomwona vile alivyo, basi atalitia jicho la huruma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie, naona kengele ya kwanza imelia. Suala la vitambulisho vya Taifa tunasema hili ni jambo zuri Serikali imeliona na wameahidi kulitekeleza. Lakini mimi nina ushauri kwa haraka haraka kwamba zaidi mwangalie sehemu za mipakani katika kutoa vitambulisho hivi. Lakini kwanza ufanyike uhakiki wa kujua wahamiaji haramu. Mimi nimefika Kigoma, Kagera, naelewa ni Mjumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa vizuri haya matatizo. Tufanye uhakiki wa kuwajua wahamiaji haramu na kwa sababu ndani ya maeneo haya unagundua kwamba mipakani mle wameoana, ukifika pale Mabamba ya Tanzania na Mabamba ya Burundi Mjomba na Shangazi wameoana. Ukifika Kilelema ambapo kuna Malagalasi imepakana pale Mjomba na shangazi wameoana. Kwa hiyo, haya ni mapungufu! Ukifika Tunduma

nako wote ni Wanyamwanga ambaye *chief* wa Kikabila amefika zaidi ya kilometa 20 ndani kule. Kwa hiyo, unakuta hapa ni matatizo! Lazima tuwajue Watanzania sahihi tuwape vitambulisho vyetu. Isije ikaonekana tunawaita Watanzania, lakini sio Watanzania. Hilo lilikuwa ni angalizo langu na ninavyoona Mheshimiwa Waziri Mkuu anavyoniangalia vizuri naona amelifahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie haraka kwenye ajali za majini. Juzi Mjumbe mwenzangu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Mheshimiwa *Brig. General* Hassan Ngwilizi wakati akijibiwa swali lake na Mheshimiwa Dr. Makongoro Mahanga alitoa takwimu hapa jinsi ya vifo vinavyotokea baharini au ajali na kwenye maziwa. Nanukuu: "Mwaka 2005 kulikuwa na ajali 11. Baharini 5, ziwani 6, vifo baharini kimoja, vifo vya ziwani 41; mwaka 2006 ajali 15 baharini 8, ziwani 7, vifo baharini vitano, na vifo ziwani 17.

Mimi ninachotaka kusisitiza au ombi langu, kwa kuwa kuna vyombo ambavyo ni vya majahazi, wanapakia mizigo, kwa nini Serikali isiwawezeshe kuwapa angalau makoti ya kuokolea maisha? Suala lipo, Mama Mongella siku ile alisema jamani vifo vipo vingi, basi angalau Serikali iangalie utaratibu wa kutoa makoti ya kuokoa maisha. Yaani hata zile boti za mizigo, majahazi, mitumbwi na mingine kwa sababu kwa vyovyote vile bahari haitabiriki, inaweza kuwa asubuhi shwari lakini jioni yakatokea mabadiliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu vifo ni vingi. Hawa ni Watanzania na ni vyema tuwafikirie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kabuye. Makatibu, angalieni dakika zake, kwa sababu ya matatizo ya kiufundi.

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru sana. Labda humu kuna mkono wa mtu. *(Kicheko/Makofi)*

Mwenyekiti na mimi pamoja na wenzangu nawapa mkono wa rambi rambi jamaa wote wanaohusika na kifo cha ndugu yetu, Mbunge mwenzetu. Nawapeni pole sana. Lakini kabla sijasahau, naomba kabisa kuunga mkono yote yaliyosemwa na Wapinzani asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania, kama mmoja alivyosema hatustahili kusahau. Baada ya kuhangaishwa na mkoloni Watanzania tuliamua kuondokana na mkoloni, lakini tukajipa masharti kwamba mkoloni akishaondoka matunda ya uhuru tugawane wote sawa. Hii nafananisha na hadithi moja niliyoisoma huko nyuma, shamba la wanyama. Shamba la wanyama, wanyama walimfukuza Bwana Jonas wakakubaliana kwamba sasa mateso waliyokuwa wanateswa na Bwana Jonas hawatayarudia. Lakini kati yao kukawepo kundi la wajanja wanakwenda wanabadilisha mapatano. Sasa wale wenzao wakiwauliza mbona mmebadilisha wanasema hapana hatujabadilisha. Mwisho wakarudi kule kule walikotoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhuru tulipanga kwamba ili tuweze kupata matunda ya uhuru 1977 tukatunga Katiba inasema, Tanzania itaongozwa na Serikali inayofuata demokrasia, ujamaa na isiyo na dini. *(Makofi)*

Je, ndivyo ilivyo demokrasia? Wakati msimamizi wa uchaguzi anateuliwa na Mwenyekiti wa Chama Tawala na mlolongo unakwenda mpaka Mkurugenzi wa Wilaya aliyeteuliwa na Mwenyekiti wa Chama Tawala. Hivi atamruhusu Kabuye awe Rais? Ana uhakika kwamba atateuliwa tena? Angalieni hilo ndugu zangu? Hiyo ndiyo demokrasia ya Watanzania? *(Kicheko/Makofi)*

Nataka usome hayo mapatano kwenye ukurasa wa 13 wa Katiba yetu. Ujamaa, ungalikuwepo, ndugu yangu Kingunge angetuelezea ujamaa ukoje tuopanga. Ujamaa, tufute kwenye katiba, hakuna ujamaa! Tunaijua misingi ya ujamaa! Ujamaa ni kugawana ile keki ndogo watu wote sawa. Lakini kuna watu wanaohimizwa kujenga maghorofa wakati wengine anakula mara moja kwa siku. Wanapewa pesa za umma kujenga maghorofa wakati watu hawajui, wakila leo kesho watakula nini. Ndiyo ujamaa! Futeni. *(Makofi)*

Kama wale wanyama, leo tukiuliza tulisema rushwa ni adui wa haki, sitapokea wala kutoa rushwa. Lakini rushwa ya uchaguzi ilipotokea sisi kama wale wanyama tukaulizwa, mbona hii rushwa? Wanasema aah, hii sio rushwa ni takrima bwana. *(Makofi)*

Serikali ikaingia kuuza mashirika tuliyotengeneza yajenge ujamaa. Ukiuliza mbona mashirika yanauzwa? Ah, tunafufua uchumi! Wewe, uchumi ulikufa mikononi mwa nani? Tunafufua uchumi, mbona tunagawa rasilimali zetu zote? Madini wanachimba, kila kitu! Ah, hawa hapana, ni ndugu zetu wawekezaji. Tumerudi kule kule tulikokataa. Huo ulikuwa utangulizi tu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima tumewafanyia dhambi na hatuna shukrani. Wakati tunajitawala kilimo ndicho kimejenga nchi hii. Kahawa, pamba, pareto, korosho, katani, ndivyo vilivyojenga barabara toka Dar es Salaam mpaka hapa. Barabara ya Dar es Salaam - Tunduma, hawa ndiyo waliotufikisha hapa. Leo hii tumeshawatupa. Tumekuwa kama yule punda! Naomba niingize pua; haya ingia bwana; na kichwa! haya ingiza, mwili umeingia, tajiri anatupwa nje. Ndiyo yamewapata wakulima. *(Makofi)*

Mimi ninawajua! Unaweza ukashangilia mambo ni mazuri, ni mazuri, lakini ninawafahamu. Waheshimiwa Wabunge wote wanakotoka wakulima wako hoi, wanatembea wengine hata viatu hawana, na nyayo zimepasuka, visigino vina ufa. Lakini bado mnakuja hapa mambo shwari, haya. Hivi wewe wa Liwale unasema mambo ni mazuri kweli? Wewe wa Lindi ni kweli kabisa! Na wananchi wanakusikia wa Lindi, wa Tunduma. Haya! *(Makofi/Kicheko)*

Mimi wa Biharamlo siwezi kuwasaliti, wako hoi pamoja na kwamba kuna mambo yamefanyika, ndiyo, lakini kasi tuliyoitarajia siyo hiyo. Mambo ni mabaya sana. Mkulima leo hii ameachiwa, walanguzi wanamrarua. Wanamlangua Mgogo karanga kimbo Sh. 300/=, hana msaada, ufuta unakwenda. Juzi nikasema jamani vipi, mnasemaje? Kabuye anasema wasisombe. Wabunge mnasemaje? Wasombe! Wabunge wote, wasombeee! Ushahidi labda wale wanaokalisha watu chini, labda mtasema nadanganya, sidanganyi. *(Kicheko)*

Wanasomba, mkulima hana bei. Mkulima zamani tulikuwa na *GAPEX* tunakusanya mazao kwa bei nzuri inayoweza ikamsaidia mkulima, leo hakuna. Tulikuwa na *National Milling,* leo hakuna. Wakulima wanararuliwa na manyang'au. Unamwambia mkulima akope, nani atamkopesha mkulima anayelima kutegemea Mwenyezi Mungu alale vizuri mvua inyeshe? Hakuna *irrigation!* *(Makofi)*

Mimi nimetembea nchi nyingi, wanasema huwezi ukalima kama hujavuna maji. Dodoma inajulikana ni kame. Mnaifanya nini ndugu zangu? Biharamlo inajulikana katika Kagera ni kame, mnafanya nini? Angalieni mkulima alichotufanyia, lazima tumuenzi jamani! Yeye ndiye aliyeifikisha nchi hii hapa. Mfugaji hajui josho. Juzi kwa kuwa wakubwa walikosa nyama, ng'ombe wote wakachanjwa. Wamekosa nyama, *Rift Valley* imeleta taabu. Nyama tayari wanakula, hakuna anayechanja ng'ombe. Hakuna josho, mpaka tunaomba *Rift Valley* iwe inakuja, ili ng'ombe wachanjwe. Wakubwa wakose nyama! *(Makofi/Kicheko)*

Wakulima wanahitaji minada ya kuuza ng'ombe wao, Wakomoro wanakwenda kununua kwa watu vijijini. Hivi kwa nini msiseme wasiende vijijini watu wa nje, wanunue kwenye mnada angalau hawa vijana ndio waende wakusanye kutoka vijijini waje wawauzie hawa wafanyabiashara kwenye mnada? Wanakwenda mpaka kule, wanamgonga mfugaji. Hivi kweli tukisema, hakuna anayekataa kuwa hakuna maendeleo, lakini tunalosema mwangalieni huyu mtu mnyonge.

Kuhusu elimu, niwaambieni siri, huwa ninasema twende na mipango, upangilie tangu tujitawale tulijua kwamba lazima watu wasome shule za sekondari. Lakini mtu anaota tu akiamka shule zote nne zijengwe kama Mungu alivyosema mbingu na nchi viwepo, vikawepo. Mnaweza mkafanya hivyo ndugu zangu. Wamelilipua hilo, mimi nikahangaika na viongozi tuwafanyeje, juzi watu wamepigwa na njaa, tunahangaika, viongozi wetu wakaitwa na ndugu yetu Waziri Mkuu na tukasema eeeh! Neema imekuja, wataleta chochote.

Wamekuja, namwuliza Mkuu wangu wa Wilaya, vipi? Anasema tumeambiwa bwana nakuomba ufumbe macho. Wametupa mwezi wa nne tuwe tumemaliza. Umeleta hela? Hakuna. Wananiambia nisipomaliza bwana unisaidie, nitafukuzwa kazi. Ufumbe macho. Yaani wamesema mwezi wa nne hawakukupa hela? Maana yake pigeni watu watapike hela. *(Makofi/Kicheko)*

Kweli! Kama mna hela simama unikalishe. Nina ushahidi, watu wamelala ndani. Lakini mimi Mkuu wangu wa Wilaya nikaona akifukuzwa kazi, maskini mtoto na mke

watapata shida, tukafumba macho. Mwenyekiti mmoja wa Kijiji amewekwa ndani mara nne. Tumejenga sekondari maelfu; ndugu yangu usione mshumaa unawaka, mshumaa umeteketea, wako walioteketea ndugu zangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kitu kizuri, lakini naomba mpangilie jamani. Pangilieni hawa watu wana hela, inatoka wapi? Wengine wamewekwa ndani kwa Sh. 10,000/=, anatoa shilingi 5,000/= mke wake awe nyumbani, yeye anakaa porini. Ninao ushahidi. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, ndugu zangu hata hivyo, hizo shule nimekwenda watoto wa kike wanalala kwenye darasa, asubuhi yake wanaweka virago pembeni. Hilo darasa ni bweni na ni darasa. Ya nini? Hivi tuna mzimu unaosema msipopeleka watoto wote *secondary school* mtakufa? Waziri Mkuu ungekufa kama mnafanya utaratibu huu! Roma ilijengwa siku moja, ndivyo wamekuambia! Kuliko kuumiza watu namna hii, tunapenda lakini hata hivyo hawa wanapomaliza *O-level* wanakwenda wapi *A-level?* *(Makofi)*

Leo hii badala ya kusema tumemaliza *O-level* sasa tuanze *high school,* mnasema mwaka kesho bwana. Baragumu inalia ya vituo vya afya, jamani. Nini hii? Nani aliyetuloga? Kwa nini tusiende vizuri sana, twende taratibu, tutafika! Afya, afya nayo ni kama ile *rift valley.* Ukimwi kwa sababu umegusa mahali nyeti, yeyeye! Ndugu yangu ukimwi! Lakini Malaria inaua wangapi? Hivi anayeuawa na Ukimwi ndiye mtu, ndiye binadamu, wa malaria sio binadamu? Tena Malaria inaweza ikatibika. Wanakufa mamilioni! Mahali pengine nchi za *tropics* wanazosema ndiyo mazalia ya mbu, wameshadhibiti mbu wamemaliza. Wakati mimi niko Darasa la Nne tulikuwa tunaua mazalia ya mbu. Tunawasaka, tunaweka mafuta ya taa kwenye vidimbwi, yaani inakuwa hiyo ndiyo dawa ya kuua mbu. Lakini leo hii hakuna kinachofanyika. Nunueni vyandarua! Anakula chakula bila chumvi chandarua atanunua wapi? *(Makofi)*

Jamani tuangalie mambo jinsi yalivyo. Haya tunajua maskini, mtu anakula mara moja kwa siku, anakuja kuugua, unamwambia hakuna chakula. Wakati sisi tunajua kwenye sayansi chakula ni sehemu ya dawa, huyu ametoka kwenye kula mlenda, ndiyo augue, hospitali waendelee kumletea mlenda, atapona huyo? *(Kicheko/Makofi)*

Hawapati chakula wagonjwa! Ni nchi yao, je, tulipatana jamani fukuzeni huyu mkoloni tule matunda ya uhuru, ndiyo haya ya kula mlenda hospitali? Serikali inasema mchangie. Hivi ni kuchangia, kwani hela yote mliyonayo Serikalini ni ya nani? Si ya hawa wananchi? Wewe umeweka ngapi bwana? Umeuza ng'ombe wangapi ukaweka kwenye mfuko wa Serikali? *(Kicheko)*

Walishachangia kodi, ukinywa soda kuna kodi, chumvi kuna kodi., wameshatoa wamejaza mfuko halafu unawaambia mchangie na nguvu zenu muweke. Wananchi tunawafanyia matatizo! Basi tutoze kodi mnayofikiri inatosha basi na sisi mtupe nafasi ya kufanya vitu vyetu nyumbani. Tutakuwa watumwa wa Serikali! Utumwa ni utumwa hata kama unatumikishwa na baba yako. Baba ulinizaa unitumikishe kwa kuwa eti ni baba! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi kwa jioni ya leo na mimi kutoa mchango mdogo katika hotuba ya Waziri Mkuu. Lakini kabla sijaendelea mbele kwanza nitoe mkono wa pole au pole kwa familia ya Marehemu Amina Chifupa na Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema Peponi. *Amina!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nitauelekeza juu ya udhibiti na ununuzi katika Serikali kwa taarifa ya Mamlaka ya Ununuzi Tanzania imeonyesha kuwa asilimia 70 ya bajeti inakwenda katika matumizi ya kawaida au manunuzi ya kawaida na asilimia 100 ya bajeti ya Serikali inakwenda katika shughuli za maendeleo ya ununuzi wa vifaa, huduma, kandarasi wa ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa hii, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwa taaluma inatolewa juu ya kuelewa jinsi gani kandarasi au taasisi zinafanya ununuzi, kaeleza vizuri sana katika hotuba yake hii. Kwa hiyo, jambo ambalo hivi sasa linatakiwa ni kusimamia tu hizi Taasisi ili kuzipa elimu zaidi kuhakikisha kuwa zinafanya manunuzi mazuri. Ukiangalia katika mfumo tulionao hivi sasa *PPRA* ni chombo ambacho kinasimamia manunuzi ya Serikali. Lakini tatizo kubwa ambalo lipo pale ni nyenzo za kufanyia kazi katika taasisi ile.

Kwa hiyo, nashauri kuwa katika chombo kile tukipe uwezo ili kihakikishe kinatoa hiyo taaluma au kinatoa uwezo kwa Halmashauri zetu au kwa taasisi zetu zinafanya vizuri. Kwa sababu jambo ambalo linafanya kuwa fedha ipotee kwa Taasisi au Halmashauri nyingi hazina taaluma ya ununuzi au ubinafsi au rushwa hazifuati tenda za ununuzi na mambo mengine ambayo yanasababisha pesa nyingi kupotea katika sekta hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo haja katika jambo hili kulifuatilia kuhakikisha kuwa *PPRA* inafanya vizuri ili kuhakikisha kuwa wanasimamia hizo fedha na hazipotei kwa wingi kama zilivyopotea miaka iliyopotea na zaidi kuziwekea sheria. Sheria ipo, lakini kama sheria ina mapungufu ifanyiwe marekebisho ili tuhakikishe kuwa sheria iliyopo inafanya kazi vizuri. Pia inaonyesha kwamba hawana jengo la kufanyia kazi. Taasisi hii ilifanya kazi zake vizuri, kwa hiyo, nashauri kuwa taasisi hii ipewe uwezo na nyenzo ili kuhakikisha kuwa inafanya vizuri kutoa taaluma ya ununuzi na ili fedha isipotee zaidi. Tuhakikishe kuwa mwaka unaofuatia ni mikutano, kubadilisha maholi ili kuhakikisha jinsi gani fedha zilivyopotea. Nafikiri tatizo litapungua katika hali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu kazungumzia kuhusu usalama na kauzungumzia vizuri tu. Mimi naongezea kuwa usalama katika nchi ni jambo la lazima, lakini tatizo kubwa ambalo linatukabili hivi sasa kuwaweka katika mazingira mazuri vyombo vyetu vya ulinzi. Juzi hapa lilijibiwa suala la nyumba za majeshi zitajengwa nyumba 100 kwa Zanzibar. Lakini tatizo kubwa ambalo linatukabili siyo nyumba wakati mwingine ni ukarabati wa nyumba zilizokuwepo, hazikaliki. Kwa hiyo, hili tuliangalie licha ya kujenga nyumba nyingine mpya. Lakini tuliangalie tatizo lingine ambalo

linatukabili hivi sasa, ni kufanya ukarabati wa nyumba zilizokuwepo na mfano mzuri ni kambi yangu ya Potoa iliyopo katika Kijiji cha Potoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo nyumba ambazo zimejengwa, lakini uwezo wa kukaa wanajeshi wa pale ni mdogo kwa sababu ukarabati wake unakuwa haufanyiki mara kwa mara. Kwa hiyo, ipo haja kuwa licha ya kujenga nyingine mpya, lakini tatizo hili tuliangalie katika mbinu nyingine ya kuhakikisha kwamba tunafanya ukarabati wa mara kwa mara. Tujenge utamaduni wa kukarabati nyumba zetu au kufanya ukarabati wa mara kwa mara uwe ni utamaduni, tusisubiri mpaka kitu ambacho kinavunjika ndiyo tukiangalie ambacho kitakuwa ni hasara zaidi kuliko kukifanyia ukarabati.

Suala lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu upande wa Polisi, Usalama wa Raia. Suala kubwa ambalo linatupata katika ukanda wetu wa Pwani hasa Nungwi, Pwani Mchangani, Kiwingu na Mwanginemu, ni matatizo ya usalama, wako Polisi ambao wanapelekwa kwa kufanya *patrol* tu wakimaliza kazi hiyo, inakuwa basi. Lakini ukimwambia, kwa kweli magari, kwa kweli tunashukuru yapo ya kutosha. Kwa hiyo, tunaishukuru Wizara ya Usalama wa Raia, niwashukuru sana kwa hili.

Lakini suala zima ambalo linaikabili Wizara hii ni mafuta. Unapowaambia wafuatilie suala fulani wanakwambia hawana mafuta na ni kweli hawana mafuta. Licha ya mafuta na hata pesa ambayo inatengwa kwa s*ervice* ya magari haipo. Kwa hiyo, ipo haja kuwa lazima tuhakikishe kuwa suala hili linafikiriwa, hili la kuweka nafasi ya mafuta, fedha ya mafuta na fedha ya ukarabati inapostahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kulizungumzia kuhusu Polisi, lazima ushauri ufanyike baina ya askari wadogo na wakubwa ambao wanatoa amri hizi. Tatizo ambalo linajitokeza Zanzibar hivi sasa ni michango ambayo wanachangishwa askari wa Zanzibar kuhusu michezo. Hili kwa kweli linazungumzika na wakizungumziwa wenyewe Polisi au askari wa vyeo vya chini linaweza likatatuliwa hili suala. Lakini kwa kweli ni kero juu yao na linachukua muda mrefu ili uongozi, Wizara na Uongozi wa Zanzibar wakae pamoja na wafanyakazi ili wahakikishe kuwa suala kama hili la michango ya wafanyakazi wanakubali kukatwa mishahara yao kwa kila mwezi au kwa kila mwaka kufanikisha mahitaji yanayohitajika. Lakini kumkata mshahara wake mtu bila idhini na wakati ambapo hajui matumizi yanakokwenda ni tatizo.

Halafu suala lingine ni suala la vyeo. Wanapopata vyeo hawafikiriwi, pale pale mtu anapopata cheo anaweza kukaa mwaka mmoja, miwili au zaidi hapandishwi cheo, hata akipandishwa cheo lakini maslahi yanabakia pale pale. Kwa hiyo, hiki ni kilicho cha wale ambao wanapata cheo lakini vyeo vyao ni vya kupigiwa saluti tu, hawana kingine ambacho kinaongezeka katika mishahara yao. Kwa hiyo, ipo haja hili liangaliwe kuhakikisha kwamba vyeo vinakwenda sambamba na posho ambayo inaendana na cheo alichopatiwa kama kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala ambalo nataka kulizungumzia kama lilivyozungumziwa ni udanganyifu wa mitihani. Hivi sasa kwa kweli wizi wa mitihani umepungua sana, lakini udanganyifu wa mitihani upo.

Lakini suala kubwa ambalo linawakabili ni tatizo kubwa la posho za maaskari ambao wanasimamia mitihani na wale wasimamizi wa mitihani. Sasa unakuta fedha ya usimamizi wa mitihani inachelewa sana au haifiki kwa wakati na haiwafikii walengwa. Askari wanalalamika kwamba fedha ambayo inatoka kwa Serikali kuwafikia wao ina mikono mingi. Kwa hiyo, tupunguze ile mikono ili iwafikie raia au askari ambao moja kwa moja wanalinda ile mitihani wakati ambapo wanafanya ile kazi. Hii ni kero ambayo wanailalamikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia, tunaishukuru sana sekta ya muungano, inafanya kazi vizuri sana, kwa mfano wamejenga majengo yao *BOT, TRA,* Ofisi ya Bunge, Uhamiaji na Taasisi nyingine. Lakini suala zima la kujiuliza Ofisi ya Makamu wa Rais itaanza lini? Hili ni suala la kujiuliza. Humu ukiuliza utaambiwa inaanza karibuni. Inaanza karibuni, lakini dalili na ishara mbona hazionyeshi? Tuonyeshe dalili basi tuvutiwe na hii hali kuhakikisha kuwa nayo Ofisi ya Makamu wa Rais pale Zanzibar inajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia ni suala la utamaduni na michezo. Hili ni suala ambalo kwa kweli ni kero kwa baadhi ya mambo yaliyoko katika nchi yetu. Hasa katika nchi tufanyie ukarabati wa viwanja vyetu ambavyo tunavyo licha ya kutosheka na kiwanja tulichojenga hivi sasa ambacho kinakidhi haja, lakini bado kinahitaji msaada wa viwanja vingine katika Mikoa tofauti. Lazima tufanye ukarabati wa viwanja hivi. Nashukuru sana, kiwanja chetu cha Taifa karibu kimalizike pale, lakini suala zima ambalo linajitokeza hivi sasa mmesikia kuwa nyasi za bandia zimekwama, hazijafika kwa sababu ya ushuru.

Hili ni suala ambalo Serikali ilizungumze ili tuhakikishe kuwa zile nyasi bandia zinapatikana na zinaweza zikafanya kazi katika Uwanja wa Taifa ili tuhakikishe kuwa mwezi wa Tisa timu yetu ya Taifa inapoingia pale inaingia kuhakikisha kuwa inafanya vizuri katika uwanja mpya wa kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhakikisha kuwa tunaibua michezo katika uraia. Limetokea suala zito hivi sasa na mgogoro mkubwa baina ya Chama cha Ngumi uraiani na Askari, mabondia kusafirishwa kwenda nje. Ni tatizo ambalo limejitokeza, inaonyesha kuwa uraiani wanamichezo hakuna na inaonyesha hamasa haipo kulinganisha na Jeshini. Kwa hiyo, ipo haja na uraiani tufufue michezo tuhakikishe kuwa wanapata michezo, wanashindana na majeshi ili kuhakikisha baadhi ya migogoro kugombea wachezaji ambapo inafikia wakati mashindano yanajitokeza, yaani wanamichezo ni wale wale wanatakiwa uraiani, wanatakiwa kwenye majeshi yetu. Kwa hiyo, ipo haja na uraiani tuhakikishe kuwa michezo inafufuliwa na inafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu lugha yetu ya Kiswahili. Kwa kweli lugha yetu ya Kiswahili kama ilivyozungumzwa katika kitabu chako hiki ni lugha lugha rasmi tumeamua na ni lugha ya Taifa. Lakini la kushangaza Tanzania Kiswahili ni lugha yetu rasmi, lakini matangazo

mengi Tanzania yaandikwa kwa Kiingereza. Sasa sijui urasmi wa lugha ya Kiswahili ukoje.

Kwa hiyo, nashauri kwamba ipo haja baadhi mambo yetu tuhakikishe kuwa tunafanya kwa lugha ya Kiswahili. Matangazo mengi tuandike kwa lugha yetu ya Kiswahili ili kila mwananchi aweze kuelewa. Lakini hata hivyo lugha yetu ya Kiswahili sasa hivi inapanuka sana na itapata soko sana kwa sababu wa Uganda wanataka kutafuta Walimu Tanzania wakasomeshe Kiswahili katika Shule zao za *Primary.* Kwa hiyo, ipo haja kwamba hii lugha ya Kiswahili tuikuze zaidi tuhakikishe kuwa inafanya vizuri na tuhakikishe kuwa inapata eneo kubwa na tunaitumia vizuri.

Lakini hata hivyo na sisi Watanzania wenyewe tuweke sheria na kanuni ya kutumia lugha ya Kiswahili. Lakini tunatumia lugha mbovu sana katika mazungumzo yetu ya Kiswahili. Ukiangalia humu Bungeni kwenye vyombo vya habari, kwenye taasisi nyingine, kwa kweli tunaitumia lugha katika mfumo ambao sio sahihi. Kwa hiyo, lazima na sisi Wabunge tubadilike, tusitawaliwe na vilahaja vyetu vya Mitaani. Hivyo, tuizungumze lugha yetu ya Kiswahili kwa ufasaha, kila mmoja aielewe, tunazungumzia lugha yetu ya Kiswahili ambayo ni ya kujivunia.

Vile vile tuhakikishe kuwa vyombo vyetu ambavyo vinakuza lugha ya Kiswahili kama BAKITA, TUKI, Taasisi ya Watu Wazima, BAKIZA Zanzibar tunavipatia nyenzo na tunawapata wataalam ambao watahakikisha kuwa wanaweza wakakikuza Kiswahili, kinaenea na kinapata soko nje na kinapata eneo kubwa na wazungumzaji katika ulimwengu huu tulionao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kulizungumzia ni mfuko wa Bima ya Afya. Mfuko wa Bima ya Afya kwa kweli unafanya vizuri na hivi sasa umeenea Tanzania nzima, lakini hata hivyo tuuboreshe na taasisi za Muungano zilioko Zanzibar, wafanyakazi wake wapata huduma ya mfuko huu ili na wao wajisikie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DUSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii niweze kuongea na kuchangia katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini kama ilivyo ada na kama walivyozungumza wenzangu na mimi kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu, ningependa kutoa salamu zangu za rambi rambi kwa familia ya Marehemu Mheshimia Amina Chifupa, Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema Peponi Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka kutoa pongezi nyingi sana kwa ofisi ya Waziri Mkuu kwa hotuba yao nzuri sana ambayo kwa kweli ina malengo mazuri ya kujikwamua Mtanzania wa hali ya kati na chini katika mwaka ujao wa fedha. Labda nianzie na uwezeshaji wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi hapa tumesikia Mheshimiwa Dr. Mzindakaya anaandamwa sana kuhusu kukopa kwake kutoka Benki. Lakini tukienda ukurasa wa kumi

na mbili wa kitabu cha hotuba ya Waziri Mkuu, itachukua sehemu chache tu, nanukuu: "Ukurasa wa 12 mwenye kitabu, Serikali ilidhamini mikopo ya mabenki kwa wananchi kupitia mifuko ya dhamana ya miradi ya muda mrefu na wakati, yaani *development finance guarantee facility*, inaendelea mfuko wa dhamana ya mikopo kwa ajili ya mauzo nje ya nchi *(export credit guarantee scheme).*

Sasa labda mtu kama amevaa miwani ya mbao hakusoma hii tunaweza kumwelewa vinginevyo, Dr. Mzindakaya ametumia fursa iliyo wazi tena sio ya mficho. Nani kati yetu hapa Mbunge ambaye hajakopa ambaye hadaiwi humu ndani amekopa benki? Nani, aonyeshe kidole! Amedhaminiwa na nani? Sio Serikali! Maana yake Bunge ni Serikali. Sasa haya mambo ya ajabu kabisa! Jamani, watu wanatisha, yaani wanaandikiwa humu lakini bado hawayaoni!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutumie fursa hizi, ziko waziwazi, hamkukataza Wabunge, watu kawaida na nani tutumie hizi fursa. Sasa mwenzetu ametumia hii fursa tunamwonea wivu. Hii ni hatari sana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki Kuu ilikuwa ni wakala na wakala huo ukahamishiwa *TIB*. Mimi nitapeleka maombi niwe wakala ninayefuatia, mwone mtakavyogawa hiyo mikopo kama pipi. Sasa sijui mtanuna mtakwenda kushitakia wapi sijui. Nitapeleka maombi niwe wakala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ilikuwa ni utangulizi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kwa niaba ya wananchi wa Nanyumbu niishukuru kwa kutujengea Makao Makuu ya Wilaya. Naishukuru sana kwa kweli. Makao Makuu imejengwa ingawa haijakwisha, lakini tunaona kazi ile inasuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu awaeleze wanaohusika kazi ile iishe haraka ili Mkuu wa Wilaya yangu ahamie kwenye ofisi yake, ahamie kwenye nyumba yake. *(Makofi)*

Pia naishukuru Serikali kwa kutujengea daraja la umoja Wilayani Nanyumbu. Daraja lile ni ukombozi mkubwa sana, litafungua milango ya uchumi Tanzania na nchi nyinginezo za Afrika Kusini. Nashukuru sana.

Vilevile ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa kampuni ya *CELTEL* kwa kutukomboa. Kule Kusini wametujengea minara pamoja na ule wa *TIGO*, lakini naomba watu wa *TIGO,* wamejenga pale bila kufanya mazungumzo na wananchi. Kwa hiyo, nawaomba sana wafanye ustaarabu wa kwenda kuzungumza na wale wananchi na kama kuna mrahaba wowote, basi waelewane kuwalipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ningependa sasa nije kwenye kuzungumzia mambo ya mikopo ya ujasiriamali. Ndugu zangu wa Nanyumbu wanalalamika sana kwamba hii mikopo haijawafikia walengwa na hasa wakulima na wajasiliamali wadogo wadogo. Nimefanya mikutano mingi tu pale Chang'ombe, Nawage na Lowasa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuna kijiji chako pale kinaitwa Lowasa naomba uje ukitembelee. Huko kote malalamiko ya wananchi ni kwamba mikopo ile haijawafikia bado, urasimu ni mkubwa sana na naomba kupitia kwako Benki ya *NMB* tawi la Masasi liongeze kasi ya kutoa ile mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ningependa kuja kwenye zao la korosho. Zao la korosho kwetu sisi Nanyumbu ni siasa. Mwaka jana tumepata tabu sana sisi Wawakilishi, Wabunge pamoja na Madiwani. Zao la korosho liliyumba sana, bei ilikuwa haieleweki, wanunuzi walikuwa wanasuasua, kwa kweli walituacha hoi sana. Naomba mwaka huu yale mambo ya mwaka jana yasirudie tena.

Kwa kweli tumepata tabu sana, maana unapita unakuta wananchi wamekaa nje na mizigo yao ya korosho, basi hata kusimama kuwasalimia unashindwa kwa sababu unaona sura zenyewe kabisa ni za huzuni, unashirikiana nao huku wana huzuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine linahusu pembejeo hasa ya *sulphur,* inachelewa sana kufika Wilayani Nanyumbu. Mwaka huu ndio kabisa! Sijui kama huko nyuma baada ya mimi kutoka kama hao wananchi wangu wameweza kupata hiyo *sulphur* kuweza kupulizia mikorosho!

Tatizo lingine ni kwamba anaeagiza hii *sulphur* ni mtu mmoja tu, *Abbas Transport.* Jamani, mbona kuna watu wengi kule Mtwara ambao wana uwezo wa kufanya hii biashara? Kwanini mmoja tu Abbas? Tunapata tabu sana! Samahani, huu umiliki wa mtu mmoja kufanya hii biashara ya *sulphur* inatuumiza sana wakulima wa korosho. Hiyo siwezi kusema sasa kwamba ni Mtwara tu, nafikiri Mikoa yote inayolima korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *export levy* nadhani mwenzangu Mheshimiwa Mkuchika amelizungumza, lakini na mimi niseme tu kwamba ile *export levy* ndiyo inayotucheleweshа sisi kufanya mambo yetu ya kulikuza zao la korosho. *Export levy* sio kwa sababu ya kununua *sulphur* tu, ni kuboresha miundombinu ya zao la korosho, ni pamoja na barabara. Maana yake sieleweki kwamba *export levy* ile ni kwa ajili ya pembejeo tu, hapana. Unaboresha zao la korosho!

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, naomba nizungumzie kuhusu elimu yote ya msingi pamoja na sekondari. Elimu ya msingi ina matatizo mengi sana, Mheshimiwa Kumchaya amezungumza hapa kwamba kuna matatizo ya walimu, Wilaya ya Nanyumbu iko pembezoni sana mwa nchi hii, ipo karibu na mpaka wa Msumbiji. Mwalimu ukimpanga kule anajiuliza mara mbili, niende au nisiende. Sasa tungependa tupate upendeleo jamani! Wilaya ya Nanyumbu hatuna Walimu mashuleni, shule ya msingi unakuta mwalimu mmoja, akienda kuchukua mshahara, basi shule inafungwa. Tafadhali tuoneeni huruma wenzenu wa Nanyumbu!

Kuhusu shule za sekondari, kwanza naomba nimpongeze sana Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, alikuwa mstari wa mbele kabisa kujituma mpaka

usiku kuhakikisha shule zinajengwa. Nataka nimpongeze vilevile *DC* wangu wa Wilaya ya Nanyumbu, yeye amesimamia kwa dhati, masuala ya utoro wa wanafunzi tunamwita Afisa Elimu wa Wilaya kule kwa sababu hajaletwa lakini yeye ndiye Afisa wa Elimu wa Wilaya, tunaomba sana tusaidiwe mambo ya Maabara. Hakuna vitabu vya Shule na walimu vilevile kuna tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna vituo vya afya vitatu, lakini vyote vitatu, Michiga na Nanyumbu havina magari ya wagonjwa, havina watumishi wa kutosha, wagonjwa wakipata rufaa kwenda Masasi Mjini wanachukuliwa kwenye matenga, wengine kwenye baiskeli. Sasa hii kwa kweli ni dunia ya ngapi? Tunaomba sana tusaidiwe magari ya wagonjwa, Michiga na Nanyumbu. Lakini pia tungependa kujua mkakati wa Serikali kuhusu hivi vituo vya Afya. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kweli ukitembelea kule kwetu Nanyumbu utaona hali ni kwa kiingereza *very pathetic,* yaani ni mbaya sana, hakuna watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuzungumzia masuala ya maji. Maji ni tatizo kubwa sana Wilaya ya Nanyumbu, akina mama wanapata tabu sana kutembea huko na huko kutafuta ndoo moja tu ya maji, wanaamka alfajiri pengine anasindikizwa na mumewe, huko chini kuna nyoka, kuna wanyama wakali kutafuta ndoo moja ya maji. Kuna tatizo pale Mangaka, Chitowe, Mkumbaru, Mkohora, kila mahali Nangomba, wana shida sana sana ya maji. Kwa hiyo, naomba ofisi ya Waziri Mkuu itusaidie Nanyumbu kutupatia maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu katika hotuba yake amesema hivi na mimi naomba nimalizie hapa: "Kama unataka kuwa na mtazamo mzuri wa maisha, msaidie mtu mwingine kupata ufumbuzi wa kero yake." Hivyo kama Serikali inataka kuwa na mtazamo mzuri wa maisha ya wananchi wake, basi tunaiomba hasa ofisi ya Waziri Mkuu itusaidie Wilaya ya Nanyumbu kupata ufumbuzi wa kero zetu. Tunakuomba sana, tuna kero nyingi sana, lakini naona tumesahauliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, Mheshimiwa Rais, alisema, namnukuu: "Serikali haitakubali msamaha wa aina yoyote ile utakaotolewa kutokana na mipango ya maendeleo kupendelea maeneo fulani ya nchi. Kuna mahali kuna upendeleo lakini kule kwetu upendeleo huo hatuna, hatupati, haufikishwi, ni matatizo makubwa sana. Tunaomba sana.

Hivi jamani mipango yote ya maendeleo mtuletee kule Nanyumbu, Lindi, Masasi, Tandahimba, Mtwara na sisi tujione kwamba ni Watanzania wengine na Newala nimekumbushwa hapa. Jamani sio kila kitu mnalundika huko huko kumoja tu, na sisi ni wananchi wenu vilevile! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache mimi naomba niishie hapo naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru wewe kwa kunipa fursa hii leo kuzungumza katika Bunge hili Tukufu.

Lakini kabla ya kuzungumza, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Chwaka, tunatoa pole kwa wale wote waliofiwa kwa msiba uliotokea katika basi la *Mohamed Enterprises* kule Singida. Lakini pia na Mbunge mwenzetu ambaye kwa kipindi kirefu tulikuwa naye hapa, ametangulia na sisi tuko njiani, kwa hivyo kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, ewe Mola wa haki uwasamehe mambo waliyotanguliza ya madhambi na waliyochelewesha na madhambi waliyofanya kwa siri na madhambi waliyofanya kwa dhahiri, *Amina!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka tulipoanza harakati hizi za kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu, kwa kweli nilijiandaa kwa mambo kama manne, lakini natumaini kwa leo na mjadala unavyokwenda naona sikuyamaliza. Kwanza hali ya kisiasa, Muungano, Ofisi za Jimbo na kama kawaida yangu habari ya UKIMWI sitasahau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mjumbe alisema hapa, kutokana na maafa na ikionyesha kama Mheshimiwa Waziri Mkuu hawajali, lakini sivyo, kinyume na taratibu zilivyo na mambo yalivyo. Chama cha Mapinduzi, hakichagui, hakibagui na wananchi wote wanajaliwa na Chama cha Mapinduzi bila ubaguzi, maafa yaliyotokea 2001, mimi nasema sio maafa. Kawaida ya maafa inaweza kuwa kimbunga, mafuriko, njaa, haya tunahesabu kwamba ni maafa. Lakini kama wananchi wamejipanga wakaona wafanye maandamo na kuchukua zana na kuelekea katika Kituo cha Polisi, baadaye wanakwenda na wanawaona kwamba wamechukua zana na wamefuatiliwa na wananchi wanajihami, halafu useme maafa! Sio kweli! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, linalosikitisha zaidi, Marehemu Mungu amlaze mahali pema, Dr. Omar Ali Juma, alipata tetesi hii na akawaeleza wananchi wake. Alitoka huku Bara na akaenda Pemba akawaeleza kwamba tendo hilo sio zuri. Leo mje hapa katika Bunge hili kudanganya wananchi walio nje mseme maafa! Haya sio maafa! Lakini kila lililokuwa maafa nasema Serikali hii inaongozwa na Chama cha Mapinduzi inawashughulikia wananchi wake.

Lakini mimi kwa upande mwingine pia sistaajabu. Leo mtu hapa anainuka anasema ambalo ni tendo baya kabisa, lakini kwa bahati tumeshasahihishwa, anasema sisi wa Pemba hatuna matatizo na Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Lakini mtu huyu huyu hajijui anatoka wapi! Hapa tumeungana, kuna Wajumbe wanatoka Tanzania Visiwani na kuna Wajumbe wanatoka Tanzania Bara, lakini kama umefika hapa ujijue kwamba wewe umekuja hapa kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na ndiko ulikofanya uchaguzi na ndiko ulikochaguliwa. *(Makofi)*

Lakini leo na Mheshimiwa Waziri kwa kweli, hawa watu jinsi mnavyowapenda sasa wanadeka! Mtoto kama unapenda kupita kiasi, basi badala ya kukuita baba atakuita *father*, kwa sababu anajenga imani kwamba sasa nikiwango kimoja kati ya yeye na wewe baba mtu, anasahau kwamba umemzaa. Ndiyo kiwango walichofikia wenzetu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashangaa sana, kwa sababu leo Rais wa Zanzibar anajulikana kikatiba, na amechaguliwa, wanakuja watu wanasema eti

hawamtambui. Kweli inaingia akilini? Wewe umetoka wapi? Hawa watu lazima tuwashughulikie. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. SAID ALI ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu. Kanuni ya 50(8)(d) ni marufuku kwa Mbunge yeyote kujiingiza katika mambo ya kuwasema wenzake au kuleta malumbano ya kisiasa ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msemaji anayechangia hoja sasa, anaelekea kuleta malumbano ya kisiasa ndani ya Bunge, jambo ambalo sio sahihi. Ni vyema akaelekea kwenye utaratibu wa kueleza kile alichonacho. Naomba mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Arfi, mpaka sasa hivi hujajenga hoja ikaeleweka kwa sababu hujasema hayo malumbano anayoleta ni malumbano gani. Kwa hiyo, inaipa ugumu Kiti kuweza kuamua jambo hili. Hujaijenga hoja ikaeleweka hasa ni jambo gani unalolisimamia. *(Makofi)*

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na umekomaa kazi yako. Kwa kweli kuna baadhi ya mambo tunawapotosha wananchi. Sisi tumechaguliwa na wananchi, wananchi mara nyingi wanawasikiliza viongozi wao nini wanachokizungumza. Kiongozi hana tofauti na Mwalimu. Sisi ni Walimu kwa wananchi walio katika Majimbo yetu. Sasa tunachokisema hapa kiwe cha ukweli na kiwe thabiti ili tusipotoshe Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulijulisha Bunge hili Tukufu kwamba alitajwa Mkuu wa Mkoa hapa Dadi Faki Dadi na hii ndiyo fursa ya peke ya kuizungumza. Huyu kijana ni hodari sana na hajali kwamba huyu ni mtu wa Chama Tawala, huyu ni mtu wa Upinzani. Tena ushahidi rasmi tunao, Mheshimiwa Maua Daftari anasaidiana naye vizuri kabisa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Maua Daftari ni shahidi, anatoa tena wengine wako katika Chama cha Upinzani, anasaidia na wale wote wanaotoka Pemba, hili suala wanalijua.

Kwa hiyo, wenzetu tunakuja hapa, tushirikiane letu liwe moja la kufanikisha maendeleo ya nchi yetu na maana ya kusema pale nyuma kidogo, kwa kweli wenzetu nasema hamuwaelewi. Hawa wenzetu mpaka sasa hivi wanakwenda na historia. Nataka kujulisha Bunge hili Tukufu kwamba historia ya Zanzibar sio ya Bara. Hili nataka lieleweke kabisa, lakini nashukuru sasa mnawaelewa. *(Makofi)*

Lakini tuna tofauti kubwa sana ya historia yetu na historia ya huku Bara iko tofauti. Huku wenzetu nchi hii mmeipata kwa kura. Zanzibar tumeipata kwa kumwaga damu na kihistoria, toka tunakotoka wenzetu wamejitenga. Mimi nashangaa sana, juzi Mheshimiwa kusema kwamba hali ya Zanzibar ngumu sana. Hii ni historia, bado wanaendeleza, ngumu sana na ndiyo tunafika kiwango hiki cha leo. Sisi tulitawaliwa na Waingereza na Waarabu, lakini nataka Mheshimiwa Waziri Mkuu ujaribu sana wakati unafanya majumuisho, hebu waangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa takwenda kuhusu …

**WABUNGE FULANI:** Bado, bado!

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza kuhusu 4.5. Kwa kipindi kirefu kwa kweli suala hili limehitaji marekebisho. Sisi wakati tunasoma kule shule, wazee wetu walitupa pesa mbili tu ya kwenda shule. Lakini leo mtoto hata umpe shilingi elfu moja kwa kweli haikidhi haja. Sasa tunaomba hapa yapite marekebisho, mkutane, mzungumze ili kuona kiwango hiki na kwenda na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la Majimbo. Imezunguzwa sana, lakini mimi binafsi katika uchaguzi ambao suala moja nililoulizwa ni hilo la Majimbo. Sasa na hili tunaliomba mtusaidie ili tupate Majimbo katika maeneo yetu tuweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni UKIMWI. Kipindi kilichopita hapa tulisema tuna idadi ya watu milioni 2.5 na watoto kama milioni 2.5 ni yatima. Juzi niliona katika Televisheni, alizungumza kwamba kuna wanafunzi kama 12,000 wamepata ujauzito. Sasa naiomba Serikali tufanye mipango kabambe ili kuhakikisha suala hili linaondoka na uwezo upo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza wanafunzi lazima wapate baadhi ya kipindi kupimwa mashuleni na mwanafunzi wakati ameonekana kwamba anafanya vitendo viovu afuatiliwe na kuweza kutaja nani aliyefanya kitendo kile. Suala hili kwa wanafunzi tunaweza kufanikisha mipango hii na yule ambaye anahusika achukuliwe hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna mpango wa kupima wananchi, kipindi kile walikuja wataalam Wizara ya Afya, lakini Wabunge tulikwenda watu kama 150 tu na sio wote waliopima UKIMWI. Sasa kiongozi ni mwalimu, kipindi hiki tunamwomba Waziri wa Afya atuletee wataalam waje hapa na tuhakikishe Wabunge wote wanapima UKIMWI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni suala la msingi sana kwa sababu leo itahakikisha wazi kwa wananchi kwamba hatuwi wa kweli. Sisi ni watu wa kuonyesha mfano na mimi mtu ni wa kwanza, nitakwenda naonyesha mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wote tupime UKIMWI, wataalam, Waziri wa Afya atuletee tupime UKIMWI. Kipindi kilichopita watu 150 na sio wote waliopima UKIMWI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja mia kwa mia. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Yahya Kassim Issa. Sasa namwita Mheshimiwa Teddy Louise Kasella-Bantu akiwa ni msemaji wetu wa mwisho. Karibu.

**MHE. TEDDY LOUISE KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kufunga dimba katika siku ya leo. Kabla ya kuendelea, kwa niaba yangu mimi mwenyewe na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Bukene naomba kutoa rambirambi kwa familia, ndugu na jamaa wa Marehemu Amina Chifupa. Vilevile kwa huruma yake Mwenyezi Mungu naomba roho yake ipate rehema kwa Mungu ipumzike kwa amani. *Amina!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasahau, naomba kuunga mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kufuatana na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 - 2010 ambayo tuliinadi na tukapata ruksa ya kuingia humu ndani kuwakilisha Majimbo yetu, napenda kuipongeza Serikali ya Awamu ya nne katika hotuba ya Waziri Mkuu hasa pale anaposema: “Mwaka huu hatutashughulika na kujenga Zahanati au Vituo vya Afya, tutashughulika zaidi na kupeleka vifaa na wataalamu kwa Zahanati zote tulizonazo hivi sasa na Vituo vya Afya.” *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni busara kwa Serikali ya awamu ya nne, ni lazima tupeleke vifaa kwanza kwa vituo tulivyonavyo vya afya, kwanza na Zahanati ili tunapofikiria mwaka 2008, bajeti inayokuja ndiyo tujikite tena katika kujenga Zahanati nyingine. Tukianza kujenga Zahanati nyingine, mwaka huu tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu. Kwa hiyo, napongeza sana busara na hekima za Awamu ya Nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ndugu zangu wa upande wa pili wa shilingi waone yaliyo kweli. Waswahili wanasema: “Mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujafikisha miaka miwili kamili tangu tumeingia katika Awamu ya Nne, lakini kwa mfano hai katika Jimbo langu la Bukene, nilipokuwa napata Ubunge kulikuwa na *Secondary School* tatu katika Kata tatu. Lakini sasa hivi kuna *Secondary School* 10 katika Kata 10 na Jimbo zima lina Kata 16 na zile sita zipo katika awamu ya mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuhakikishia kwamba mwaka kesho *Secondary School* zile nyingine za Kata sita zitakuwa tayari. Kwa hiyo, kutokana na hilo, napenda kuipongeza Serikali ya CCM ya Awamu ya Nne. Napenda kuwapongeza Watendaji katika Wilaya, *DC* na Mkurugenzi, *DED* na zaidi vilevile napenda kuwapongeza wananchi wa Bukene kwa kuchangia na kujikwamua kielimu. Hii ni katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi katika elimu kuondokana na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niende kwenye lile ambalo ni tatizo kubwa kwa wananchi wa Bukene. Wananchi wa Bukene waliahidiwa kupata umeme na waliahidiwa wakati Rais alipokuwa anapita kuomba kura, aliahidi umeme wa Bukene

pamoja na Ndala. Vilevile katika ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya, tulipitisha umeme huu katika bajeti inayokwisha mwezi huu. Lakini cha kusikitisha, tumepata katika bajeti hiyo ya sasa shilingi milioni 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini shilingi milioni 50 hizi ni kwa sababu zile shilingi milioni 900 na usaza zilizopitishwa kwenye bajeti ambayo tunaimaliza zilikwenda kwenye maafa na wananchi walielezwa wakaelewa. Nilikuwa nimezungumza na Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Naibu Waziri. Nimefuatilia kila mahali mpaka kwenye *TANESCO,* umeme vijijini, mikakati yote ya kupeleka *tender* imekwisha, kilichobaki ni fedha kutoa Hazina kupeleka *TANESCO* ili tuweze kupata umeme wa vijijini Bukene na Ndala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Bukene wanajua hili na kila nilipokuwa natoka nikipitapita kwenye Wizara ya Nishati na Madini nazungumza na Mheshimiwa Waziri, nakwenda Ubungo nazungumza na *TANESCO* vijijini kisha napeleka taarifa hii Bukene. Kwa hiyo, watu wa Bukene wanajua hicho! Cha kushangaza tumepata shilingi milioni 50 sasa hivi baada ya kuambiwa kwamba kila kitu, ule mradi wa mwaka jana ulikuwa unakwenda ku–*paste* kwa mwaka huu.

Lakini nimezungumza na Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri ameniahidi kwamba hizo pesa zinaonyesha kwamba mradi huo upo na mimi naamini kabisa kwamba kweli mradi huu upo. Kama vile mtu anapokuwa mgonjwa anataka kuchomwa sindano, na hata kama ugonjwa ule hauendi kwenye sindano, zamani walikuwa wanawachoma sindano ya maji na kwa imani mwananchi anapona. Kwa hiyo, nami kwa imani hiyo naamini umeme wa Bukene utapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba tu, tukiondoka hapa tuweze kufuatana na Mheshimiwa Waziri, maana Mheshimiwa Jenista Mhagama mwenzangu ameomba Naibu Waziri na tulikuwa wote katika mikakati hiyo ya kuomba umeme. Kwa hiyo, mimi naomba tuondoke na Mheshimiwa Waziri ili akanisaidie kueleza wananchi wa Bukene kwamba hii shilingi milioni 50 maana yake ni chanzo, lakini Waswahili wanasema: *"Chiruru si Ndondondo."* Naamini kabisa akieleza yeye watamwelewa zaidi kuliko mimi nikienda itakuwa ngumu kwa sababu watafikiria sasa Mama namna gani? Kila siku ni umeme na mimi nimewapa hadithi zote kadri inavyokwenda, lakini sasa naomba basi anisaidie kwenda kueleza. Kwa sababu hitimisho lipo tu kutoa fedha Hazina kupeleka *TANESCO* vijijini na basi tunagonga *goal* hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vilevile nizungumzie juu ya umwagiliaji na nionyeshe Serikali ya Awamu ya Nne ilivyo na kasi. Niliuliza swali Na.50 mwezi wa Nne kuhusu umwagiliaji kwa kufuatia ahadi ya Hayati Moringe Sokoine. Nafurahi kueleza kwamba kweli watu wameshafika pale katika *site* ya Kamahalanga. Wameshaweka zile *beacons* na hilo bwana limekuwa kubwa litafika katika Kata ya Mogwa. Wananchi wamefurahi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba, kama nilivyopewa katika jibu hilo kwamba bajeti yake itakuwa katika mwaka 2007/2008 ambayo tunaianza Julai, kwa hiyo,

tunaiomba basi Serikali iendelee baada ya hiyo kazi iliyoonekana na matumaini hayo waliyopewa wananchi wa Bukene hasa katika Kata ya Kamahalanga na Mogwa, basi waweze kutengenezewa bwawa hilo ili waweze kulima kilimo cha kisasa cha mpunga na tuweze kupata mazao kwa ajili ya chakula na mengine kuuzwa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Bukene lina historia ndefu ya mabwawa. Yapo mabwawa mengi na mimi naamini mabwawa hayo yatakarabatiwa au kufufuliwa kutokana na hesabu niliyoambiwa kwamba kama ni mabwawa madogo madogo ya shilingi milioni 90 mpaka shilingi milioni 200 yatafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali iweze kufanya mabwawa ya Ikindwa, Kisasiga, Mahene, Buhondo, Sojo, Ilalo na mengine yote ambayo pengine sikuyataja hapa kwa ujumla wao ili wananchi wa Bukene wapate kulima na tutakuwa tumetengeneza ajira kwa wananchi wengi kwa sababu asilimia 80 ya wananchi ni wakulima katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukishalima, basi tunategemea kupata usafiri kwa ajili ya kusafirisha mazao yetu kwenda katika masoko. Kwa hiyo, naomba basi Reli ya Kati inayotoka Mwanza - Bukene – Tabora isiishie Dodoma, bali iendelee kama zamani mpaka Dar es Salaam ili iweze kusaidia mazao hayo yafike Dar es Salaam na mazao hayo yaende mpaka Mwanza ili wananchi wa Bukene waweze kujikwamua kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuchelewa, kwa sababu bado nina dakika mbili au tatu, naomba kuzungumzia haraka haraka barabara ya kutoka Nzega – Tabora – Sikonge – Rukwa. Barabara hii ikitengenezwa pale itakuwa imeunga barabara ya kutoka Rukwa au Mbeya kupitia Sikonge kuja Tabora - Nzega na inaunga mpaka Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kuna mazao mengi sana yanayotoka Rukwa ambayo hayawezi kufika kwenye sehemu kama za kwetu, kuna wakati kunakuwa na mahindi mengi sana na sisi tunapenda kula ugali, kwa hiyo, tunahitaji mahindi ya Rukwa kutufikia katika sehemu yetu na kufika Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna samaki wengi sana kutoka Mwanza ambao wanaweza kuteremka mpaka Rukwa hadi Mbeya katika kubadilishana biashara. Kwa hiyo, naomba barabara hii itengenezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mawasiliano, naomba mnara wa Mwambali ambao umeshatengenezwa, hawaja-*bust* tu! Kwa hiyo naomba waende waka-*bust* ili wananchi wa Mwambali na wenyewe wapate raha katika mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vilevile katika sehemu ya Mwangoye hakuna mawasiliano, unapata mawasiliano pengine ukiwa katika duka au ofisi, ukitoka kidogo hupati mawasiliano. Kwa hiyo, naomba mnara uongezwe pale ili wananchi wa Mwangoye wapate mawasiliano.

Naomba vilevile pale Itobo kuna Mradi wa *TTCL,* tayari umekwenda, ila unakwama kwa sababu hauna jenereta. Naomba Serikali iweke jenereta pale ili wananchi wa Itobo na wenyewe waweze kupata mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa tukipata umeme, kilimo cha umwagiliaji na mawasiliano tutakuwa … *(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MHE. TEDDY LOUISE KASELLA-BANTU:**Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Teddy Louise Kasella-Bantu.

Waheshimiwa Wabunge kama mnavyofahamu, Mheshimiwa Spika akiongozana na ujumbe mzito wa Wabunge aliondoka jana mchana kwenda Dar es Salaam kutuwakilisha katika msiba mkubwa uliotupata kwa kuondoka kwa mwenzetu, natumaini jioni hii atakuwa amerudi.

Naomba tuwashukuru sana wale wote ambao wametuwakilisha kule wakiongozwa na Mheshimiwa Spika na namtambua Mheshimiwa Jenista J. Mhagama amesharudi pia na Wabunge wengi wamerudi japo wengine bado wako kule Lupembe Njombe ambapo inatarajiwa mazishi yatakuwa yamefanyika jioni hii ya leo.

Baada ya maneno hayo niwakumbushe tu kwamba, hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inaendelea mpaka keshokutwa, yaani Jumatatu, lakini kesho ni mwisho wa kuchangia.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa shughuli zilizopangwa katika orodha ya shughuli za leo zimekwisha mezani kwangu hapa, basi naomba kutamka kwamba naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 01:45 usiku Bunge liliahirishwa Mpaka siku ya Ijumaa,*
*Tarehe 29 Juni, 2007 Saa Tatu Asubuhi)*